SUPA JACKPOT
TZS. 1,034,905,195
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 4

**AJUZA** adaiwa kuuawa na mwanawe mwenye ulemavu


8 Nipashe Jumanne Oktoba 1, 2022
TOLEO MAALUMU
KATIKA KUADHIMISHA MIAKA 73 YA KUANZISHWA KWA JAMHURI YA WATU WA CHINA
HOTUBA YA BALOZI CHEN MINGJIAN KATIKA TAFRIJA YA MTANDAONI KATIKA MAADHIMISHO YA MIAKA 73 YA KUANZISHWA KWA JAMHURI YA WATU WA CHINA
Oktoba 1, 2022

UKURASA 8


# Nipashe

Jumamosi Oktoba 1, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581085

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Samia ashtuka 'Vumbi la Congo'









Rais Samia Suluhu Hassan

**ATAKA** utafiti tatizo nguvu za kiume, awa mbogo ma-DC kutofanya kazi kisa...

*Endelea ukurasa 2*

# Watuhumiwa watano ujambazi wauawa jaribio wizi kiwandani

UKURASA 3



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, Allan Bukumbi akionyesha kwa waandishi wa habari jana, sare za jeshi zilizokamatwa kwa watuhumiwa wa ujambazi waliotaka kuvamia kiwanda cha Daazhong, eneo la Changarawe, wilayani Mufindi usiku wa jana, ambapo watano waliuawa na saba walitoroka. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

UKURASA WA 11

## WATAKA HAKI ZA WAZEE KUWAMO MAONI YA KIKOSI KAZI CHA KATIBA

MJADALA wa Kitaifa wa masuala ya wazee, umetoa maazimio 10 ikiwamo kupendekeza haki za wazee ziwasilishwe...

## TEC yaonya Watanzania kwa unafiki wa kisiasa

UKURASA 3

**MICHEZO** **ZANZIBAR SASA YARUHUSU NGUMI** UK. 32 **KABWELA** UK. 7



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula (kulia), akipokea zawadi kutoka kwa Balozi wa India nchini, Binaya Srikanta Pradhan, wakati wa uzinduzi wa mkutano wa kimataifa wa kudumisha utamaduni kati ya Tanzania na India kwa kudumisha mashirikiano ya usalama wa bahari, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Rais Samia ashtuka 'vumbi la Congo'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TABIA ya vijana kutumia supu ya pweza, Vumbi la Kongo na ulaji wa chipsi mayai, imemshtua Rais Samia Suluhu Hassan, hivyo kuagiza wataalam kufanya utafiti wa tatizo la nguvu za kiume kwa kundi hilo ili kuepusha kuwa na taifa goigoi.

Akizungumza kwenye hafla ya utiaji saini mkataba wa usimamizi wa shughuli za lishe na tathmini ya sita ya mkataba wa lishe jijini hapa, Rais Samia alisema utafiti ufanyike ili kujua wamekosea wapi na kwa nini kuwapo na lishe mbovu kwa vijana.

"Kwa nini kunakuwa na 'gap' (pengo), tunakuwa na watoto ambao hawako vizuri kiafya wa kike na kiume. Je, haya ni masuala yaliyoingia ya mitindo, nataka niwe 'sixpack au niwe 'slim' (kupunguza mwili) nisizidi kilo ngapi nataka sijui mbavu ikae hivi. Kuna nini hapo?

"Kwa nini watoto wetu wako hivyo. Wakifika wakati wa kuwajibika kuzaa kuongeza jamii wanahangaika, mara supu ya pweza, mara sijui... tuna tatizo na mnalijua mnalificha.

"Watafiti fanyeni utafiti tena, na tatizo halisemwi ni siri linaumiza zaidi vijana wetu. Mara ndo hayo ninayoyataja, mara sijui vumbi la Kongo, mara sijui kitu gani. Lakini tatizo kubwa liko kwenye lishe.

"Watafiti tafuteni tunafanyaje watoto wetu wawe shababi waweze kuzaa watoto wenye afya. Matatizo yanayotokea twendeni jamii ni yetu, matatizo yetu sote twendeni kushughulikia.

Nasema haya kwa sababu ilishasemwa hapa tukiacha hali ikaenda hivi, tutakuwa na taifa goigoi, lenye watu lakini si rasilimali watu, ni watu ambao ni mzigo kwa taifa. Si watu ambao watazalisha kwa ajili ya taifa. Hatumjui mke nani na mume nani nendeni tukasimamie," alisema.

Rais samia alisema, chakula kikuu kwa vijana ni chipsi zege na juisi na wanajaza matumbo bila kuangalia kama inawajenga nguvu ipasavyo.

"Haikatazwi kula chips zege lakini, waelewe wanachokila ni nini pamoja na ugumu wa maisha. Na sisi tutengeneze mifumo ambayo hata akila chips na kuku, mafuta yaliyotumika ni yapi. Tuhakikishe mafuta yanayotumika na hivyo vinavyotumika," alisema.

**TATIZO LA VITAMBI**

Samia alisema, utafiti wa lishe uliofanyika mwaka 2018 unaonyesha wakati Tanzania inapambana na lishe pungufu, kuna tatizo la uzito uliopitiliza.

"Tuna vitambi, naona kila mtu anajichungulia tumbo lake. Tuna tatizo hilo pia wataalamu mnapaswa kulitekeleza. Niwape mfano nina kajukuu kabonge sasa ukimwekea lishe ile ukiidhibiti anawasubiri mmelala saa 5:00 usiku anateremka ngazi taratibu, anakula mtakuta sahani asubuhi yeye ameshalala. Kila unapojaribu wapi, nasubiri akue nimpeleke mchakamchaka apungue.

"Sasa tuna tatizo hilo wakati tunazungumzia lishe duni, udumavu, utapiamlo lakini tuna tatizo la uzito uliopitiliza inabidi tuufanyie kazi. Suala hili la lishe hatuna budi kuchukua hatua za dhati kukabiliana nalo kama zilivyoanza kuchukuliwa,"alisema.

**BAJETI ZA LISHE**

Alisema, fedha nyingi zimetumika kwenye semina na makongamano lakini hali ya lishe bado ipo vile vile.

"Tushughulikie lishe kuepuka kuwa na watoto matahila , na taifa goigoi, ni hasara kubwa kwa taifa, unagombana na mtu mara tano unamueleza haelewi unasema jeuri, kumbe maskini historia yake imefichwa na suti na tai aliyoivaa,"alisema.

Alisema, matumizi ya fedha za lishe bado ni tatizo hazifanyiki kwa malengo yaliyokusudiwa zingine zinaelekezwa kwenye posho na safari.

Samia, aliwaagiza wakuu wa mikoa kuhakikisha fedha inayopangwa kutekeleza masuala ya lishe zitolewe kwa wakati na kamati za lishe zilikuwa hazifanyi vizuri.

Pia, alimwagiza Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, kuwachukulia hatua wote ambao wametumia vibaya fedha za lishe kwa kuwa ni ukosefu wa nidhamu.

"Huna nidhamu kwenye matumizi ina maana unafanya hivyo hivyo na maeneo mengine. Waziri naomba ripoti nilinganishe maeneo mengine au utawakingia kifua nasubiri nione," alisema.

Alitaka taarifa za utekelezaji wa mpango wa lishe zitolewe kila robo mwaka kutoka kwa Waziri Mkuu.

**WATOTO MAZINGIRA HATARISHI**

Rais alisema, wimbi la watoto wanaoishi mazingira hatarishi ni kubwa ambapo kwa mwaka 2021 watoto 992,901 walitambuliwa na kupewa huduma mbalimbali za kukabiliana na lishe duni na utapiamlo.

"Kuna watoto wanaishi kwenye mazingira magumu na kukua kwao kuna kuwa kugumu na hawa ndio panya road wa baadaye kwa sababu kama anaishi mazingira hayo magumu ina maana atatoka nyumbani kwenda kujitafutia, hana elimu wala njia yoyote atakuwa mwizi na mwenye vitendo viovu.

"Tunapiga kelele 'panya road' tunawazaa wenyewe kwa hiyo twendeni. Waziri wa Maendeleo ya Jamii hili lako, twende tukakabiliane na hii hali tuwatambue na kuwasaidia," alisema.

## ... Aonya ma-DC kutofanya kazi kisa wanangoja mkeka

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, amewaonya wakuu wa wilaya ambao hawafanyi kazi wakisubiri kutangazwa kwa mkeka (uteuzi) na kuwaagiza wakuu wa mikoa kumpatia orodha yao.

Akizungumza jana jijini hapa kwenye hafla ya utiaji saini mkataba wa usimamiaji wa shughuli za lishe, Rais Samia alisema: "Nasikia hamfanyi kazi mnasubiri mkeka. Napata meseji naambiwa huku hawafanyi kazi wapo kama wamepigwa ganzi. Nikute mkuu wa wilaya amepigwa ganzi.

"Nilisema nitawapima kwa utendaji kazi wenu, sikusema kwamba nitawabadilisha leo na kesho nimesema tumefanya performance (utendaji kazi) tumeangalia nani mzuri nani mbaya. Aliyesema anataka kuwabadilisha ni nani?, alihoji.

"Wakuu wa wilaya nchi nzima fanyeni kazi zenu. Kutoa mkeka ni kazi yangu na nitatoa wakati ninaoona mwafaka, sasa hivi kwenu ni kufanya kazi. Wakuu wa mikoa nataka ripoti za wakuu wenu wa wilaya, aliyepigwa ganzi nani, mwenye nusu kaputi nani. Kama hawawezi tutoe tuweke wengine. Nataka ripoti za wakuu wenu wa wilaya leo jioni (jana)," alisema.

Kuhusu lishe alisema Rukwa ni miongoni mwa mikoa iliyofanya vizuri huku Mara ikiwa imefanya vibaya zaidi na kwamba mikataba ya lishe waliyotia saini ni silaha katika kupima utendaji kazi wao.

"Wakuu wa mikoa nimewaona leo na sitaki kuwaacha saa 11 jioni (jana) tukutane Chamwino kuna mambo ya kushikana masikio, tuyafanye kwa mmoja mmoja," alisema.

**UJENZI MADARASA**

Rais alisema ameshatoa Sh. bilioni 160 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 8,000 ya shule za sekondari na ifikapo Januari, mwakani, hataki kusikia kuna eneo mtoto hajaenda sekondari kwa uhaba wa madarasa.

"Niliomba tathmini nikaletewa madarasa 8,000 nimefanya bajeti Sh. bilioni 160 tayari nimeshatoa kwa hiyo wembe ule ule tuliofanya mwaka jana tufanye mwaka huu. Nyie ni jeshi kubwa makatibu tawala wa mikoa, wakuu wa wilaya mkasimamie halmashauri kupitia 'force account' madarasa yatajengwa na yawe na ubora," alisema.

Katika hatua nyingine, Rais alisema hatavumilia kuona kifaa tiba baada ya miezi sita au mwaka mmoja hakifanyi kazi na atawabana walioagiza na watumiaji.

"Nitataka wanieleze kwa nini kifaa muda mfupi kimekaa pembeni. Nihimize mafunzo kwa wataokwenda kutumia vifaa hivi, wapate mafunzo ya kutosha ndipo waende kutumia hivi vifaa, hivyo hakuna sababu ya kuharibika, kinatakiwa kisiharibiwe kwa uzembe," alisema.

Awali, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, alisema Rais amezindua magari 52 ya maofisa elimu wa wilaya.

Naye, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alisema udumavu umepungua kutoka asilimia 34 hadi kufikia asilimia 32 kwa mwaka 2018/19 sawa na watoto wenye umri chini ya miaka mitano milioni tatu, hawafundishiki, hawaelewi na si wabunifu.

Alisema Wizara itaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwamo utoaji wa matone ya vitamin, madini na virutubishi vya madini kwenye vyakula.

# TEC yaonya Watanzania unafiki wa kisiasa

**Na Romana Mallya**

KATIBU Mkuu wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Padri Dk. Charles Kitima, amesema Watanzania karibu wote wamekuwa na unafiki wa kisiasa kwa kutoyasemea mambo ya haki za binadamu.

Kutokana na tabia hiyo, Dk. Kitima ametahadharisha kuwa jambo hilo litaharibu na kuliua taifa.

Padri Kitima alisema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati wa mkutano uliohusisha viongozi wa dini walio chini ya Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT) na TEC.

Katika mkutano huo, pamoja na mambo mengine, kilizinduliwa kitabu chenye jina la 'Elimu ya Haki za Binadamu' kwa lengo la kusaidia watu kujua namna ya kulinda uhai wa mtu.

"Unafiki unaharibu nchi. Unafiki wa kisiasa uliopo miongoni mwa Watanzania kupenda kusifia viongozi ili tu kujipendekeza wapate vyeo utaliua taifa na tatizo hili linaendelea kwa sababu watu hawajui misingi ya haki za binadamu," alisema.

Padri Kitima alisema endapo tabia hiyo haitakomeshwa itasababisha uhusiano mzuri miongoni mwa Watanzania kupotea.

Alisema Watanzania karibu wote wamekuwa na unafiki wa kisiasa kwa kuwa mambo ya kisiasa hawayasemei kama haki za binadamu zinavyotaka, bali kadri ya maslahi wanayotarajia kutoka kwenye mfumo wa jamii kisiasa.

"Hatuongozwi na haki za binadamu, tunaongozwa na maslahi binafsi, hii ndiyo inayoharibu nchi, utamaduni wa haki za binadamu ndiyo utarekebisha haya yote," alisisitiza.

Kuhusu Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu iliyoko Arusha, alisema Tanzania kujiondoa huko wakati ni kinara wa ukombozi Bara la Afrika ni unafiki wa kisiasa.

"Tuna maslahi binafsi ambayo tunatafuta ambayo hatutaki yaongozwe na haki za binadamu, kama kosa tumelifanya tujirudi, ndiyo maana viongozi wetu daima wanasema tubuni na rudini kwenye njia ya mwenyezi Mungu, rudini kwenye ukweli wa haki za binadamu.

"Kwa hili Tanzania tuna kosa kubwa sana, tulikuwa mfano wa ukombozi wa Bara la Afrika, tunakuwa mfano mbaya wa kutoheshimu haki za bindamu, kwa sasa serikali imefungua milango ya kujirekebisha, tujirekebishe," alisema.

Kuhusu vitendo vya ukiukaji wa haki za binadamu na baadhi vikifanywa na viongozi wa dini, Padri Kitima alisema wamekuwa wakilisimamia hilo na inapotokea kiongozi wa dini amehusika kuvunja, huwajibishwa kwa mujibu wa sheria.

"Ikivunjwa na mtu yeyote, haki za binadamu hatuangalii wewe ni Waziri, wewe ni Padri, wewe ni kiongozi wa serikali ya mtaa. Tunaangalia utaratibu wa kisheria ukoje kuhusu mtu kupata haki yake. "Lengo letu ni kuhakikisha uelewa unamfikia kila mtu kujua kwamba binadamu yeyote anaweza kuvunja haki za binadamu, kama vile tunavyotaka binadamu yeyote aziheshimu, na tusione kwamba mtu kuwa kiongozi wa dini yeye ndiye amekuwa kama Mungu, hapana.

"Yeye ni balozi wa Mungu lakini wakati mwingine anaweza kufanya matendo kinyume na ubalozi wake, kwa hiyo atawajibishwa kama sheria zinavyolinda haki za binadamu," alisema. Akizungumzia mkutano huo, alisema ni mkakati wa uliokusudiwa na viongozi wa dini kueneza elimu ya haki za binadamu katika ngazi za familia, lengo ni kuwafanya watu wawe na uelewa kuhusu haki za binadamu ili watimize majukumu yao kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake wa Wakiislamu Tanzania (JUWAKITA) walio chini ya BAKWATA, Hajjat Shamim Khan, alisema Tanzania ina watu milioni 60 na wanawake wako zaidi ambao ni asilimia 51 na wanaofuata dini ni asilimia 80.

Alisema katika suala la haki za binadamu, wanawake ndiyo wahanga wakubwa katika matukio ya ubakaji na ulawiti katika ngazi zote kuanzia vijijini.

Askofu Mkuu wa Kanisa la Mennonite Tanzania na Mwenyekiti wa Kamati ya Dini mbalimbali kuhusu haki za kiuchumi na maadili ya uumbaji (ISCEJIC), Nelson Kisare, alisema kitabu hicho kimetengenezwa kwa lengo la kutoa elimu.

"Matumaini yetu, jamii ya Watanzania kila mmoja kwa ngazi zote wakipata elimu na kujua haki yake ya msingi, ambayo ya kwanza ni haki ya kuishi, hakuna binadamu yeyote anatakiwa akunyang'anye kuishi kwako isipokuwa kwa mujibu wa sheria, ukishtakiwa mahakamani majaji wamepewa uwezo wa kumhukumu mtu," alisema.

## Watuhumiwa ujambazi wauawa wakijaribu kuvamia kiwandani

**Na Waandishi Wetu**

JESHI la Polisi Mkoa wa Iringa, limewaua watuhumiwa wa ujambazi watano kati ya 12 wanaodaiwa kuvamia usiku wa manane kutaka kupora fedha na mali.

Watuhumiwa hao wanadaiwa kufanya jaribio la uporaji na wizi katika kiwanda uchakataji wa mazao ya misitu cha Daashong, kilichoko kata ya Changarawe, Mafinga wilayani Mufindi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, Kamishna Msaidizi (ACP) Allan Bukumbi, alisema watuhumiwa hao waliuawa wakati wa majibizano ya risasi baina yao na polisi.

Kamanda Bukumbi alisema watuhumiwa hao walikutwa na mabegi mawili ndani yakiwa na sare za Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT).

Alisema tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia jana majira ya saa 8:00 usiku baada ya wahalifu hao kufika kwenye kiwanda hicho kwa lengo la kuvamia na kuiba. Bukumbi alisema Jeshi la Polisi lilipata taarifa kutoka kwa raia wema kuwa kuna watuhumiwa wa ujambazi wanapanga njama ya kwenda kuvamia kiwandani hapo usiku ndipo mtego ulipowekwa.

"Polisi waliwataka wahalifu hao kujisalimisha lakini walikaidi amri na kuanza kuwarushia polisi risasi. Baada ya majibizano ya risasi, wahalifu watano walijeruhiwa na wengine saba walitoroka. Walifariki dunia wakati wakipelekwa Hospitali ya Wilaya ya Mufindi mjini Mafinga," alisema.

Kamanda huyo alisema katika tukio hilo, wamepata silaha mbili aina ya Shotgun na Pump Action pamoja na mabegi mawili.

"Ndani ya begi moja kulikuwa na sare za Jeshi la Wananchi Tanzania na risasi 13 za shotgun. Begi la pili lilikuwa na sare za JKT, jaketi moja la mtumba linalofanana na kombati ya jeshi, shoka moja na kitambaa kimoja kinachofanana na kombati ya jeshi.

Pia alisema wamekuta laini mbalimbali za kampuni tofauti za simu, Tigo zikiwa 12, Airtel 25 na Vodacom saba.

"Tunawashukuru wananchi wote wanaoendelea kutoa ushirikiano kwetu kwa kufichua uhalifu na wahalifu. Tunawataka wote wanaomiliki silaha kienyeji kusalimisha silaha zao vituo vya polisi," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Mufindi, Saad Mtambule, amelipongeza Jeshi la Polisi kwa kazi hiyo na kueleza kuwa ndani ya wiki hii, kumekuwa na matukio mfululizo ya uvamizi wa kutumia silaha.

Alisema kuuawa kwa washukiwa hao wa ujambazi ni hatua kubwa ya kupambana na uhalifu wilayani humo.

Mtambule alisema tayari wenyeviti wa serikali za vijiji wamepewa maelekezo ya kuanza misako ya kuwafichua wageni wote ambao hawatambuliki

**Imeandaliwa na Francis Godwin na Martha Sambo (Iringa)**




# Ajuza adaiwa kuuawa na mwanawe mwenye ulemavu

**Na Elizabeth John,** Njombe

MKAZI wa Idofi, Makambako mkoani Njombe, Elina Nzilano (87), amefariki dunia baada ya kudaiwa kupigwa na mtoto wake mwenye ulemavu wa macho, Elisha Mwema (42).

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Kamishna Msaidizi (ACP) Hamisi Issah, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa mtuhumiwa huyo wa mauaji anashikiliwa na jeshi hilo. Kamanda Issa alitaja sababu ya bibi huyo kupigwa na mtoto wake ni baada kumzuia mjukuu wake ambaye ni mtoto wa mwanawe, kula chakula baada ya kuiba kuku kisha kumchinja na hatimaye kumla bila ya kushirikiana na mtu yeyote.

Alisema baada ya bibi kumzuia mjukuu wake, mtuhumiwa alichukua fimbo yake na kuanza kumshambulia mama yake mzazi.

"Huyu ni mtu mzima, hawezi kujitetea kwa lolote, hivyo alimpiga na kumjeruhi kisha kumpeleka hospitalini. Hakuweza kukaa hata siku mbili, madaktari walijitahidi kuokoa maisha yake lakini akafariki dunia," aliisema.

Wakati huo huo, Jeshi la Polisi mkoani hapa linawashikilia watu 11 kwa tuhuma za kuhusika na jaribio la wizi katika mradi wa ujenzi wa chuo cha ufundi (VETA) kilichoko wilayani Ludewa na kusababisha kifo cha mlinzi Romanus Mkinga, ambaye ni miongoni mwa wanaolinda mradi huo.

Alisema kundi la vijana linadaiwa kuvamia eneo hilo usiku na kuanza kuwashambulia walinzi hao kwa vitu vyenye ncha kali na kuwasababishia majeraha maeneo mbalimbali ya mwili.

Alisema mlinzi mwingine, Edwin Mwapinga, alikimbia na kumwacha mwenzake akishambuliwa na kundi hilo hadi kufariki dunia.

Akisimulia tukio hilo lilivyotokea, mlinzi Mwapinga aliyenusurika kuuawa alisema lilitokea saa nane usiku na wakati akikimbia alisikia mwenzake akipiga kelele za kuwa anakufa.

"Mwenzangu alikuwa akipiga kelele akilitaja jina langu akiomba msaada, 'mwenzio nakufa' nikawa ninakimbia kufika kule sauti za kuomba msaada zikawa zimekata," alisimulia.



Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Prof. Mark Mwandosya (katikati waliokaa), akiwa katika picha ya pamoja na wajumbe na watumishi wa EWURA na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA CCC), alipotembelea baraza hilo, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. Wengine (kutoka kushoto waliokaa) ni Makamu Mwenyekiti wa Baraza hilo, Anna Mungai, Mwenyekiti wa Baraza, Mhandisi David Ngula, Makamu Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Ahmad Kilima na Mjumbe wa Baraza, Baruany Luhanga na (watatu kushoto waliosimama) ni Mjumbe wa Bodi hiyo, Richard Kayombo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mtoto wa mwezi mmoja afanyiwa upasuaji kichwa

**Na Mary Geofrey**

MTOTO Sinaini Kalokole mwenye mwezi mmoja, amefanyiwa upasuaji kuondoa tatizo la kichwa kikubwa, katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Mtwara kwa ushirikiano kati ya madaktari bingwa wa Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI) pamoja na hospitali hiyo.

Upasuaji huo ni sehemu ya kambi ya matibabu ya siku tano ambayo inaendeshwa na madaktari, wauguzi na wataalamu wa MOI kwa kushirikiana na wenzao wa hospitali ya rufani ya kanda na hadi sasa zaidi ya wagonjwa 600 wamehudumiwa.

Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Ubongo, Mgongo na Mishipa ya Fahamu wa MOI ,Dk. Maxigama Ndossi, alisema mtoto huyo alifikishwa katika kliniki na kubainika kuwa na ugonjwa wa kichwa kikubwa.

"Leo tuko hapa katika vyumba vya upasuaji vya hospitali ya rufani ya kanda kusini na tumefanikiwa kwa mara ya kwanza kufanya upasuaji wa kichwa kwa mtoto wa mwezi mmoja. Upasuaji umekwenda salama na mtoto yuko salama kabisa na amepelekwa wodini. Tulimwona kliniki na tukabaini anahitaji upasuaji, hivyo tumefanikiwa kumfanyia upasuaji wa kichwa," alisema Dk. Ndossi.

Alisema mzazi wa mtoto huyo alishakata tamaa kwa sababu hakuwa na uwezo wa kusafiri kwenda Dar es Salaam kufuata huduma ya upasuaji.

Dk. Ndossi alitoa wito kwa wakazi wa mikoa ya kusini kuendelea kujitokeza kwa wingi kupata huduma katika hospitali ya rufaa ya kanda kusini kwa sababu wataalam wapo na serikali imeweka vifaa vya kisasa katika hospitali hiyo mpya na ya kisasa.

Alisema taasisi ya MOI imekua ikitekeleza kwa vitendo agizo la serikali la kuhakikisha huduma zake za kibingwa zinasogezwa karibu na wananchi.

# Ukaguzi zabuni PPRA waokoa bil. 13.9/-

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

UKAGUZI maalum uliofanywa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) kwa taasisi 11, zilizokuwa na zabuni 98 na mikataba midogo (LPO) 582 ya bidhaa yenye thamani ya Sh. bilioni 202.33, umesaidia serikali kuokoa kiasi cha Sh. bilioni 13.87.

Aidha, ukaguzi huo pia ulipima uwezekano wa kuwepo kwa viashiria vya rushwa katika taasisi au miradi ya umma.

Kati ya taasisi 232, zilizofanyiwa ukaguzi, 30 zilionekana kuwa na viashiria vya rushwa, hivyo ripoti za ukaguzi za taasisi hizo, zitapelekwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), ambayo ndiyo yenye dhamana juu ya masuala ya rushwa.

Kutokana na hali hiyo, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Hassan Chande, ameitaka Mamlaka hiyo kutomfumbia macho mtu yeyote bali hatua kali za kisheria zichukuliwe kwa kila atakae bainika kufanya ubadhirifu.

Naibu waziri huyo, alibainisha hayo jana jijini Dodoma mara baada ya kupokea ripoti ya tathimini ya utendaji wa Mamlaka hiyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2021/22.

Alisema bado kuna taasisi za umma ambazo hazifuati sheria ya ununuzi wa umma, hivyo kurudisha jitihada za serikali ya awamu ya sita nyuma.

Chande alisema mamlaka hiyo inapaswa kuzichukulia hatua taasisi hizo bila kujali zinaongozwa na kiongozi gani.

"Mwenyekiti wa bodi nimesikia hata kwenye taarifa yako kuna vitu kama hujaviweka wazi ni lazima utoe kila kitu unachokijua kwani kuficha ubadhirifu na wewe unaweza kuonekana ni sehemu ya ubadhirifu huo.

"Mwenyekiti taasisi zote ambazo hazifuati sheria za ununuzi usiwe na uvumilivu na mbadhirifu" alisema Chande.

Pia alisema serikali haitamfumbia macho mtu yeyote ambaye atajihusisha na vitendo vya ubadhirifu kwa kukiuka sheria na kanuni za ununuzi wa umma.

"Haya mambo ya rushwa katika manunuzi kipindi cha nyuma yalikuwa yamepungua, lakini sasa kama kuna watu wameanza kubipu sasa wanao bipu wapigieni na kama hamna hela ya vocha wizara ya fedha itawapa vocha.

Awali Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya PPRA, Dk. Leonada Mwagike, alisema ripoti aliyoikabidhi ni ya 16, tangu Mamlaka hiyo ilipoanzishwa.

Alisema ripoti hiyo inatoa tathmini ya utendaji kwa kuelezea majukumu mbalimbali yaliyotekelezwa na Mamlaka katika mwaka wa fedha 2021/22.

Alisema katika kuboresha huduma kwa wateja, PPRA imeanzisha dawati la huduma kwa wateja lenye lengo la kutoa msaada kuhusu huduma mbalimbali zinazotolewa na Mamlaka kupitia dawati hilo.

# DC aipongeza GGML kwa kuajiri Watanzania asilimia 98 mgodini

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

MKUU wa Wilaya ya Nyang'wale, Jamhuri William amesema uongozi wa Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGM) umeitoa kimasomaso Serikali ya Mkoa wa Geita katika ufadhili wa maonyesho ya teknolojia ya madini tangu yalipoanzishwa miaka mitano iliyopita.

Pia ameipongeza kampuni hiyo kwa kutoa fursa za ajira kwa watanzania, akibainisha kuwa zaidi ya asilimia 98 ya waajiriwa wote wa kampuni hiyo iliyoanza shughuli za uchimbaji wake rasmi hapa nchini mwaka 2000 ni wazawa.

Mkuu huyo wa wilaya alitoa pongezi hizo jana mjini Geita alipotembelea mabanda yaliyopo katika Maonyesho ya Tano ya Kitaifa ya Teknolojia ya Madini Geita na kufanya majumuisho katika banda la GGML kwenye viwanja vya Bombambili mjini hapa.

Alisema katika kipindi cha miaka mitano GGML wameshiriki maonyesho hayo lakini pia wamekuwa wadhamini wakuu na kufanya kazi kubwa ya kuboresha maonyesho hayo.

"Niwapongeze na kuushukuru uongozi wa GGML kwa kazi kubwa wanayoifanya katika mkoa wetu wa Geita. Kwa kweli wametutoa kimasomaso na tunaendelea kuwashukuru na kuwasihi tuendelee hivyo hivyo," alisema.

Mkuu wa wilaya alikumbusha kuwa kipindi fulani wakati madini yakiwa chini ya ardhi, Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Nyerere alizuia kuchimbwa mpaka watanzania wawe na uwezo na teknolojia sahihi ya kuyachimba ili yanufaishe wananchi.

"Tumeona wafanyakazi wengi wa GGML ni Watanzania wenzetu, tena ni mahiri kabisa katika kusimamia hii sekta ya madini kwani katika kila sekta wapo Watanzania wanasimamia, hivyo ni muhimu wananchi kushiriki katika tasnia hii ya madini," alisema.

Kiongozi huyo alisema maonyesho ya mwaka huu ni mazuri kwa sababu yamejumuisha wadau wengi zaidi ya 600 kutoka kampuni mbalimbali za madini na wadau wake.

"Niwashukuru wadau wote ambao wamejitokeza kuleta bidhaa kwa ajili ya maonesho haya. Nitoe wito kwa wananchi wa Geita na mikoa jirani kujitokeza kwa wingi kuja kuona teknolojia mbalimbali za madini na uzalishaji mali ambazo zitasaidia kuboresha maisha yao.

"Pia nimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kutoa fursa kwa Mkoa wa Geita kuonyesha dunia nini ambacho tunaweza kufanya, tumejaliwa bidhaa za kilimo, madini na shughuli mbalimbali za kiuchumi, ni muda mwafaka kwa watanzania kutoka sehemu mbalimbali kuja kuwekeza katika Mkoa wa Geita kwani fursa zipo," alisema.

Awali Meneja Mawasiliano wa Kampuni ya GGML, Stephen Mhando mbali na kumkaribisha mkuu huyo wa wilaya katika banda hilo kuu la GGML, pia alimweleza kampuni hiyo imetekeleza kwa vitendo maboresho ya sheria ya madini ambayo inatoa nafasi kwa wazawa kushiriki mnyororo wa shughuli za uchimbaji wa madini.

Alitolea mfano baadhi ya kampuni hizo kuwa ni pamoja na African Underground Mining Services (AUMS), ambayo inahusika na kutoa huduma za uchimbaji na uendeshaji wa migodi hasa chini ya ardhi (underground) kwa GGML.

Pia akiitaja Kampuni ya Blue Coast Investment Limited ambayo ni mmoja wa makandarasi watoa huduma wa kampuni ya GGML.

# Gambo asema hatishiki

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MBUNGE wa Arusha, Mrisho Gambo, amesema hatishiki na mchezo mchafu unaofanywa na baadhi ya viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoani hapa dhidi yake ili kumdhoofisha kisiasa.

Gambo amesema, watu hao wanaendesha mchezo mchafu wamejaa unafiki na usaliti dhidi yake katika mapambano dhidi ya ufisadi.

Alisema kauli hiyo juzi wakati akizungumza na wafanyabiashara wa soko la Krokoni jijini hapa, alipokwenda kukabidhi matofali na mabati kwa ajili ya ujenzi wa choo katika soko hilo.

Alisema kamwe hatarudi nyuma katika kupambana dhidi ya ulaji wa fedha za umma katika Halmashauri ya Jiji la Arusha hata kama atabaki peke yake katika mapambano hayo.

"Wako watu wachache hapa Arusha ambao wameweka genge lao kwa ajili ya kupiga dili na kufanya ufisadi na wizi wa fedha za halmashauri yetu, suala ambalo nimelikataa.

"Kuna baadhi ya watu wanasema mbunge haelewani na viongozi wenzake. Nataka wananchi wenzangu waelewe hata ashuke nani hapa hatuwezi kuelewana na watu wanaotetea wezi

"Jimbo la Arusha Mjini si jepesi, lina watu wanaojielewa itafika mahala wananchi wataamua kuchagua mtu na si chama," alisema.

Alitolea mfano kwamba kuna mtu amekwenda halmashauri na kuiba fedha Sh. milioni 103 badala ya kuungana kutetea maslahi ya umma, wako watu wanaungana kutetea mafisadi.

"Wakati Rais Samia (Suluhu Hassan), anapambana na ufisadi kwenye nchi na kutafuta fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo, serikali yake inawakamata wahalifu lakini leo hii wako viongozi katika mkoa huu wanamtembelea mhalifu gerezani," alisema.

Aliongeza kuwa, kitendo kama hicho kinachofanywa na viongozi hao ni kuidharau serikali na mamlaka zake inayopiga vita dhidi ya ufisadi.

Gambo, aliapa kuendelea kupingana hadharani na viongozi wa namna hiyo ambao wamejikita kuendeleza wizi na ufisadi ila atashirikiana na viongozi wenye nia njema na jimbo la Arusha Mjini.

Alisema watu wote wanaosimamia haki wamekuwa na misukosuko mingi na yeye akiwa mbunge wa miaka mitano akisimamia wezi na kulinda maslahi ya wananchi na kusema hatakaa chini kamwe kumsujudia mtu ili awasaliti wananchi.

Alionya kikundi cha watu wachache ndani ya CCM wanaoendelea kumpiga vita, kamwe hakitashinda yeye ni mbu ge wa wananchi na ataendele kusimama na wananchi .

## NOTISI / TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD ,YARDLEY RECOVERIES AUCTION LTD,** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya benki ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| ARUSHA | MARY WILLIAM KESSY | 1.NYUMBA YENYE HATI NO.177686 KIWANJA NA.68 KITALU 'J' 2.NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO | 1.JOHN EUDES RUHANGISA 2. JOHN EUDES RUHANGISA NA MARY WILLIAM KESSY | 1. KINYEREZI ILALA 2.OLASITI ARUSHA | 17/10/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| DODOMA | SELEMANI HAMZA ISSA | NYUMBA YENYE HATI NAMBA 80531-DLR | MONICA ANSELM TUWA | DODOMA | 18/10/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| AGGREY | JULIAS SIMBO LEMA | NYUMBA | HUSSEIN MTOBA FUNGALINDO | PUGU-KINYAMWEZI | 17/10/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | RAJABU MOHAMEDI MUOMBWA | NYUMBA | RAJABU MOHAMEDI MUOMBWA | YANGEYANGE-MSONGOLA | 18/10/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| AGGREY | MAKONGORO MGABO NYAMHOZA | NYUMBA | MWAJUMA MAKONGORO MATUTU | VINGUNGUTI | 19/10/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| AGGREY | WENCESLAUS JOHN MASSAWE | NYUMBA | MATESO JOHN MASSAWE | MAVURUNZA | 20/10/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | RAHMA ATHUMAN MKINDI | NYUMBA | MOHAMED A. SANGAWE | KISIWANI KIGAMBO | 21/10/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| AGGREY | PAULO GIREMBE RAWE | NYUMBA | PAULO GIREMBE RAWE | KIVULE | 18/10/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| AGGREY | YUSTER WESTON AYOLA | NYUMBA | SHABANI HARUNA MLENDA | MACHINJIONI -VINGUNGUTI | 19/10/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| AGGREY | SAMSON MUSSA SAMANYI | NYUMBA | ZAKARIA WAMBURA NYAHULE | MAJOHE | 18/10/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| AGGREY | JOYCE MICHAEL SAMSO | NYUMBA | MOHAMED JUMA MTOTE | MBAGALA NZASA | 21/10/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| ILALA | SWALIHINA JUMA KALYANGO | NYUMBA | SWALIHINA JUMA KALYANGO | KIVULE | 18/10/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUINGO | BERNARD KAIGWA BAIS | NYUMBA | BERNARD KAIGWA BAIS | TEGETA WAZO | 17/10/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| UBUNGO | KULWA JACOB MDIGWA | NYUMBA | KULWA JACOB MDIGWA | MPIGI MAGOHE | 18/10/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| UBUNGO | ASHA SALUM HASSANI | NYUMBA | ASHA SALUM HASSANI | KIBAMBA HONDOGO | 18/10/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UBUNGO | BENJAMINI PATRICK MABINZA | NYUMBA | BENJAMINI PATRICK MABINZA | MBEZI MSAKUZI | 18/10/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| UBUNGO | NICOLAUS EDMAEL MWENISOGOLE | NYUMBA | NICOLAUS EDMAEL MWENISOGOLE | KIMARA SUKA GOLANI | 19/10/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| UBUNGO | VERONICA CLEMENCE MAKASI. | NYUMBA | MARIAM HEROJONI MBILINYI | BUZA MAKANGARAWE TEMEKE | 19/10/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TANDALE | JOYCE ERNEST JONAS | NYUMBA | JOYCE ERNEST JONAS | MBAGALA KUU | 20/10/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| UKONGA | JOFREY MTITU THEOFIRI | NYUMBA | JOFREY MTITU THEOFIRI | VIWEGE MAJOHE | 21/10/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| UKONGA | JELINA ISSA MANGALE | NYUMBA | JELINA ISSA MANGALE | MACHIMBO KATA YA KIPUNGUNI | 24/10/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | GRACE GODY NGAHATILWA | NYUMBA | GRACE GODY NGAHATILWA | MACHIMBO KATA YA KIPUNGUNI | 25/10/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| UBUNGO | JOSEPH FRANCE NAYINDA | NYUMBA | JOSEPH FRANCE NYAYINDA | MBEZI KWEMBE-UBUNGO | 26/10/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| TEGETA | BAHATI CLEMENCE MWAUNGA | NYUMBA | BAHATI CLEMENCE MWAUNGA | NYAGASAGWE-WAZO | 17/10/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| TEGETA | NICE CHANDEMOHAMED | NYUMBA | ROSEMARY DESDELIUS HAULE | KWA AZIZI ALLY | 18/10/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| MAIN | CAPITAL ONE LIMITED | VIWANJA (2) | SUDI MARUNGU SIMBA NA FATUMA ABDUL MBWANA | PONGWE TANGA | 19/10/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | YOHANA BRUNO SHAYO | KIWANJA | WILSON ELICHILIA MBOYA | KEREGE BAGAMOYO | 20/10/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| TEMEKE | SELEMAN YUSUPH MAGANGA | NYUMBA | SELEMAN YUSUPH MAGANGA | MPONDA MIANZINI | 17/10/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | HUSSEIN ABDUL KARIM | NYUMBA | ESTER SIMON BUSOLWA | MBAGALA KUU | 18/10/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| TEMEKE | SALIM SULEIMAN HEMED | NYUMBA | SALIM SULEIMAN HEMED | MKURANGA | 19/10/2022 SAA 5:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |
| TEMEKE | SULEIMAN HAMZA MGAGI | NYUMBA (2) | SULEIMAN HAMZA MGAGI | KISEMVULE NA BUNGU RUFIJI | 20/10/2022 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja, Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.

2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.

3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.0759648448/0754497396/0714939933/0765999000/0712667989

4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.

217071702

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maandalizi ya Michezo ya Afrika 2023 ianze sasa

**MICHEZO** ya 13 ya Mataifa ya Afrika itafanyika Accra, Ghana mwakani na Tanzania ni miongoni mwa nchi 53 zinazotarajia kushiriki michezo hiyo.

Wachezaji watakaoshiriki watatumia michezo hiyo kama maandalizi kwa ajili ya kufuzu kushiriki Michezo ya Olimpiki itakayofanyika Paris, Ufaransa mwaka 2024.

Baada ya michezo ya 22 ya Jumuiya ya Madola kumalizika na Tanzania kurudi na medali tatu, moja ya fedha na mbili za shaba ni jambo la kujivunia, kwani kwa takribani miaka 16 hatukuwahi kurudi na medali katika michezo hiyo.

Imebaki chini ya mwaka mmoja kabla ya kufanyika kwa michezo hiyo ya Afrika, hivyo mashirikisho na vyama vya michezo vianze maandalizi mapema kwa ajili ya kupeleka timu.

Michezo hiyo kama ile ya Olimpiki na Jumuiya ya Madola, nayo huratibiwa na Kamati za Olimpiki za nchi (NOC), hivyo ni jukumu la vyama au mashirikisho ya michezo, serikali kuungana na TOC kuanza maandalizi mapema.

Hakuna siri kwani siku zote maandalizi ya mapema yamekuwa yenye manufaa, kwani tumeona maandalizi ya timu zetu kushiriki michezo iliyopita ya Jumuiya ya Madola imeleta tija na kutuwezesha kurudi na medali tatu.

Huwezi kuiweka kando serikali kwa mafanikio yaliyopatikana katika Michezo ya Jumuiya ya Madola ya mwaka huu, kwani yenyewe chini ya Rais Samia Suluhu Hassan ilitoa fedha na kuzifanya timu kukaa kambini kwa muda mrefu.

Ni jambo la aina yake kuona timu zetu tangu Februari ziko kambini kwa ajili ya michezo iliyokuja kufanyika kuanzia Julai hadi Agosti.

Kwa miaka mingi wachezaji na mashirikisho ya michezo au na vyama vya michezo wamekuwa wakiililia serikali kutaka isaidie timu kukaa kambini mapema, kilio ambacho imekisikia.

Ni matarajio yetu kuwa mashirikisho ya michezo kwa kushirikiana na serikali kupitia Wizara husika ya michezo na Baraza la Michezo la Taifa (BMT) wataanza kukutana mapema kwa ajili ya maandalizi ya michezo hiyo ya Afrika.

Kwa mara ya mwisho Tanzania ilitwaa medali katika Michezo ya Jumuiya ya Madola ilikuwa miaka 16 iliyopita wakati Samson Ramadhani na Fabian Joseph walipotwaa medali ya dhahabu na fedha katika marathoni na mbio za mita 10,000.


Na katika mchezo wa ndondi, ambao mwaka huu umetupatia medali mbili za shaba, wenyewe kwa mara ya mwisho ulituletea medali miaka 24 iliyopita wakati bondia Michael Yombayomba (sasa marehemu) alipotwaa dhahabu katika Michezo ya Kuala Lumpur, Malaysia mwaka 1998.

Ni miaka mingi imepita, hivyo ushindi huu wa mwaka huu unatakiwa kuwa na mwendelezo kama ilivyokuwa huko nyuma wakati Tanzania iking'ara katika michezo mbalimbali ya kimataifa na hasa katika riadha na ngumi.

Ushindi ni gharama na hauji kama mvua, hivyo wakati umefika wa kutumia fedha kwa ajili ya kuziandaa timu zetu ili zifanye vizuri katika mashindano mbalimbali ya kimataifa.

Ni wakati muhimu zaidi kujipanga kwa sasa, kwa sababu mwakani sio mbali na ili uweze kufanikiwa kwa jambo lolote, maandalizi ni muhimu sana, hivyo tunawakumbusha wadau wote kuhakikisha maandalizi yanafanyika kwa wakati ili tuweze kupata mafanikio.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Kamwe, Ahmed warudishe utani, uhasama ufe

**UTANI** wa jadi kwa klabu za Simba na Yanga uliisha siku nyingi sana, kwa sasa uliokuwepo ni uhasama tu. Klabu hizi ziliundwa katikati ya miaka ya 1930 kwa minajiri ya kutoa burudani, kudumisha undugu na umoja, na baadaye zikawa chachu cha kuusaka Uhuru wa Tanzania.

Kuna dhana imejengeka kuwa ni klabu moja tu ndiyo iliyotumika kudai uhuru, lakini ukweli ni kwamba Chama cha TANU kilizitumia klabu zote mbili kudai uhuru na ukapatikana mwaka 1961.

Klabu ya Yanga ilianzishwa mwaka 1935 na Simba ikaanzishwa mwaka mmoja baadaye, na waanzilishi wengi wao walikuwa ni wale waliojiengua kutoka Yanga.

Ukitembelea kwa sasa kwenye mitandao ya kijamii na baadhi ya vijiwe vya soka, utaona kabisa athari za waliokuja baadaye kujiita wasemaji wa klabu walivyowafanya mashabiki wa timu hizi mbili kuwa maadui badala ya watani wa jadi.

Unakutana na matusi, kuvunjiana heshima, dharau, badala ya utani ule ambao umezoeleka huko nyuma.

Nina uhakika Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Abeid Amani Karume kama wangeona uhasamu wenyewe ndiyo kama huu wa sasa wangeweza kuzipiga marufuku klabu hizi.

Lakini, walizilea na kuzipa kila aina ya msaada kwa sababu pamoja na kuzitumia kukusanya watu, kuzitumia kisiasa, kudumisha amani na umoja, pamoja na kuwa na ushirikiano.

Mfano, mwanachama au shabiki wa Simba wa Morogoro, leo anaweza kwenda Mwanza, anaweza kuwa hana ndugu, lakini akakuta tawi la klabu yake, akajieleza akapewa msaada na kuhudumiwa kama vile ndugu yao au mtu wanayemfahamu. Kumbe tu wote ni mashabiki wa timu moja.

Mtu anaweza kuwa shabiki wa Yanga, halafu ndugu yake Simba, huku anaweza kumuacha kumpa msaada ndugu yake na kumsaidia mtu asiyemfahamu, kwa sababu tu ni Yanga mwenzake.

Hii hadi leo imeendelea kuifanya Tanzania kuwa moja. Utani wa jadi ninaoufahamu mimi tangu enzi zile ni kwamba Yanga ikiifunga Simba, mashabiki wa timu hiyo wanakuwa na furaha isiyo kifani, wanawanunulia chakula, soda na vitu mbalimbali wale wa Simba, wanawapa wale huku wakiwazodia kwa maneno ya utano. Kule Kigoma wanawanyoa nywele kabisa na wanaonyolewa hawapingi.

Na wa Simba nao wanafanya hivyo hivyo, watawakirimu kwa kuwaninilia vinywaji na chakula, huku wakiwacharura wenzao. Unakuna, unapakiwa na maneno.

Hata kwenye misiba, klabu hizi mbili zimekuwa zikishirikiana, watu wanazikana, kwenye msiba wa watu wa Yanga, wa Simba wanashughulika na ule utani kama wa makabila unaendelea kama kawaida.

Kwenye miaka ya karibuni mashabiki wamegeuka kabisa. Badala ya kuwa utani imekuwa uhasama. Watu badala kutaniana wanatukanana na kuvunjiana heshima. Kwa kiasi kikubwa imeletwa na watu wanaoitwa au kujiita wasemaji kwenye miaka ya hivi karibuni.

Nimemsikia Afisa Habari mpya wa Yanga, Ali Kamwe, mara baada ya kuchaguliwa amesema ataondokana na aina hiyo ya usemaji, badala yake anataka kuendelea utani tu.

"Katiba ya Yanga ibara ya 39 inasema kazi ya Afisa Habari ni kufanya mawasiliano yote ya klabu na kuwajibika kwa Mtendaji Mkuu, kwa hiyo mimi nahakikisha kuwa nahusika na mawasiliano ya klabu kwenda kwa mashabiki na wanachama kupitia tasnia ya habari, hili suala la kucharurana ni utamaduni uliojengeka, tunaheshimu utani wa jadi ndiyo mpira wetu ilipo, utani wa hapa na pale unaweza kuwepo, lakini sidhani kama mimi naweza kufika hatua ya kumvunjia mtu heshima, kumdhihaki, kumtusi, mimi nimelelewa kwenye familia yenye kutunza maadili ya Mwafrika," anasema Kamwe.

Hili ni jambo la kupongezwa na kuungwa mkono si na Wanayanga wenzake, na Maafisa Habari wenzake, bali hata Watanzania wote.

Tuondokane na ushahibiki ambao umewaondoa Watanzania kuwa wamoja na kuwagawanya pande mbili. Wanajiona ni maadui zaidi kuliko watani wa jadi.

Nakumbuka mwanachama mmoja wa Simba aliyekuwa na rafiki zake wanachama wa Yanga, alikutana na mashabiki wawili ambao alitaniana nao sana, na baadaye alipowazoea, aliwapeleka kwa rafiki zake ambao ni wanachama wa Yanga ili wakapate kadi ya uanachama. Huu ndiyo utani wa jadi unaotakiwa.

Unatakiana na mtani wako, halafu baadaye unapata faida ya kupata kadi, kazi, kuoa, kuolewa, kusafiri na siyo kuishia kutukanana, kukashifiana, ambapo mwisho wake ni ugomvi na kupigana.

"Afanye kazi kwa bidii na kwa kujituma, aheshimu kila shabiki, ili mradi wa klabu yake, haijalishi amechoka kiasi gani, ili mradi wa klabu yakeMimi namfahamu Kamwe, ni kijana mwenye nidhamu

Tambo zitaendelea na ni muhimu, hatuwezi kuishi kama tuko msibani, lazima tuishi kwa tambo, Simba na Yanga ndiyo maisha yetu, mashabiki wetu ndiyo wanapenda maisha ya kutunishiana misuli, kuzodoana lakini siyo kwa kuvuka mipaka, zitaendelea ila safari hii zitakuwa za kitaalamu kidogo na siyo za kuropoka," alisema Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally kwenye salamu zake za pongezi kwa Kamwe.

Mashabiki wa soka wanachohitaji kwa maafisa hao, ni kuwaondoa kwenye uhasama uliopo na kuwarudisha kwenye utani wa jadi.

## HABARI KITAIFA




Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo, akikata utepe kuzindua unga wa ngano wa Azania kwa ajili ya matumizi ya chakula ili kuongeza thamani, kuleta suluhisho, utofauti na kurahisisha huduma kwa wateja wake, Jijini Dar es Salaam juzi. Kulia ni Mkurugenzi wa Biashara wa Azania Group, Joel Laiser. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

### KABWELA




# Watumishi wa umma waonywa wizi, rushwa

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

TUME ya Utumishi wa Umma, imewaonya watumishi kujiepusha na utovu wa nidhamu, wizi na uombaji wa rushwa kwa kuwa kufanya hivyo ni kuhatarisha ajira zao. Mwenyekiti wa Tume hiyo, Jaji Mstaafu Hamisa Kalombola, alitoa onyo hilo jana jijini hapa kwenye ziara ya wajumbe wa tume hiyo walipotembelea Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA).

Kalombola, aliwataka watumishi hao kuhakikisha muda wote wanatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma.

Pia alisema, waajiri wanapaswa kuweka mizania kati ya kutoa haki na motisha kwa wakati kwa wale wanaotekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kwa kuzingatia maadili na kutoa ushauri na adhabu kwa wale wanaokiuka maadili kulingana na kiwango cha uzingatiaji au ukiukwaji.

Aidha, mwenyekiti huyo alisema lengo la kutembelea DUWASA ni kuwatia moyo na kuwahamasisha watumishi wa Mamlaka hiyo kuendelea na kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sheria.

Alipongeza viongozi wa DUWASA kwa ubunifu walioanzisha wa kuhakikisha kuwa huduma za maji zinawafikia wananchi pamoja na ongezeko la watu kutokana na makao makuu ya nchi kuhamia hapa.

Kadhalika, alisema tume katika kutekeleza majukumu yake imejiwekea utaratibu wa kutembelea taasisi mbalimbali kwa lengo la kuelimisha ,kuhimiza uwajibikaji kujifunza na kubadilishana uzoefu kuhusu masuala ya uendeshaji na usimamizi wa rasilimali watu katika utumishi wa umma.

Jaji Mstaafu Kalombola, alisema majukumu ya tume hiyo ni pamoja na kupokea rufani na malalamiko ya watumishi kutoka maeneo mbalimbali nchini ili kutoa haki.

Mkurungenzi Mtendaji wa DUWASA, Mhandisi Aron Joseph, alisema mamlaka hiyo inaendelea kuhakikisha huduma ya maji inawafikia wananchi kwenye maeneo yote inayoyahudumia.

Joseph alisema, mahitaji ya maji kwa sasa ni lita milioni 130 kwa siku lakini mahitaji halisi ni lita milioni 67.1 kwa siku hivyo upungufu ni zaidi ya asilimia 50.

# Shule yafaulisha wanafunzi wote daraja A

**Na Mwandishi Wetu**

SHULE ya Hazina ya Magomeni jijini Dar es Salaam, imeendelea kutesa kwenye matokeo ya utahimilifu (moko) Mkoa wa Dar es Salaam, ambapo wanafunzi wote waliofanya mtihani huo wamepata alama A.

Mkuu wa taaluma wa shule hiyo, Wilson Otieno, alisema jana kwamba matokeo hayo mazuri yamewapa moyo wa kuendelea kufanya vizuri hadi kwenye mtihani wa darasa la saba.

Alisema matokeo hayo yameifanya kuwa miongoni mwa shule zilizofanya vizuri zaidi kwenye matokeo ya mtihani huo wa utahimilifu.

Otieno alisema wastani wa shule nzima imepata alama 283/300 ambayo ni sawa na band 1 ikimaanisha kwamba ni miongoni mwa shule zilizofanya vizuri zaidi kwenye matokeo hayo ya mwaka huu.

Alisema mwanafunzi wa kwanza kwenye shule hiyo ni Blessing Mayombo, ambaye amepata alama 293 kati ya 300 zinazotakiwa kwenye masomo yote.

Mbali na kufanya vizuri kwenye matokeo ya mock mkoa, alisema shule hiyo imekuwa ikiongoza kwa wilaya ya Kinondoni kwa mwaka wa pili mfululizo.

"Mwaka 2021 na mwaka huu tena shule ya Hazina imekuwa ya kwanza kwa Mkoa wa Dar es Salaam. Tunashukuru kwa mafanikio haya na tunaahidi kuwaandaa wanafunzi wetu waweze kufanya vizuri zaidi kwenye matokeo ya darasa la saba," alisema.

Alisema siri ya mafanikio hayo ni kujituma kwa walimu na ushirikiano ambao wamekuwa wakiupata kwa uongozi wa shule na wanafunzi ndiyo kitu wanachojivunia.

"Walimu wanafanyakazi kwa moyo sana, wazazi wa wanafunzi wamekuwa wakitoa ushirikiano mzuri sana kwa shule na uongozi wa shule unawajali sana walimu, hayo kwa pamoja yamekuwa yakisaidia ufaulu wetu kuwa juu mwaka hadi mwaka," alisema.

Aliwapongeza wanafunzi kwa mafanikio hayo na kuwataka wasome kwa bidii ili hatimaye waweze kuendelea kuongoza kitaifa na mkoa wa Dar es Salaam kwenye mitihani ijayo.



## KATIKA KUADHIMISHA MIAKA 73 YA KUANZISHWA KWA JAMHURI YA WATU WA CHINA

# HOTUBA YA BALOZI CHEN MINGJIAN KATIKA TAFRIJA YA MTANDAONI KATIKA MAADHIMISHO YA MIAKA 73 YA KUANZISHWA KWA JAMHURI YA WATU WA CHINA

*Oktoba 1, 2022*



**Mh. Chen Mingjian, Balozi wa China nchini Tanzania**

***Mheshimiwa Balozi Liberata Mulamula, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki,***

***Marafiki, Wananchi,***

***Mabibi na mabwana,***


Tarehe 1 Oktoba hii ni kumbukumbu ya miaka 73 ya kuanzishwa kwa Jamhuri ya Watu wa China (PRC). Nina furaha kusherehekea Siku ya Kitaifa ya China mtandaoni pamoja na marafiki wa Kitanzania kutoka matabaka mbalimbali na wananchi wa China nchini Tanzania. Kwa niaba ya Ubalozi wa China nchini Tanzania, napenda kufikisha salamu za sikukuu kwenu nyote, na kutoa shukrani zetu za dhati kwa marafiki ambao wamekuwa wakiendeleza urafiki wa China na Tanzania kwa muda mrefu.

Oktoba ni msimu wa vuli. Pia ni wakati mzuri wa mavuno. Katika mwaka huu, China ilianza safari mpya ya kujenga kikamilifu nchi ya kisasa na yenye nguvu ya ujamaa. Kwa kutafuta maendeleo yenye ubora na uwazi wa hali ya juu, China imeendelea kuchangia amani, utulivu na maendeleo endelevu duniani.


Ikikabiliwa na mabadiliko na janga ambalo halijaonekana katika karne moja, China imesonga mbele na kupata mafanikio ya kushangaza katika maendeleo. Kwa kuweka maisha na usalama wa watu kwanza kama kawaida, China imefanikiwa kulinda mafanikio yaliyopatikana kwa bidii katika kuzuia na kudhibiti janga. Uchumi wa China umevumilia vipingamizi na kuendelea kukua. Katika nusu ya kwanza ya mwaka huu, Pato la Taifa la China lilifikia dola za Marekani trilioni 8.68, na biashara ya nje ya nchi hiyo iliongezeka kwa asilimia 9.4 mwaka hadi mwaka. Juhudi zilizoimarishwa za China katika kujenga muundo mpya wa maendeleo zimeleta msukumo mkubwa katika kufufua uchumi wa dunia. Tumefanikiwa pia kuandaa Michezo ya Olimpiki ya Majira ya baridi bila vikwazo, salama na vizuri , tukiwasilisha kwa ulimwengu tena China iliyostawi, inayojiamini na yenye uwazi. Chombo cha anga za juu cha Shenzhou-13 kimekamilisha misheni zake kwa ufanisi. China imeendelea kukuza maendeleo ya kisayansi na kiteknolojia ili kuwanufaisha wanadamu wote.

Ikikabiliwa na dunia ambayo imeingia katika kipindi cha ghasia na mabadiliko, China imechukua jukumu lake katika diplomasia, na kushikilia bango ya amani, maendeleo na ushirikiano. Mwaka huu umeshuhudia pendekezo la Rais Xi Jinping yeye mwenyewe la Mpango wa Usalama wa Kimataifa (GSI), na kukuza utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Kimataifa (GDI), ambao unalenga kuongeza "mbawa mbili" katika ujenzi wa jumuiya yenye mustakabali wa pamoja kwa wanadamu. China inaendelea kuwa mhimili mkuu wa ushirikiano wa kimataifa wa kupambana na janga. Kufikia Juni mwaka huu, China imetoa zaidi ya dozi bilioni 2.2 za chanjo ya UVIKO-19 kwa zaidi ya nchi 120 na mashirika ya kimataifa. Kuanzia Olimpiki ya Majira ya baridi ya Beijing hadi Mkutano wa kilele wa BRICS, kutoka Mazungumzo ya Juu ya Maendeleo ya Kimataifa hadi Mkutano wa Wakuu wa Jumuiya ya Ushirikiano ya Shanghai (SCO) uliofanyika hivi karibuni huko Samarkand, tunaweza kuhisi dhamira thabiti ya jumuiya ya kimataifa katika kutetea umoja wa pande nyingi, na matumaini yake ya dhati kwa China kuchukua nafasi kubwa zaidi kwenye jukwaa la dunia.

Ikikabiliwa na mabadiliko ya mara kwa mara katika hali ya kimataifa, uhusiano kati ya China na Tanzania umekuwa ukiendelea kwa kasi na kufikia viwango vipya. Rais Xi Jinping na Rais Samia Suluhu Hassan wanathamini na kuongoza maendeleo ya uhusiano wa China na Tanzania wao wenyewe. Februari mwaka huu, Shule ya Uongozi ya Mwalimu Julius Nyerere iliyosaidiwa na China imekabidhiwa kwa Tanzania. Katika mwaka huu, Mjumbe wa Taifa la China na Waziri wa Mambo ya Nje Wang Yi, na Mjumbe wa Baraza la Taifa la China na Waziri wa Ulinzi wa Wei Fenghe, walifanya mazungumzo kwa njia ya video na wenzao wa Tanzania Waziri wa Mambo ya Nje Balozi Liberata Mulamula na Waziri wa Ulinzi Dkt. Stergomena Tax mtawalia. Majadiliano ya kisiasa ya tabaka mbalimbali kati ya China na Tanzania yameenda ndani zaidi. Pande hizo mbili zimekuwa zikifanya mawasiliano ya kina kuhusu hatua za ufuatiliaji wa Mkutano wa Nane wa Mawaziri wa FOCAC, na utekelezaji wa "programu tisa" za ushirikiano kati ya China na Afrika umezaa matunda ya mapema nchini Tanzania. Katika nusu ya kwanza ya mwaka huu, kiwango cha biashara kati ya China na Tanzania kilifikia dola za Marekani bilioni 3.558, na hivyo kusajili ukuaji wa mwaka hadi mwaka wa asilimia 31.5. Tanzania imesaini hati hizo na China ambazo hazitoi ushuru wa forodha kwa bidhaa chini ya asilimia 98 ya bidhaa zinazotozwa ushuru zinazotoka Tanzania. Idadi kubwa ya miradi ya ushirikiano kati ya China na Tanzania, kama vile Kituo cha Kufua Umeme wa Maji cha Julius Nyerere na Kituo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi cha Mkoa wa Kagera, inaendelea kwa kasi. Aidha, China imetekeleza kikamilifu ahadi yake ya kuisaidia Tanzania katika mapambano dhidi ya UVIKO-19. Hadi sasa, China imetoa dozi milioni 5.61 za chanjo ya UVIKO-19 kwa Tanzania.




**Rais Xi Jinping wa China anaongoza Mazungumzo ya ngazi ya juu kuhusu Maendeleo ya Dunia kwa njia ya video mjini Beijing, mji mkuu wa China, Juni 24, 2022. Xi alitoa hotuba muhimu yenye kichwa cha habari "Kuanzisha Ubia wa Hali ya Juu kwa Enzi Mpya ya Maendeleo ya Kimataifa". (Picha/Xinhua)**



**China ilizindua chombo cha anga za juu cha Shenzhou-14 mnamo Juni 5, 2022, na kutuma wanaanga watatu kwenye kituo chake cha anga cha Tiangong. (Picha/Xinhua)**

Ni sawa kutaja kwamba China na Tanzania zinaendelea kuelewana na kusaidiana katika masuala yanayohusu masilahi ya msingi na mambo makuu, na kufanya kazi pamoja ili kulinda haki kimataifa. Muda mfupi uliopita, Waziri wa Mambo ya Nje, Liberata Mulamula, kwa niaba ya Serikali ya Tanzania, alisisitiza hadharani msimamo wa Tanzania kuhusu suala la Taiwan, akisema kwamba Tanzania bado inajitolea kwa kanuni ya kuwa na China moja na kuunga mkono msimamo wa haki wa China kuhusu suala la Taiwan. Huu ulikuwa mfano wazi wa urafiki wa nyakati zote kati ya China na Tanzania, ambao tunathamini sana.

Mwezi Oktoba mwaka huu, Kongamano la 20 la Kitaifa la Chama cha Kikomunisti cha China (CPC) litafanyika. China itajitahidi kufufua taifa lake kutoka mwanzo mpya katika historia, na ushirikiano kati ya China na Afrika, China na Tanzania utabarikiwa na fursa mpya za kihistoria. China iko tayari kuimarisha ulinganifu wa mikakati ya maendeleo na mawasiliano ya kisera na Tanzania, kuendelea kujumuisha maendeleo ya China katika maendeleo ya pamoja ya nchi hizo mbili, kuunga mkono juhudi za Tanzania za kupata maendeleo huru na endelevu, na daima kuimarisha na kuendeleza ushirika wa kina kati ya China na Tanzania.

***Naitakia nchi mama kubwa heri ya siku ya kuzaliwa na mafanikio!***

***Udumu urafiki wa China na Tanzania!***

## TOLEO MAALUMU

# KATIKA KUADHIMISHA MIAKA 73 YA KUANZISHWA KWA JAMHURI YA WATU WA CHINA

# HOTUBA YA WAZIRI WA MAMBO YA NJE WA TANZANIA LIBERATA MULAMULA KATIKA TAFRIJA YA MTANDAONI YA MAADHIMISHO YA MIAKA 73 YA KUANZISHWA KWA JAMHURI YA WATU WA CHINA

*Oktoba 1, 2022*



**Mhe. Balozi Liberata Mulamula Waziri wa Mambo ya Nje wa Tanzania**

***Mheshimiwa,***

***Wapendwa marafiki Watanzania,***

***Mabibi na Mabwana,***

Nina furaha kubwa kujumuika nanyi leo kusherehekea miaka 73 ya kuanzishwa kwa Jamhuri ya Watu wa China.

Kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa niaba yangu binafsi, napenda kuwapongeza kwa mafanikio haya makubwa.

Katika miaka 73 iliyopita, watu wa China chini ya uongozi bora wa Chama cha Kikomunisti cha China wamepata ustawi na ukuaji wa uchumi ambao sote tumeshuhudia na kuupenda.

Inavutia kwamba zaidi ya watu milioni 700 nchini China wameondokana na umaskini, na hivyo kuchangia zaidi ya asilimia 70 ya kupunguza umaskini duniani kote. Hakika haya ndiyo mafanikio makubwa zaidi ya kupunguza umaskini katika historia ya binadamu.

Kwa kuongozwa na kanuni tano za kuishi pamoja kwa amani, China imeimarisha urafiki na ushirikiano kati yake na nchi nyingine ikiwemo Tanzania, na imetoa mchango muhimu katika kujenga jumuiya yenye mustakabali wa pamoja wa wanadamu na kuendeleza mambo adhimu ya amani na maendeleo ya binadamu.

Mabibi na Mabwana, marafiki wapendwa wa Tanzania, tunapoadhimisha miaka 73 ya kuanzishwa kwa Jamhuri ya Watu wa China, pia tunaadhimisha miaka 58 ya uhusiano wa kidiplomasia kati ya nchi zetu mbili.

Tanzania na China ni marafiki wa nyakati zote, wanafurahia ushirikiano wa kina na wa pamoja. Tanzania inazingatia kwa dhati Kanuni ya China Moja.

Viongozi wetu wawili, Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Xi Jinping, Rais wa Jamhuri ya Watu wa China, walifikia makubaliano, ambayo ni kuunganisha Mpango wa Ukanda wa Njia (BRI) na Jukwaa la Ushirikiano kati ya China na Afrika (FOCAC) na mikakati ya maendeleo ya Tanzania.

Katika suala hili, walikubaliana kupanua ushirikiano katika kilimo, usafiri, mawasiliano, utalii na nishati, ili kuimarisha maudhui ya ushirikiano wa pande zote wa Tanzania na China.

Katika mwaka uliopita, tumeshuhudia ushiriki wetu katika kudumisha kasi na kufikia kilele hiki cha kimkakati cha uhusiano wetu wa nchi mbili kwa kusaidiana katika masuala yanayohusu masilahi husika na kuimarisha mabadilishano baina ya nchi hizo.



**Rais Samia Suluhu Hassan na Balozi Chen Mingjian walizindua Shule ya Uongozi ya Mwalimu Julius Nyerere, pamoja na katibu wakuu au wawakilishi wa ngazi za juu wa vyama ndugu sita vya kusini mwa Afrika, Kibaha, Tanzania, Februari 23, 2022. (Picha/Ubalozi wa China )**

Mabibi na mabwana, Tanzania imejitolea kuimarisha zaidi mkakati wetu wa mawasiliano na ushirikiano wa kisera, na kutekeleza kikamilifu Mipango Tisa ya FOCAC. Tuko tayari kufanya kazi na China ili kuendeleza ari ya reli ya Tanzania-Zambia (Tazara), kuifanya kuwa ya kisasa kulingana na mwenendo wa nyakati na kuifanya Tazara kuwa njia muhimu wa usafirishaji katika ukanda huo.

Pia, Tanzania iko tayari kufanya kazi na China ili kuendeleza kikamilifu utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Kimataifa na Mpango wa Usalama wa Kimataifa ili kuimarisha ushirikiano wa pande zote.

Mabibi na mabwana, marafiki wapendwa,

Ninapohitimisha, nichukue fursa hii kwa niaba ya Serikali na wananchi wa Tanzania pamoja na Chama Tawala, Chama Cha Mapinduzi, kufikisha salamu za kheri kwa Chama cha Kikomunisti cha China (CPC) kinapojiandaa kufanya Kongamano la Kitaifa la 20 la CPC. Tunalitakia Kongamano mafanikio madhubuti.

***Naitakia serikali na watu wa China wafurahie maadhimisho ya miaka 73 ya kuanzishwa kwa Jamhuri ya Watu wa China.***

***Ninawashukuru kwa umakini wenu mzuri.***

***Asanteni Sana.***



**Michezo ya Majira ya baridi ya Olimpiki ya Beijing 2022 ilifanyika Beijing na Zhangjiakou kuanzia tarehe 4 hadi 20 Februari 2022. Picha inaonyesha kwamba Dinigeer Yilamujiang (kushoto) na Zhao Jiawen waliwasha kikauldron ya Olimpiki katika sherehe za ufunguzi kwenye Uwanja wa Kitaifa wa Beijing, Feb. 4, 2022. (Picha/Xinhua)**



**Mjumbe wa Taifa la China na Waziri wa Mambo ya Nje Wang Yi afanya mazungumzo kwa njia ya video na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki wa Tanzania Liberata Mulamula, Machi 20, 2022. (Picha/Wizara ya Mambo ya Nje ya China)**

RIPOTI MAALUM

# KATIKA KUADHIMISHA MIAKA 73 YA KUANZISHWA KWA JAMHURI YA WATU WA CHINA

## MFANO MBADALA WA MAENDELEO KWA NCHI ZA AFRIKA KUTOKA KWA UZOEFU WA MIAKA 73 YA CHINA

*Oktoba 1, 2022*



**Mhe. Mbelwa Kairuki, Balozi wa Tanzania nchini China**




**Balozi wa China nchini Chen Mingjian na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo wa Tanzania Mohamed Mchengerwa wakitia saini Mpango wa Utekelezaji wa Miaka 2022 - 2025 Chini ya Makubaliano ya Utamaduni kati ya China na Tanzania, Dar es Salaam Mei 26, 2022. (Picha/Ubalozi wa China)**

China sasa inaadhimisha Miaka 73 tangu kuanzishwa kwa Taifa hilo. Sisi - Watanzania, kama kawaida, hatutakosekana katika wakati huu muhimu wa kutoa pongezi zetu za dhati kwa rafiki yetu wa nyakati zote - Jamhuri ya Watu wa China.

Katika kipindi cha miaka 73 iliyopita, China imekuwa nchi yenye uchumi mkubwa zaidi duniani (kwa msingi wa usawa wa uwezo wa kununua), mzalishaji, mfanyabiashara wa bidhaa, na mmiliki wa akiba ya fedha za kigeni. China iliinua wastani wa watu milioni 800 kutoka kwenye umaskini ndani ya kipindi hicho. Baada ya kuona hatari za maafa ya njaa ya mara kwa mara, Uchina ikiwa na asilimia 9 tu ya ardhi inayofaa kwa kilimo, imefanikiwa kulisha watu wake bilioni 1.4.

Pamoja na ukuaji wa China katika miaka 73 iliyopita, nchi za Afrika zimeendeleza ushirikiano wa pande nyingi, wa kisayansi na wa kunufaisha pande zote mbili. Tanzania imekuwa miongoni mwa washirika wa kutegemewa na wa dhati tangu waasisi wetu wawili walipochukua hatua ya kuanzisha uhusiano wa kidiplomasia miaka 58 iliyopita. Kwa macho ya kizazi cha baba zetu, uhusiano kati ya China na Tanzania ulijikita katika TAZARA, katika ziara za mara kwa mara za viongozi wa ngazi za juu, na jukumu muhimu lililofanywa na Tanzania na nchi nyingine katika kurejesha haki halali ya Jamhuri ya Watu wa China nchini China. Umoja wa Mataifa. Uhusiano wetu wa karibu umepanuka kutoka ushirikiano kati ya serikali na serikali hadi muungano wa leo kati ya watu na watu. Watu wa China na Tanzania wamefungamana bila kutengana na mabadilishano ya kina ya biashara, uwekezaji, utalii na elimu.

Kama moja ya nchi za Majaribio ya Afrika kutekeleza Mpango wa Ukanda na Njia, tunaweza kuona msukumo mpya na nishati kutoka China imeingizwa katika mabadilishano ya China na Tanzania katika maeneo ya kiuchumi. Hivi karibuni tumeshuhudia bidhaa nyingi zisizo za rasilimali za Tanzania, hususani mazao ya kilimo yakiingia kwenye soko la China, ambayo yanaleta manufaa yanayoonekana na yanayoonekana kwa wananchi wa kawaida.

China na Tanzania zimesaidiana kulinda haki kimataifa; kujenga maendeleo thabiti zaidi na endelevu, na kuimarisha amani na utulivu wa kikanda. Mazingira yanayozidi kuwa magumu duniani na matishio mapya yanayoibuka yanailazimu China na Tanzania kushirikiana kwa karibu zaidi kuliko hapo awali. Ni lazima tuwe na maelewano juu ya kushughulikia changamoto hizo kwa sababu hatima yetu na kuishi vinafungamana.

Tunajua kwamba takriban wiki mbili kutoka sasa, katika msimu mzuri zaidi wa Beijing, Kongamano la Kitaifa la 20 la CPC litaitishwa katika mji mkuu. Macho yote na masikio yatazingatia Beijing. Sote tuna matarajio makubwa kwa Kongamano hilo. Na hiyo ni kwasababu China ni kubwa sana kupuuzwa na vile vile ni kubwa sana kushindwa. Utulivu na ustawi wa China ni muhimu kwa dunia. Kwa hivyo, tunatamani na kutarajia CPC kufanya maamuzi na chaguo sahihi. Mwishowe, natumai urafiki wetu utadumu milele!



**Mradi wa ujenzi na upanuzi wa gati namba 1–7 za Bandari ya Dar es Salaam unaofanywa na kampuni ya China. (Picha/Xinhua)**



**Shehena ya kwanza ya maharage ya soya ya Tanzania yenye jumla ya tani 120.2 iliwasili katika bandari ya Qingdao ya China, Mei 2021. (Picha/CCTV)**

# KATIKA KUADHIMISHA MIAKA 73 YA KUANZISHWA KWA JAMHURI YA WATU WA CHINA

## MAADHIMISHO YA MIAKA 73 YA KUANZISHWA KWA PRC: MAFANIKIO YA KUFURAHISHA YA MAENDELEO

*Oktoba 1, 2022*



**Profesa Humphrey P. B. Moshi, Mkurugenzi wa Kituo cha Mafunzo ya Kichina, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**

Uongozi na watu wa China wanaadhimisha miaka 73 tangu kuanzishwa kwa taifa lao, Jamhuri ya Watu wa China (PRC). Kwa kweli, katika miaka hii 73, jamii ya China imepitia mabadiliko ya ajabu katika nyanja mbalimbali: kutoka jamii iliyofungwa hadi iliyo wazi, kutoka maskini hadi nchi yenye ustawi, kutoka kwa mtazamo usio na kikomo hadi kukumbatia utandawazi na utandawazi wa pande nyingi, kutoka kwa tendaji hadi nafasi ya kuwa makini katika siasa za jiografia. PRC haya yote na hatua muhimu ni ushuhuda wa wazi wa ukweli kwamba PRC imekuwa msukumo, sio tu kwa ulimwengu ulioendelea, lakini zaidi kwa nchi zinazoendelea, na haswa Afrika. Mafanikio haya na hatua muhimu zitafafanuliwa zaidi katika sehemu za kuhakikisha.

Kwanza kabisa, kuanzishwa na kuibuka kwa PRC baadae kumechangia pakubwa katika maendeleo ya kimataifa, hivyo kuwa na manufaa kwa dunia nzima. Hasa, China inachangia takriban asilimia 30 katika ukuaji wa uchumi wa dunia kwa zaidi ya miaka kumi mfululizo. Kiwango hiki cha ukuaji hakina kifani katika historia ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi, hata kwa nchi zilizoendelea za magharibi.

Pili, katika kipindi cha zaidi ya miaka 40 China imeweka rekodi mpya, sio tu ya kupanda hadi kuwa nchi ya pili kwa uchumi mkubwa duniani baada ya Marekani, bali pia ukuaji huo ulipatikana bila mgogoro au vita. Hali hii ni kubwa pia ni ya kipekee, ikilinganishwa na historia ya maendeleo ya Marekani, Umoja wa Kisovyeti, Uingereza, Ufaransa, Ujerumani na Japan, maendeleo ambayo yaliambatana na mgogoro wa kiuchumi na kifedha, pamoja na vita.

Tatu, Kuinuka kwa China sio tu kumekuwa msukumo kwa nchi zinazoendelea, bali pia ni kichocheo cha maadili, kwa maana kwamba kurudi nyuma na umaskini havizingatiwi tena kuwa suala la hatima. Hakika, kwa uongozi sahihi, kusudi na kujitolea, pamoja na imani ya watu katika mfumo wa utawala, changamoto mbili zinaweza kushinda kwa urahisi na PRC imethibitisha hilo na kuonyesha njia. Hata hivyo, ni lazima kuwe na mfumo madhubuti wa upangaji ili kuimarisha uundaji wa sera zinazohitajika, mifumo ya kitaasisi na kisheria, inayoambatana na mfumo uliowekwa wazi wa ufuatiliaji na tathmini.

Nne, Kuinuka kwa China kunaongozwa na "Makubaliano ya Beijing" na sio dhana ya maendeleo ya Makubaliano ya Washington. Hii inaonyesha wazi kwamba kuna dhana mbadala za maendeleo zinazopatikana kwa nchi zinazoendelea kuchagua, na hivyo kukandamiza mtazamo potofu kwamba kuna moja tu na kubwa, ile ya mazungumzo ya uliberali mamboleo. Hata hivyo, hatutetei jambo la "kuiga". Kinyume chake, mtindo wowote utakaopitishwa, lazima ubadilishwe kulingana na sifa za kisiasa, kitamaduni, kijamii na kiuchumi za nchi husika. Sio kwa bahati kwamba China imepitisha mtindo unaoitwa "ujamaa wenye sifa za Kichina". Kwa maneno mengine, tunaamini kwa dhati kwamba kile tunachoita "mazoezi bora" inamaanisha "kile kinachofanya kazi vizuri zaidi katika hali ya mtu mwenyewe". Kwa hiyo, nchi zinazoendelea zinapaswa kuzingatia jambo hili.

Tano, ari ya China ya mshikamano na ushirikiano, kupitia makubaliano ya pande nyingi na za nchi mbili, umewezesha kuanzishwa kwa majukwaa mbalimbali ya ushirikiano, kama vile Jukwaa la Ushirikiano wa China na Afrika (FOCAC), Mpango wa Ukanda na Njia (BRI), Jukwaa la Wataalam ya China na Afrika (CATTF), n.k. Ushiriki wa nchi katika mikutano hii tofauti umeongeza kasi ya maendeleo yao ya kijamii na kiuchumi, kupunguza umaskini, kukuza Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka Nje (FDI) na maendeleo ya miundombinu, kutaja machache tu. Ushahidi kutoka Afrika unaonyesha kuwa kupitia FOCAC, China imefanya zaidi ya asilimia 60 ya miundombinu barani Afrika, na biashara kati ya China na nchi za Afrika imekua zaidi ya mara 20 na kufikia dola za Kimarekani bilioni 255 mwaka 2021 kutoka dola 10 bilioni ndogo mwaka 2000. Zaidi ya hayo, Hisa ya China ya uwekezaji wa moja kwa moja barani Afrika imefikia dola bilioni 110, huku takriban makampuni 4,000 ya China yakianzisha viwanda na biashara barani Afrika, huku yakitengeneza nafasi za kazi 300,000 katika bara hilo.

Kwa upande wa ushirikiano kati ya China na Tanzania, tunashuhudia kuimarishwa kwa biashara na Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka China, ambayo imekuwa mshirika mkubwa zaidi wa kibiashara na chanzo kikubwa cha Uwekezaji wa Moja kwa Moja kutoka Nje kwa Tanzania. Mgawanyo wa kisekta wa miradi ya uwekezaji ya China nchini ni kama ifuatavyo: kilimo (16), ujenzi (67), viwanda (456), maliasili (8), huduma (22), mawasiliano (5), utalii (56), usafiri (39), na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) (1). Kwa hakika, mgawanyo huo hapo juu unaonyesha kuwa uwekezaji huo umeegemea upande wa viwanda, jambo ambalo linawiana vyema na Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025, ambayo inaeleza kuwa Tanzania itahitimu kutoka nchi yenye maendeleo duni hadi nchi ya kipato cha kati na uchumi wa nusu viwanda ifikapo mwaka huu. 2025. Mpangilio huu licha ya kuwa, usambazaji ulio hapo juu unahitaji kusawazishwa ili kutafakari na kushughulikia changamoto zinazoletwa na UVIKO-19 na janga linaloendelea la Ukrainia, huku tukitumia fursa zinazojitokeza kutokana nazo.



**Rais wa Zanzibar Dk Hussein Ali Mwinyi akiwatunuku nishani wanachama 21 wa Kundi la 31 la Timu ya Madaktari wa China kwa Zanzibar kutokana na huduma bora ya mwaka mmoja ya matibabu huko Visiwani Zanzibar Septemba 11, 2022. (Picha/Xinhua)**

Changamoto kimsingi ni mbili: Kwanza, hitaji la kuimarisha mifumo dhaifu ya afya ya umma barani Afrika ili kuifanya iweze kustahimili magonjwa ya milipuko ya sasa na yajayo. Pili, umuhimu wa kuimarisha kiwango dhaifu sana au cha chini cha usalama wa chakula barani Afrika kupitia uboreshaji wa kilimo cha kisasa. Kuhusiana na fursa zinazojitokeza, umakini zaidi unahitaji kuwekwa kwenye uwekaji uchumi wa kidijitali kwa kuhakikisha kwamba sio tu miundo msingi inayohitajika iko, lakini pia ni jumuishi, kama njia ya kuziba mgawanyiko wa kiteknolojia wa ndani, na vilevile katiAfrika na kwingineko duniani. Haya ni masuala muhimu ambayo yanahitaji kuchukuliwa kwenye bodi na mifumo ya ushirikiano ya sasa na ya baadaye.

Mafanikio yaliyo hapo juu ya kutia moyo na hatua muhimu za PRC, ndani na nje ya mipaka yake, ni ushuhuda wa wazi kwamba yamekuwa ya manufaa kwa wanadamu kote ulimwenguni. Kwa hivyo, kuna sababu zinazokubalika kwa nini PRC inapaswa kupongezwa kwa dhati kwenye siku yake ya kuzaliwa ya 73. Katika suala hili, tunaitakia, PRC, uongozi wake na watu wa China sherehe za kukumbukwa. Wakati huo huo, tunakutakia mafanikio mema katika juhudi zako za baadaye za kuunganisha mafanikio na hatua muhimu, huku tukidumisha ari ya kutia moyo na majukwaa ya ushirikiano, kwa ulimwengu wenye amani na mafanikio.

**Uishi kwa muda mrefu PRC, uongozi wake na watu wa China!**



**Sherehe za uwekaji msingi wa awamu ya pili ya uzalishaji wa klinka ya Huaxin Maweni 4000T/D awamu ya pili inafanyika katika kata ya Maweni, Wilaya ya Tanga, Mkoa wa Tanga, Julai 26, 2022. (Picha/Huaxin Cement)**



HABARI ZANZIBAR

## Bilioni 470/- zatengwa uwanja ndege Pemba

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIKA mikakati ya kukifungua kisiwa cha Pemba kwa miundombinu ya mawasiliano na uchukuzi, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imetenga Sh. bilioni 470 kwa ajili ya ujenzi wa uwanja wa ndege wa Pemba.

Hayo yalisemwa Jana katika kikao cha baraza la wawakilishi na Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Nadir Abdulatif wakati akitoa ufafanuzi wa miradi mikubwa inayotarajiwa kutekelezwa katika kisiwa cha Pemba ambayo ni sehemu ya ahadi za Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Alisema ujenzi wa uwanja wa ndege wa Pemba ni miongoni mwa miradi ya kimkakati kwa ajili ya kukifungua kisiwa hicho kiuchumi na uwekezaji, hatua ambayo itaongeza mapato ya serikali na uchumi kwa wananchi.

Naibu Waziri alizitaja hatua zilizofikiwa hadi sasa kuwa ni pamoja na kuwatambua wananchi wote ambao wamebomolewa nyumba zao vikiwamo vipando vyao kwa ajili ya kupisha upanuzi wa uwanja huo.

"Mheshimiwa Spika tumekamilisha mchakato wa kuwatambua watu wote wenye sifa ya kulipwa fidia kwa ajili ya kupisha ujenzi wa uwanja wa ndege wa Karume kisiwani Pemba," alisema.

Pia alisema wizara imejipanga kuifanyia ukarabati mkubwa bandari ya Wete ambayo ni kiungo muhimu kwa mikoa miwili ya kisiwa hicho katika usafirishaji wa bidhaa mbalimbali.

Bandari ya Wete, alisema ni muhimu kwa kuwa ina uwezo wa kuiunganisha na mikoa jirani ya Tanzania Bara ukiwamo Tanga na Mombasa nchini Kenya katika kusafirisha bidhaa mbalimbali pamoja na wananchi kufanya shughuli za kiuchumi na biashara.

Alizitaja hatua zilizofikiwa kwa sasa kupitia Shirika la Bandari Zanzibar kuiteua kampuni ya INROS LACKNER SE kutoka Ujerumani kwa ajili ya upembuzi yakinifu kujua mazingira yatakayotumika kwa ajili ya ukarabati wa bandari hiyo.

"Tayari tumeiteua kampuni ya Ujerumani kufanya kazi za upembuzi yakinifu ambazo zitatuongoza katika kufanya ukarabati wa bandari ya Wete ambayo ni lango kuu la kiuchumi linalounganisha mikoa miwili ya Pemba kiuchumi na uwekezaji," alisema.

# Uagizaji bidhaa kutoka nje wapanda

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

OFISI ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imesema uagizaji bidhaa kwa Zanzibar umeongezeka kutoka asilimia 5.1 kwa Julai hadi asilimia 9.9 kwa Agosti, mwaka huu.

Mbali na kuongezeka kwa uagizaji bidhaa, Zanzibar pia imesafirisha bidhaa zenye thamani ya Sh. bilioni 12.1 idadi ambayo imeonekana kushuka kwa asilimia 70.

Akiwasilisha takwimu za biashara za kimataifa kwa mwezi Agosti kwa waandishi wa habari mjini hapa, Mtakwimu kutoka Kitengo cha Biashara na Kodi Idara za Takwimu za Kiuchumi Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Sharikh Khatib Faki, alisema hali hiyo inatokana na kupanda na kushuka kwa bei za bidhaa katika soko la dunia.

Pia alisema nchi zilizoongoza kwa uagizaji bidhaa kwa mwezi huo ni Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), China, India na Oman na kwa usafirishaji ni Singapore na Denmark.

Alisema bidhaa hizo zilizoagizwa kutoka nchi hizo za nje ni ngano, mabomba ya maji na nyaya za umeme na kwa bidhaa zilizosafirishwa kwenda nje kwenye nchi tano zilizoongoza ni mwani, pumba, vikoi na kanga.

Naye Ofisa kutoka Jumuiya ya Wafanyabiashara, Haji Weka Abdalla, aliwashauri wakulima na wafanyabiashara kuzalisha bidhaa bora na zenye viwango vya kuuzika ndani na nje ya nchi. Alisema hali hiyo itawarahisishia kupata soko la uhakika la bidhaa zao na hatimaye kuwainua kiuchumi.

Pia aliishauri serikali kuwashajihisha wakulima kuongeza kasi ya kilimo cha mazao ya chakula ili kupunguza gharama za uagizaji wa bidhaa hizo nje ya nchi na kwamba hali hiyo itasaidia kukuza soko la ndani na kuwainua wakulima wadogo na kuwa na kipato cha uhakika.

Alisema endapo uzalishaji wa bidhaa za vyakula na nafaka utakuwa mzuri, hakuna sababu kwa serikali kuagiza vyakula nje na badala yake itanunua kutoka kwa wakulima wa ndani.

Kadhalika, alisema uzalishaji mzuri wa bidhaa unachangia uchumi wa nchi kukua kwa kasi, hivyo wakulima wajitahidi kuzalisha bidhaa zenye viwango ili kupata soko la uhakika.




Mwakilishi wa Viti Maalum Mkoa wa Kaskazini Unguja, Panya Ali Abdallah, akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Rais Mwinyi aahidi kuunga mkono wahisani

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema serikali itaendelea kuunga mkono juhudi za wahisani katika kuzitafutia ufumbuzi changamoto zinazoikabili jamii.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo alipozungumza na daktari bingwa wa upasuaji kutoka Uingereza, Dk. Charlotte Hawkins, aliyefika Ikulu Zanzibar kwa ajili ya kusalimiana.

Alisema Zanzibar inahitaji wataalamu wengi zaidi kutoka nje ili kusaidiana na wataalamu wazalendo katika kuimarisha utoaji wa huduma za kijamii kupitia sekta mbalimbali zikiwamo afya na elimu.

Rais Mwinyi alisema ujio wa Dk. Hawkins nchini na kujikita katika kukabiliana na changamoto inayowakabili watoto wanaozaliwa na hitilafu katika miguu, imewawezesha watoto wengi kunufaika na huduma zilizotolewa.

Alimpongeza daktari huyo kwa kazi kubwa na nzuri aliyofanya katika kipindi chote akiwa nchini na kubainisha azma ya serikali ni kuvutia wahisani na wataalamu kwa kuzingatia kuwa haiwezi kuwafikia watoto wote wenye mahitaji.

Pamoja na daktari huyo kupitia changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa shughuli zake, alisema amechangia kwa kiasi kikubwa ustawi wa maisha ya watoto.

Dk. Mwinyi alimwomba daktari huyo kuendelea na juhudi za kusaidia jamii katika kukabiliana na changamoto hiyo, huku akiahidi serikali yake kumpa kila aina ya ushirikiano kufanikisha malengo yake.

Naye Dk. Hawkins, aliipongeza serikali ya Zanzibar kwa mabadiliko makubwa yanayofanyika katika kuimarisha sekta ya afya.

Kwa upande wake, Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, alisema Dk. Hawkins Hawkins amekuwa Zanzibar kwa miaka 13 sasa akisaidia juhudi za serikali katika kukabiliana na changamoto zinazowakabili watoto wachanga wanaozaliwa wakiwa na miguu yenye hitilafu.

Alisema katika kipindi hicho amefanya kazi kubwa na nzuri ya kutoa huduma katika Hospitali ya Abdalla Mzee Kisiwani Pemba kwa kuboresha miguu bandia pamoja na kutengeneza viatu vya ngozi, ikiwa ni hatua ya kwanza ya kuondoa hitilafu ya miguu kwa watoto.

Pia alisema Dk. Hawkins amesaidia kwa kiasi kikubwa kujenga uwezo na kurekebisha miundombinu katika shule mbalimbali ambazo watoto wenye hitilafu ya miguu wanasoma.


JUMAMOSI OKTOBA 1, 2022

Nipashe

MWANGA WA JAMII

BT

BURUDANI TELE

# BARNABA

## usiwe mkali, jibu hoja wakuelewe

YUKO WAPI ?

# ABDUL PANGAMAWE

## Aliajiriwa akiwa na miaka 17 Msondo
## Pesa alizotunzwa zilimponza



**Na Adam Fungamwango**

HEBU fikiria, mtoto wa miaka 17 ambaye anatakiwa alale nyumbani ili kesho awahi shule, lakini unamkuta jukwaani akiwa anapiga muziki, tena kwenye bendi kubwa nchini Tanzania, Juwata Jazz band maarufu kama Msondo Ngoma.

Unapoona kwa mara ya kwanza ni lazima ushangae, utajiuliza kwa nini mtoto kama yule anapiga muziki badala ya kuwa muda huo amepumzika nyumbani.

Pia, utashangaa umahiri wa mtoto mwenyewe kiasi cha kuaminiwa kuwa pale, tena mbele ya wanamuziki wakubwa.

Hivi ndivyo ilivyokuwa na mwanamuziki Abdul Ridhiwani Pangamawe. Ni mwanamuziki ambaye tangu ajiunge mwaka 1980 hadi leo yupo na bendi hiyo hiyo, akidumu kwa miaka 42 bila kuhama.

Alijiunga akiwa mdogo tu wa miaka 17, huku mwenyewe akielezea kisa cha kujiunga kwake kikiwa cha kufurahisha na kushangazwa kwa wakati mmoja.

"Nilitoka mkoani Iringa nikaja Dar es Salaam kwa kaka yangu kwa ajili ya masomo, lakini kabla ya hapo nilikuwa naishi tu nyumbani. Nilikuwa bado mdogo wa miaka 17 nikiwa na akili za kitoto sana na hata kujiunga kwangu Msondo, bendi kubwa Tanzania ilikuwa kwa bahati na hedi leo hii nikifikiria siamini," anasema Pangamawe na kuendelea.

"Ndugu zangu walikuwa ni mashabiki wa Msondo na eneo jirani alipokuwa anaishi mwanamuziki Joseph Lusungu. Nakumbuka wakati huo Waziri Ally ambaye sasa ni marehemu alikuwa ameihama Msondo na ikawa na pengo kubwa kwenye upigaji wa kinanda," anasema pangamawe.

Kisha, anaendelea "Niliambiwa kuwa walikwenda wanamuziki wakubwa kabisa kujaribu bahati yao kutaka kuziba pengo lake, lakini hakuna aliyefuzu. Lusungu alikuwa anapita yumbani, akisalimiana na kaka yangu anamwambia nina mdogo wangu hapa anajua kupiga kinanda, atawasaidia. Halafu nikirudi kucheza na watoto wenzangu ananiambia, Msondo wanakuhitaji ukawapigie kinanda, mimi nilikuwa nacheka, unajua ni utoto wala siamini, na hata kama nikienda nilijua nitapiga tu kwa sababu nafahamu,"

Kwa kifupi tu, Pangamawe hadi anafikia umri huo alikuwa anajua kupiga magitaa yote, solo, rhythm, na kinanda kutokana na kwamba baba yake mzazi alikuwa mwanamuziki wa Highland Stars iliyosambaratika mwanzoni mwa miaka ya 1960.

Vyombo vya muziki vya bendi hiyo vilikuwa vikikaa nyumbani kwao na yeye alikuwa akijifunza kwa kujificha kwa sababu baba yake hakutaka hivyo, kwani ingeweza kumsababishia asipende shule.

"Kwa sababu kaka yangu alijua naweza kupiga kinanda, alimsisitizia Lusungu hadi akamwambia kesho nakuja kumchukua. Kwanza aliponiona mwenyewe alishangaa, akauliza ndiyo huyu? Lakini kwa heshima ya kaka akakubali kunichukua. Nikafuatwa kesho yake na gari Land Rover ya Juwata. Kwanza watu walinishangaa, mtoto mdogo kapanda gari la Juwata, mwenyewe nimevaa raba mtoni zangu, we acha tu," anakumbuka mwanamuziki huyo ambaye baadaye alikuwa mpiga gitaa la solo mahiri.

"Nilifika hapo, lakini haikuwa rafiki kama nilivyodhani. Kwanza nilishindwa kukipiga. Tatizo ni kwamba kinanda kile kilikuwa tofauti na kile cha kule nyumbani. Hiki cha Msondo kilikuwa kikubwa na muundo tofauti. Kilikuwa cha kisasa sana. Lusungu akaniambia nipige nikashindwa kabisa. Hebu piga 'bluzi' nikashindwa. Akakasirika na kuondoka," anaelezea.

Anakumbuka alikuwa kwenye mazoezi ya bendi hiyo katika ukumbi wa Amana Social Hall, kinanda kilikuwa kwenye chumba kimoja ndani.

Anasema kuwa alipokuwa peke yake, alianza kukikagua na kuangalia sehemu ambazo anaweza kukipiga, na kwa sababu hakuwa na presha ya kusimamiwa na mtu, taratibu akaanza kupiga kwa ufasaha.


"Kuna wimbo wa Msondo uitwao 'Epuka Tabia Mbaya', nilikuwa najifundisha kupiga nikiwa nyumbani Iringa, nikaanza kuupiga, kumbe kiongozi wa bendi Saidi Mabera alikuwa anakuja mazoezini, alipofika mlangoni kabla ya hajafika ukumbini akasikia sauti ya kinanda kinapigwa kwa ustadi akawa anajiuliza ni nani.

Aliingia kwenye chumba. Pangamawe hakumuona na aliendelea kupiga, ghafla alikasikia sauti ikisema 'enhee ongeza hapo kidogo', alishtuka, akaondoka na kwenda kuwaambia wenzake kuwa yule dogo anaweza.

Pangamawe anasema baada ya hapo walikuja wote ndani na kumkuta akipiga kwa ustadi kwani tayari alishaanza kukizoea.

**Itaendelea wiki ijayo**

# UDAKU TU



## Kili Paul kaalikwa na Shahrukh Khan?

UNAWEZA kusema kama utani vile, lakini msanii maarufu wa kuimba nyimbo za Kihindi katika mtandao wa Tik Tok, Kili Paul amekwea pipa na kwenda nchini India kutokana kupewa mwaliko maalum.

Kili, ambaye ni kijana wa kimasai kutoka kule Bagamoyo mkoani Pwani, amejizolea sifa kem kem kutokana na uhodari wake wa kuimba nyimbo za mastaa wa filamu kutoka nchini humo.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Kili ameweka picha akionekana akiwa ndani ya ndege na kuandika kwamba yupo njiani kelekea India na kuwaomba mashabiki wake nchini humo wataonana usiku.

Hata hivyo, kuna taarifa ambazo hazijathibitishwa kwamba Kili amealikwa na mwigizaji maarufu Shahrukh Khan kufanya ziara maalumu.

Haijafahamika nini anakwenda kufanya akiwa nchini humo, lakini taarifa kutoka vyanzo mbalimbali vinasema inawezekana Kili akashirikishwa katika filamu ya mmoja wa wasanii maarufu.

Miezi michache iliyopita, Kili alionekana akiwa katika ofisi ya ubalozi wa India hapa nchini, akifuatilia taratibu za usafiri.

Kama taarifa hizo ni za kweli basi Kili atakuwa msanii wa kwanza Tanzania kukutana na Khan ana kwa ana.

Kutokana na habari hiyo njema baadhi ya mashabiki wake nchini humo waliingia katika ukurasa wake kwa wingi na kuanza kumkaribisha kwa furaha

**@monika.9819** ameandika karibu sana India, huku

**@sonirawat297** akimwambia karibu Mumbai

## INSTA-TWITTER

Tuffolow/ Tu-tag

**@burudanitele**



**@billnass**
Mama, Nakupenda sana mke wangu my pyg kuna muda maneno hayatoshi kuelezea upendo @official-nandy !


**@shamsaford**
Inshaaallah Mwenyezi Mungu atuepushe na roho za visasi hata tunapokosewa.. Ijumaaa kareem






**@officialabdukibaa**
Eti SImba? Simba ni sifa, Simba analiwa, Simba anafugwa? Simba anazaa, bado anazaliwa @officialalikiba

**@mlelandro**
Sio kila mtoto anayefeli darasani kuwa hana akili au haelewi. Lakini kuna mtoto anakutana na mazingira magumu kutoka nyumbani hadi anapofika darasani yanayomfanya apoteze umakini na kutokufurahia elimu yake. #Samia, nivishe viatu.





**@whozu_**
Ona mwenzako nang'ang'ana, wanatamani tukorofishane wana wivu wivu..Mimi Chibaba we Chimama, Halua mwenzake Tende isiwe chumvi itaharibu.Kasura macho ya gololi,Mtamu uko sweet sweet laini, Kishori, Nikikosea ntaomba Sorry,Usije ukani cheat cheat wanafki wapate Story

BASI SAWA

## Bien Melody afikiria kuoa



Mwanamuziki wa kizazi kipya mwenye makazi yake nchini Australia, Bien Melody, ameweka wazi mpango wake wa kuvuta jiko mapema mwakani baada ya kuwa singo kwa muda mrefu.

Melody, anayetamba na wimbo 'Single Boy', ameliambia BT kuwa kwa sasa amekuwa mtu mzima ndiyo maana ameamua kufanya maamuzi hayo.

"Nimekuwa mwenyewe kwa muda mrefu, sasa nimepanga kuwa mume wa mtu, naweza kuoa popote hapa Australia au huko nyumbani Afrika kwasababu kote kuna wanawake wazuri wenye sifa za kuwa mke," amesema Bien.


## Jaffarai akataa umaskini



Mwanamuziki wa bongo fleva, Jaffarai amesema ukimya wake una mambo muhimu ya kufanya baada ya kuacha muziki zaidi ya miaka kumi.

Jaffarai, ameiambia East Africa TV kuwa wakati wote anafanya kazi katika kampuni yake ya kuosha magari na kwamba huko kunamuingizia kipato cha kutosha.

Pia, amefunguka kuhusiana na mkasa uliowahi kumkuta miaka ya nyuma wa kuvamiwa na kundi la watu zaidi ya 100 akiwa maeneo ya Coco Beach, Dar es Salaam



## BARNABA USIWE MKALI, JIBU HOJA WAKUELEWE

MKALI wa Muziki wa Bongo Fleva, Barnaba Classic amekasirishwa na kitendo cha kujadiliwa kutokana na kusaidiwa na Diamond, akieleza suala hilo linakuzwa kutokana na urafiki.

Amesema, kusaidiwa na Diamond kufanya Album yake mpya ya Love Sounds Different, sio suala ajabu kwani hata kama msanii ana kipaji, lakini anatakiwa kupata ujuzi na maarifa ili kufika safari yake.

"Kutangulia si kufika, ukipata kumi unaweza kushuka, tunajadili vitu havina mpango, hakuna ubaya Diamond Platnumz kunisaidia bila kupata chochote," amesema Barnaba.





## Danzak unataka kuyeyusha tu

MWANAMUZIKI wa BongoFleva,Danzak amekana fununu kuwa yuko kwenye uhusiano wa kimapenzi na staa wa filamu Bongo, madam Wema Sepetu.

Akizungumza katika kipindi cha Friday Night Live cha East Africa TV na Radio, Danzak amesema yeye na Wema wana ukaribu wa kawaida na hakuna suala lingine nyuma ya pazia.

"Wema ni mwanangu sana, mshkaji wangu na rafiki yangu sana. Sijui kwanini wananiita mimi shemeji wa Taifa mnanipa kesi tu ila nampenda na historia yake ina-inspire sana" amesema

Kwa sasa staa huyo wa filamu Wema Sepetu inasemekana yupo penzini na msanii Whozu.

## MIAMBA YA MAGALATONI HAWA HAPA

**Na Adam Fungamwango**

WIKI iliyopita tuliangalia nyimbo tano zilizopigwa kwa mtindo wa 'twist' zilizochangua Watanzania wegi.

Tulikuwa na nyimbo kama 'Tanganyika Twist', 'Msichana wa Elimu', na 'African Twist' wa Daudi Kabaka, 'Taxi Driver' wa Fadhili William na 'Angelike wa John Zenze.

Hizi ni nyimbo zilizopigwa miaka ya zamani sana kuanzia 1940, 1950 mpaka 1960 ambazo zilivuma na kuwa na wapenzi wengi nchini Tanzania.

Leo, tutawaangalia baadhi ya wanamuziki wa miaka hiyo ambao walitamba na kuwa maarufu sana Tanzania na Afrika Mashariki na Kati kwa ujumla.

Ni miaka ambayo teknolojia ilikuwa bado, hivyo nyimbo nyingi za wanamuziki hao zilipigwa na magitaa baridi, yaani yasiyotumia umeme, maarufu kama 'magalatoni' zikihamishwa mapigo ya chupa, ngoma, au manyanga, mbao, au bati ili kunogesha muziki. Hakukuwa na nyombo vingi.

**Omari Kungubaya-Tanzania**

Huyu ni mwanamuziki Mtanzania ambaye umaarufu wake unatokana na wimbo wa 'Salamu za Wagonjwa', ambao ulikuwa ni kiashirio kwenye kipindi cha Redio Tanzania Dar es Salaam (RTD) kiitwacho 'ugua pole'.

Kilikuwa ni kipindi ambacho mtangazaji kutembelea wagonjwa kwenye hospitali mbalimbali nchini, kuwahoji, kuwafariji, wakipata wakati wa kusalimia ndugu zao wa kuomba nyimbo.

Kungubaya, mpiga galatoni aliyezaliwa 1939 na alianza kujifunza muziki akiwa na miaka 16 kwenye bendi ya Cuban Marimba ya Salum Abdallah, baadaye akawa mwanamuziki mkubwa hadi alipofarikiOktoba 20, 2016 nyumbani kwake Njeteni, Mbezi ya Kimara.

**Daudi Kabaka-Kenya**

Huyu anatajwa kuwa ndiye baba au mfalme wa nyimbo za 'twist' Ukanda wa Afrika Mashariki. Kabaka alikuwa mwanamuziki raia wa Kenya, ingawa inadaiwa asili yake ni nchini Uganda akitokea kwenye ukoo wa mfalme Kabaka.

Pia, alipiga muziki staili ya 'benga' na ndiye mwanamuziki, nyimbo zake nyingi zilipendwa mno ukanda huu na akapachikwa jina la 'Mtoboa Siri' kutokana na kufichua ukweli ambao watu hawataki kuusema.

Baadhi ni 'Harambee', 'Western Shilo', 'Helule Helule', 'Msichana wa Elimu', 'Bachelor Boy', 'Tanganyika Twist', 'Mulofa Mmoja' na nyingine nyingine nyingi. Alizaliwa 1939 na kufariki 2001.

**Jean-Bosco Mwenda-Congo**

Anatajwa kama ndiye mtaalamu wa kupiga galatone kwenye ukanda wa Afrika Mashariki na Kati. Nyimbo zake zilipendwa sana hapa nchini, Kenya na ukanda wote. John Mwenda Bosco wa Bayeke kama anavyopendwa kuitwa na mashabiki wake, alizaliwa 1930 nchini Congo ya Ubelgiji sasa inaitwa Congo DR, na alivuka mipaka kwenda nchini Kenya miaka ya 1950 hadi 1960 ambapo alivuma na nyimbo zake nyingi zina mashabiki hadi leo.

Moja ya nyimbo zake bora ni ule unaosikika kwenye kipindi cha 'zilipendwa' cha RTD, ambapo gitaa baridi limepigwa kwa ustadi mkubwa. Unaitwa 'Masanga'. Nyingine ni 'Bibi Mpenzi' na 'Mama na Mwana' Alifariki 1990 nchini Zambia kwa ajali ya gari.

**George Mukabi-Kenya**

Muda wake mfupi tu wa kuishi duniani mwanamuziki huyo mzaliwa wa Kenya, alifanya makubwa na kurekodi nyimbo mbili ambazo zilitetemesha mno.

Hizo ni 'Sengula Nakupenda' na 'Mtoto si Nguo'. Huyu ni Gerge Mukabi, mwanamuziki aliyeibuka ghafla kuwa maarufu ambao hakuufaidi kabla ya kuuawa kama mnyama.

Kuuawa kwa mpiga galatone huyo ni kisa cha kusikitisha ambacho kipo kwenye gazeti la kesho Nipashe Jumapili safu ya Burudani Iliyotikisa.

Alizaliwa Kakamega Kenya 1930 na kufariki 1963 akiwa bado kinda tu wa miaka 33, lakini nyimbo zake hizo zikiendelea kutamba hadi leo.

**Charles Sonko-Uganda**

'Please baby love me, sikulavuu, bai bai go.' Ni baadhi ya rap ambayo imo kwenye baadhi ya nyimbo za TOT Plus Band, kipindi hicho ikiwa na Papy Kocha. Hayo maneno asili yake ni wimbo wa 'Please Baby' wa Charles Sonko, mmoja wa wapiga magalatone wakati huo. Alikuwa akipenda kuimba na dada yake Frida Sonko ambao walikuwa wanamuziki maarufu sana wa aina hiyo ya miondoko, wakiwa raia wa Uganda.

FILAMU

## Mona: Maji matamu nenda mwenyewe kisimani

**Na Adam Fungamwango**

SIKU zote kitu kizuri ni kile ambacho umekihangaikia mwenyewe. Wakati mwingine tusipende sana kutuma kwa sababu si vitu vyote vya kutuma kwa sababu yeyote ile unatakiwa kwenda mwenyewe.

Mifano inaweza kuwa mingi sana, lakini mmoja wapo ni kwamba kama unataka maji ili umalize kabisa kiu yako, nenda kisimani au bombani na si kumtuma mtu akakuchotee kwenye kata au kikombe.

Mafunzo kwenye hili hebu tuyaangalie kwenye filamu hii iitwayo 'Mona'. Imechezwa na Selemani Kitola akicheza kama Sobo, Nasra Juma kama Mona mwenyewe au Melisa, Bakari Lungamo kama Vance, Shaaban Athumani aliyecheza kama Zomwa, Khalid Athumani kama Ndoza na Rajab Hassan kama Bobby.

Inaanza kwa kuonyesha kuwa,0 kwenye kijiji fulani hapa nchini kuna msichana mmoja mzuri aitwaye Mona. Alikuwa mrembo kuliko msichana yeyote kijijini hapo.

Kila kijana alimpenda, lakini wengi walikuwa waoga. Walioonyesha angalau ujasiri na kukabiliana naye ni Sobby na Vance tu.

Sobby alikutana na msichana huyo njiani, lakini akampigisha stori nyingi za kupindishapindisha. Hakulekekea kwenye njia iliyonyooka, hivyo kwa msichana hata kama amekuelewa inakuwa ngumu kukubali.

Alivyoona hawezi kumwambia mambo yake moja kwa moja, akaamua kumwita rafiki yake Vance na kumueleza lililo moyoni mwake.

Akamwambia anampenda sana Mona na anataka awe mpenzi wake, ikiwezekana amuoe, lakini tatizo jambo hilo hawezi kumwambia wakiwa laivu. Kwa hiyo akamtuma Vance akamwambie maneno hayo.

Vance akakubali, akaenda kumkabili Mona. Lakini kwa sababu na yeye alimpenda na alikuwa ana hofu ya kukabiliana naye, kutumwa huko kukawa kumempa nafasi ya kupata ujasiri wa kusimama naye.

Alipokutana naye njiani akamweleza maneno yote aliyoelezwa na Sobby amwambie Mona. Tofauti ni kwamba Vance hakusema kama maneno hayo yametoka kinywani mwa Sobby bali ni yeye mwenywe. Demu akamuelewa na kumkubali.

Likaanza penzi changa kati ya Vance na Mona. Lilikuwa ni pigo kuu kwa Sobby. Ndipo alipoelewa kuwa rafiki yake amemzunguka, Akaenda kumwambia rafiki yake mwingine Ndoza. Huyo alimpa makavu Sobby kwa kumwambia vitu vingine si vya kutuma.



Kitu kama hicho unatakiwa uende mwenyewe. Akaongezea kuwa hata angemtuma yeye angefanya hivyo hivyo, lakini akamshauri akakutane na Mona laivu ili umueleze kilichotokea.

Ukawa ugomvi mkubwa kijijini kati ya Sobby na Vance. Siri ikagundulika kuwa Vance alitumia nafasi ya kuagizwa na rafiki yake Sobby 'akamsomeshe' demu ili kumpata yeye.

Mona aliposikia hilo, akaamua kubadilisha kibao. Akaanza kumpenda Sobby, na Vance akapigwa chini. Kwa hasira Vance akamuua Sobby. Naye akahukumiwa kifungo cha maisha. Mona akaendelea kubaki pekee.

BARIZI LA PWANI

# Siti Binti Sadi chimbuko la Taarab asili

KIZAZI cha sasa wanapolisikia jina la Siti Binti Saad, huwa wanajiuliza ni nani na alikuwa wapi?

Maswali hayo si kana kwamba wanakejeli, lakini ni wazi hawamtambui na wanahitaji msaada kumfahamu. mwanamke huyo mahiri katika muziki wa taarab aliyesifika miaka 1900.

Mwanamke huyo mahiri anatoka kisiwa cha Unguja, Zanzibar, aliivunja miiko ya Taarab na akawa mwanamke wa kwanza ambaye hajasoma kuimba mtindo huo wa muziki kwa Lugha ya Kiswahili.

Siti binti Saad aliishi wakati gani?

Siti binti Saad, alizaliwa mnamo mwaka 1880 katika kijiji cha Fumba, Alizaliwa katika familia masikini na aliuza vyungu vya udongo barabarani kabla ya kuhamia Zanzibar mjini mwaka 1911 ambako sasa kunapojulikana sasa kama Stone Town.

Akiwa hapo alianza kufanya kazi na wanamuziki, akawa muimbaji maarufu wa muziki wa aina ya Taarabu. Aliendelea kuwa mwanamuziki wa Taarab hadi uzeeni. Alifariki mwaka 1950.

Siti binti Saad anajulikana kwa kipi?

Siti binti Saad, alikuwa ni nyota wa miondoko ya muziki wa taarabu, muziki ambao yeye mwenyewe aliupenda sana. Alikuwa na sauti nzuri na ya kuvutia, alialikwa kutumbuiza katika nyumba ya sultani.

Lakini Siti binti Saad hakuwaimbia tu wasomi, alitumbuiza pia mbele ya mihadhara ya watu wa kawaida na nyumba yake ilikuwa mahala pa kubadilishana mawazo na kufanyia mijadala.

Kipi kilimfanya kuwa mwasisi wa Taarab?

Kabla yake, muziki wa taarabu ulikuwa unatumbuizwa na wanaume wasomi ambao mara nyingi waliimba kwa lugha ya kiarabu, lugha iliyokuwa ikitumiwa na wasomi wachache wa kisiwa cha Zanzibar.

Siti binti Saad, ambaye hakuwa na elimu rasmi alikuwa ni mwanamke wa kwanza aliepata umaarufu kwaajili ya uimbaji na aliupa umaarufu muziki wa taarabu kwa kuimba kwa lugha ya kiswahili.



Kutokana na umaarufu wake, kampuni ya Gramophone ya Uingereza ilimpeleka Bombay nchini India kuirekodi sauti yake, na kumfanya kuwa mwanamke wa kwanza kutoka Afrika Mashariki kurekodi muziki na kutengeneza albamu kwa ajili ya mauzo.

Nyimbo za Siti bint Saad zinahusu nini?

Nyimbo zake zinahusu maisha ya kila siku ya watu wa Zanzibar na zinazungumzia kuhusu matukio halisia. Zimebeba maudhui ya kuikosoa jamii, kupinga unyanyasaji wa matabaka, rushwa, unyanyasaji kwa wanaume na wanawake na mapungufu ya mfumo wa kisheria. Kwa namna hiyo, nyimbo za tarab zilizokuwa zikiimbwa na Siti binti Saadi zilikuwa ni siasa ya hali ya juu.

Siti Binti Saad alitunga na kuimba nyimbo zaidi ya 250, lakini nyimbo chache sana ndio zilizobaki hadi hii leo. Nyimbo zake zinachezwa sana Zanzibar, Tanzania na nje ya Tanzania. Nyimbo zake ni sehemu kubwa ya bendi nyingi za taarab.

Aude Gensbittle, Salma Said na Gwendolin Hilse wamechangia kuandika makala hii. Ni sehemu ya makala maalum za mfululizo wa "Asili ya Afrika",.

**Kwa msaada wa mtandao**



## BATA LA WIKI

Je una kiwanja cha burudani piga -0717336368

**TOT-Band na Taarab**

Bendi ya muziki wa dansi na taarab ambayo yako chini ya TOT, wikiendi hii wameamua kujichimbia mjini Morogoro wakifanya vitu vyao huko ambako ni maarufuku kama 'Mji Kasoro Bahari' Morogoro wakifanya vitu vyao huko

**Tukuyu Sound.**

Kila Ijumaa wapo ukumbi wa TTG Kimara Korogwe, Jumamosi huwa wapo ukumbi wa Mikocheni na Jumapili wanamalizia wikiendi yao katika ukumbi wa Mawasiliano Park Ubungo.

**Msondo Ngoma**

Ijumaa wanatoa burudani katika ukumbi wa Gwambina Lounge Chang'ombe, Jumamosi wapo Makutano Park Vikindu mkoani Pwani, na Jumapili wanakuwa ukumbi wa Dar Safari Buza Dar.

**Twanga Pepeta**

Kila Ijumaa wapo Mawasiliano Park Ubungo, Jumamosi ndani ya ukumbi wa Andrews Lounge Sinza na Jumapili wanawasha moto, katika ukumbi wa Gwambina Lounge Chang'ombe.

**Kimokimo Band**

Bendi hii ambayo inaongozwa na mwimbaji wa siku nyingi Khadija Kimobitel, hutoa burudani siku mbili kwa wiki ambapo Ijumaa wapo Kontena Kibaha mkoani Pwani na Jumamosi, katika ukumbi wa Kijichi Royal Garden Dar.

**Mambo Live Band**

Kila Ijumaa inafanya vitu vyake katika ukumbi wa The Crown Pub, kisha Jumamosi inakuwa ndani ya ukumbi wa Village Hotel.

**Maina Band**

Wao huanza kutoa burudani siku ya Alhamisi, katika ukumbi wa The Marz, Namanga, Ijumaa wapo Regancy Park, Jumamosi External na Jumapili wanamalizia wikiendi ndani ya ukumbi wa Trinity Oysterbay.

**Bogos Musica**

Bendi hii chini ya Nyoshi El-sadat, Ijumaa huwa inatoa burudani katika ukumbi wa Masai Bar Mwananyamala, Jumamosi ipo ndani ya ukumbi wa Muungano Park Kivule na Jumapili inakuwa Board Room Sinza Mori.

**Waluguru Original**

Bendi hii inafanya shughuli zake mjini Morogoro, hutoa burudani kuanzia Alhamisi katika ukumbi wa Didi's Break Point Iringa Road, Ijumaa ndani ya ukumbi wa Kambarage SUA, Jumamosi wapo Terminal Pub Msamvu na Jumapili wapo eneo hilo, katika ukumbi wa F2 Florida.



# SHAKIRA KUPANDISHWA KIZIMBANI HISPANIA

**BARCELONA, Hispania**

MALKIA wa muziki wa pop kutoka nchini Colombia, anayefanya kazi zake Marekani, Shakira anatarajiwa kupandishwa kizimbani kwa madai ya ukwepaji kodi.

Mahakama moja katika mji wa Barcelona nchini Hispania imeamuru Shakira kupandishwa kizimbani kukabiliana na mashitaka ya udanganyifu wa kodi inayokisiwa kufikia zaidi ya euro milioni 14.

Shakira, ambaye jina lake halisi ni Shakira Isabel Mebarak Ripoll anakabiliwa na kesi hiyo baada ya kukwepa kodi kipindi anaishi nchini humo na mumewe Gerard Pique mchezaji wa timu ya Barcelona ambaye alifunga naye ndoa mwaka 2011 na kutalakiana mapema mwaka huu.

Mahakama hiyo imeamua kuwa kesi hiyo inapaswa kufanyika, hata baada ya mwanamuziki huyo kulipa kiwango kilichodaiwa na mamlaka ya kodi ya Hispania, pamoja na riba ya euro milioni tatu.

Julai mwaka huu, waendesha mashitaka walisema wangeiiomba mahakama imuhukumu mwanamuziki huyo mwenye umri wa miaka 45 kifungo cha miaka nane jela.

Shakira anatuhumiwa kudanganya kwamba haishi Hispania, wakati alikuwa akiishi nchini huko pamoja na Pique.

Wawili hao, ambao wamezaa watoto wawili, walitangaza kutengana Juni mwaka huu.




# DJ Cuppy hatimaye kafaulu

DJ maarufu nchini Nigeria, DJ Cuppy, amesema baada ya kufanya vibaya mitihani yake ya chuo, hatimaye majibu yake yametoka na kuonyesha amefaulu.

Kupitia ukurasa wake wa Twitter, DJ Cuppy, amesema japo matokeo hayo hayapo vizuri sana, lakini anamshukuru Mungu alama alizopata zinamtosha kupata cheti.

"Nimepata matokeo yangu ambayo yanaainisha shahada yangu ya MSc, sikupata ubora wa juu lakini nimefaulu baada ya mwaka mgumu, naweza kusema rasmi sasa ni mhitimu kutoka UniofOxford," ameandika DJ Cuppy.



## Kanye West amuomba radhi Kim

RAPA nyota wa Marekani Kanye West, amemuomba msamaha aliyekuwa mke wake Kim Kardashian, kutokana kile anachoamini kwamba alimsababishia msongo wa mawazo wakati wakiachana kwa fujo.

Rapa huyo bilionea alifahamisha hayo wakati akihojiwa na 'Good Morning America, amesema Kim ni mama wa watoto wake na pale anapoona amefanya kosa ni muhimu kumuomba radhi.

"Huyu ni mama wa watoto wangu, naomba radhi kwa mfadhaiko wowote niliopata, hata katika kuchanganyikiwa kwangu, kwani Mungu ananiita niwe na nguvu zaidi," amesema kanye kupitia ukurasa wake wa Instagram.

## Toke anataka kupumzika akiwa kijana

MSANII wa filamu na mtangazaji wa redio nchini Nigeria, Toke Makinwa, hatimaye amestaafu baada ya kufanya kazi katika kituo cha habari kwa miaka 12.

Nyota huyo amefunguka kupitia ukurasa wake wa Instagram kwamba anafurahia mafanikio yake tangu alipoanza kama mtangazaji wa kujitolea hadi kupata umaarufu.

Katika kile kilichoonekana kuwa cha kutia moyo, aliandika: "Hii imenichukua muda mrefu sana kushiriki lakini hapa ninaaenda. Imepita miaka 12 tangu siku yangu ya kwanza kwenye redio, na hatimaye nilipiga magoti kumshukuru Mungu,"





## Cormier afariki dunia

MWIGIZAJI Robert Cormier, anayejulikana sana katika kazi yake katika filamu ya "Heartland," amefariki dunia baada ya kuanguka.

Dada yake, Stephanie, aliambia Mwandishi wa Hollywood kwamba Robert alifariki Ijumaa katika hospitali ya Ontario, CA, kutokana na majeraha aliyoyapata wakati wa alipoanguka .

Hata hivyo, haikuelezwa sababu ya msanii huyo kuanguka hadi kusababisha kifo chake.

## Livine, Behati hawaambiwi kitu

MWANAMUZIKI wa Marekani, Adam Levine na mke wake Behati Prinsloo, penzi lao linazidi kuimarika zaidi baada ya siku kadhaa kukabiliana na tuhuma ya kutoka nje ya ndoa.

Wawili hao, wakiwa na furaha walipanda ndege wakiwa pamoja huku wakionekana katika hali ya kimahaba.

Adam na Behati ambaye ni mjamzito walichukua ndege binafsi kutoka Santa Barbara hadi Las Vegas siku ya Jumanne kwa ajili ya kula bata.

Wanandoa hao hawaonekani kuwa katika msukosuko kutokana na kashfa ya hivi karibuni ya Adam ya kuwa na uhusiano na mwanamke mwingine.



MAKALA

# Wakati Uganda ikihangaika na Ebola, Tanzania, Kenya zajiandaa kuudhibiti

**Na Mwandishi Wetu**

HIVI karibuni Rais wa Uganda Yoweri Museveni, ameondoa hofu kwa raia wa nchi hiyo ambao wengi waliamini angetangaza karantini katika hatua za kudhibiti mlipuko wa ugonjwa hatari wa Ebola.

Rais Museveni, ameeleza kuwa ipo haja ya kuweka vizuizi kwa sababu ameona kuna urahisi wa kudhibiti maambukizi ya Ebola ikilinganishwa na virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa COVID-19.

Mpaka mwishoni mwa wiki, waathirika wametajwa kuwa 31 na kwamba idadi kubwa wako katika wilaya tatu zilizo jirani.

Shirika la Afya Ulimwenguni WHO, limesema ugonjwa wa Ebola ulioanzia Sudan umeonesha kuenea kwa kasi na pia kiwango cha vifo ni cha chini tofauti na mlipuko wa hapo awali uliotokea nchini Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Congo ambapo karibu watu 2,300 walikufa mwaka 2018.

Hata hivyo, nchi za Tanzania na Kenya, inachukulia hatua hiyo kama kitisho na zimetangaza hatua mbalimbali ya kukabiliana na ugonjwa huo pale unapoweza kuvuka mipaka.

Wizara ya afya ya Tanzania, imechukua tahadhari baada ya kutangaza mikakati ya kujiweka tayari kukabiliana na ugonjwa wa Ebola.

Sehemu ya mkakati huo ni kuimarisha udhibiti katika maeneo ya mipakani baada ya Uganda kutangaza mlipuko huo wiki iliyopita

Hata hivyo, Tanzania haijathibitisha kisa chochote ya mtu mwenye maambukizi ya ugonjwa huo.

Waziri wa afya, Ummy Mwalimu amewaagiza waganga wakuu wa mikoa nchini kutenga vituo maalumu vitakavyotoa huduma za haraka kwa wanachi wanaohisiwa kuwa na dalili za ugonjwa huo.

Mikoa ambayo inapakana na mataifa ambayo tayari yamewahi kushuhudia visa vya maambukizi hayo ikiamriwa kuchukua hatua kuhakikisha huduma utambuzi inakuwepo kwa muda wote.

Waziri Mwalimu amesema licha kwamba hakuna kisa cha kuwepo kwa mgonjwa yoyote, lakini hiyo haimanishi serikali kutochukua hatua za kujilinda na kwa maana hiyo hatua zote zitazosaidia kujiweka kando na maambukizi

"Nawaagiza wakuu wa mikoa kote nchini kila mkoa kujiandaa" Alisema waziri ummy katika mkutano wake na waandishi wa habari.

Aidha amezitaka mamlaka za mikoa kutodharau aina yoyote ya tetesi kuhusiana na washukiwa wa homa hiyo na kuhakikisha eneo la mazishi linatengwa.

"Tukipata kifo cha mgonjwa wa Ebola leo tunapaswa kujua tutamuhifadhi wapi." Aliongeza waziri Mwalimu.

Amesisitiza kwamba kila washukiwa wanapaswa kutengwa kulingana na maelekezo ya wataalamu wa masuala ya afya.

Wananchi wajihadhari vipi?

Serikali imewaelekeza wananchi kujitafakari mara mbili kama kuna ulazima wa kufunga safari kwenda Uganda ambako kumeripotiwa kuibuka maambukizi ya ugoinjwa huo.

Kulikuwa na ripoti pia, serikali za mikoa hasa Kagera unaopakana kwa kilometa 230 ulikuwa katika tahadhari kubwa huku maafisa wa afya wakiwa kwenye maeneo hayo kuimarisha usalama.

Mkurugenzi wa huduma za kinga DK Beatrice Mutayoba, amesema serikali inaendelea kutoa uzito kuhusu tahadhari ya kinga dhidi ya maambukizi ya ugonjwa huo.

Aidha, amesema kuna haja ya wananchi kujielimisha kupitia wataalamu wa masuala ya afya juu ya virusi hivyo ambayo vinasababisha homa.

Mkoa wa Kagera unaotajwa kuwa hatarini zaidi kukumbwa na maambukizi ya ugonjwa huo, pia kuna mikoa mingine kadhaa ambayo inatumbukia kwenye hatari ya aina hiyo.

kama Mwanza, Kigoma, Geita na Mara.

Ugonjwa wa Ebola tayari umeyashambulia mataifa kadhaa barani Afrika na hivi karibuni, Jamhuri ya kidemokrasia ya Congo imetangaza kupata visa vya ugonjwa huo.



Kambi ya kuwatibu wagonjwa wa Ebola katika eneo la Mubende nchini Uganda.



Mfanyakazi wa afya katika hospitali ya wilaya ya Mubende nchini Uganda akiwa katika nguo maalum ya kujikinga na Ebola.

**Mikoa ambayo inapakana na mataifa ambayo tayari yamewahi kushuhudia visa vya maambukizi hayo ikiamriwa kuchukua hatua kuhakikisha huduma utambuzi inakuwepo kwa muda wote.**

**KENYA YAWEKA MGUU SAWA**

Wizara ya afya nchini Kenya imetangaza tahadhari katika kaunti 20 kati ya kaunti 47 kuwa maeneo yaliyo kwenye hatari maambukizi ya Ebola.

Aidha, nchi hiyo imesema tayari inaweka mikakati inayohitajika ikiwemo kuwachunguza wasafiri na kuunda vituo vya kuwatenga wagonjwa, ili kuzuia kusambaa kwa virusi hivyo.

Wizara ya afya imeunda mpango wa dharura utakaotoa mwongozo wa namna ya kuzuia na kupambana na virusi vya Ebola nchini humo.

Serikali imeunda kikundikazi cha kudhibiti Ebola, moja ya ajenda kuu ya kikundikazi hiki ni kutambua dalili za hatari, kufanya tathmini ya mara kwa mara, na pia kuimarisha uchunguzi wa watu katika maeneo ya mipaka ya nchi.

Kaimu mkurugenzi mkuu katika wizara ya afya, Dkt. Patrick Amoth, amesema kutokana na taifa hilo kuwa na muingiliano mkubwa na Uganda kuna haja ya kuchukua tahadhari hasa katika maeneo ambayo yana muingiliano mkubwa, kijamii, kibiashara na hata kiutamaduni.

"Kwa hiyo tunapozingatia kitisho hicho, tunatekeleza hatua za ufanisi kuhakikisha, kwanza, tunazuia mlipuko huo kuvuka mipaka." Amesema kaimu mkurugenzi mkuu huyo.

Aliongeza kuwa, iwapo ugonjwa huo utaingia,kutokana na muingiliano uliopo mamlaka hiyo imejiweka tayari katika kukabiliana na udhibiti wa maambukizi hayo ya homa hatari.

# Taasisi ilivyoona tatizo migogoro ya ndoa

- Yaandaa kongamano kutafuta njia za kuitatua, wanasaikolojia mahiri kutoa mada



**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI serikali ikiwekeza nguvu katika kukabiliana na majanga yanayoikabili nchi kama umaskini na tatizo la ajira, kuna tatizo limeibuka na kuhatarisha ustawi wa jamii na taifa.

Kadhalika viongozi wa serikali, kuanzia Rais Samia Suluhu Hassan, na wengine katika ngazi mbalimbali, wamekuwa wakikosa usingizi wakiwaza ni jinsi gani wanaweza kuiletea maendeleo nchi kwa kuboresha maisha ya Watanzania katika nyanja mbalimbali, zikiwamo huduma za afya na elimu.

Wakati hayo yakiendelea, kuna migogoro ya ndoa imezidi kushika kasi na kusababisha madhara mbalimbali kama vile mauaji, watoto kukosa malezi ya wazazi. Tatizo hilo la ndoa kwa sasa ni janga jipya la kitaifa ambalo kama hatua madhubuti hazitachukuliwa, kuna hatari ya taifa kuyumba.

Hiyo inatokana na ukweli kwamba ustawi wa taifa huanzia katika ngazi ya familia, hivyo kama familia zitakuwa katika migogoro na kuendelea kuwapo kwa matukio ya kutisha yanayohusiana migogoro ya ndoa, taifa haliwezi kuwa imara.

Hivi sasa migogoro ya ndoa na uhusiano wa kimapenzi pamoja na magonjwa ya afya ya akili vinavyosababisha vitendo vya ukatili na kuvunjika kwa ndoa na uhusiano husika, vimeshika kasi.

Matukio ya hivi karibuni yaliyotokea na kulitikisa taifa, ni vitendo vya wenza kufikia hatua ya kujitoa au kuwatoa wenzao uhai kutokana na kile kinachodaiwa kuwa ni wivu wa mapenzi, wazazi kukimbia familia, ukatili dhidi ya watoto na mengineyo kama hayo.

**WADAU WAJITOSA**

Kwa kutambua hilo, Taasisi ya Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), imeona ni vyema kuiunga mkono serikali katika kukabiliana na janga hilo ambalo limezidi kushika kasi kwa siku za hivi karibuni.

TaMCare, inayoundwa na wanataaluma wa fani mbalimbali, imeandaa kongamano la siku mbili litakalofanyika Oktoba 8-9, mwaka huu, mkoani Dar es Salaam ili kuelimisha jamii juu ya masuala ya ndoa, familia na malezi ya watoto pamoja na afya ya akili na ukatili.

Tukio hilo la aina yake, litaambatana na utoaji wa huduma za ushauri wa kisheria, msaada wa kisaikolojia, kisosholojia na upimaji hiari wa afya kwa wananchi bila malipo.

Akizungumzia kongamano hilo, Mkurugenzi Mtendaji wa TaMCare, Dk. Enock Mlyuka, anasema katika utoaji wa huduma hizo, watashirikiana na Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA) na Taasisi ya Ustawi wa Jamii ambayo ni mshirika wao.



"Kongamano hili la aina yake, litafanyika katika ukumbi wa Maktaba Mpya ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) Oktoba 8-9, mwaka huu, likitarajiwa kushirikisha watu kati ya 700 na 1,000," anasema Dk. Mlyuka.

"Tutashirikiana na TAWLA na Taasisi ya Ustawi wa Jamii ambayo ni mshirika wetu katika kongamano hili katika kutoa huduma za ushauri wa kisheria, msaada wa kisaikolojia, kisoshiolojia pamoja na upimaji wa afya kwa hiari bila malipo.

"Mada Kuu katika kongamano hili ni Ustawi wa Ndoa na Familia Msingi wa Maendeleo na Mapambano dhidi ya Ukatili na Mgeni Rasmi atakuwa ni Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima," anasema.

Dk. Mlyuka anazitaja mada zingine zitakazowasilishwa kuwa ni Msingi wa Ndoa na Familia, Uongozi wa Familia katika Jamii Inayobadilika, Malezi na Makuzi ya Watoto, Msongo wa Mawazo, Afya ya Akili na Uhusiano na Ukatili katika Familia, ikiwamo Utandawazi, Mila na Utamaduni wa Kiafrika.

Walengwa katika kongamano hilo ni wanandoa, wazazi wasio na wenza na vijana wanaotarajiwa kuingia katika ndoa jijini Dar es Salaam na kwingineko.

Anawataja watoa mada baadhi katika kongamano hilo lisilo na kiingilio kuwa ni Mwanasaikolojia Dkt. Chris Mauki, Mkuu wa Polisi wa Mkoa wa Kipolisi (RPC) Ilala ACP Debora Magiligimba na Mshauri Nasaha na Mwanasaikolojia Esther Mollel.

Wengine ni Mshauri Mwandamizi Dk. Katanta Simwanza, Mratibu Kitaifa THRDC Wakili Msomi Onesmo Olengurumwa, Mhadhiri Mwandamizi Taasisi ya Ustawi wa Jamii (ISW) Dk. Zena Mabeyo, Sheikh wa Dar es Salaam, Dk. Alhad Mussa Salim na Askofu Jackson Sosthenes wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Dar es Salaam.

"Tunapenda kuwakaribisha wakazi wa Dar es Salaam na maeneo ya jirani kujitokeza kushiriki katika kongamano hili ambalo tunaamini litakuwa la kipekee na lenye umuhimu mkubwa kwa jamii yetu ya Tanzania," anasema Dkt. Mlyuka.

Kongamano hilo, anasema linatarajia kugharimu zaidi ya Sh. Milioni 29 ambazo zinatolewa na wafadhili mbalimbali na kuwaomba wadau zaidi kulichangia.

"Tunawaomba wadau kujitokeza kutuunga mkono katika jambo hili muhimu kwa taifa kwa kuchangia chochote wanachoweza au kudhamini Kongamano ili kusaidia jitihada zetu hizi za kumsaidia Rais wetu mpendwa, Mama Samia Suluhu Hassan, katika kuijenga Tanzania ambayo kila mmoja wetu anaitamani.

"Kwa wale watakaokuwa na nia ya kushirikiana nasi katika tukio hili, wanaweza kutuma michango yao kupitia akaunti yetu ya Tanzania Marriage and Child Care Foundation, namba A/C No. 015C532737600 CRDB, Tawi La Mlimani City," anasema.

Baada ya kongamano hilo la Dar es Salaam, anasema wanatarajiwa kuandaa matukio mengine kama hayo katika mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara na Visiwani kwa lengo la kuhakikisha migogoro ya ndoa, kuvunjika kwa ndoa na ukatili wa jinsia vinapungua kama si kutoweka kabisa ili kuwa na ndoa imara kwa ustawi wa familia na maendeleo ya taifa.

# TBL inavyowatajirisha wakulima Tanzania kupitia kilimo mkataba

Na Joseph Mwendapole

KILIMO cha mkataba kimeelezwa kuwa ndiyo njia pekee inayoweza kumwondoa mkulima kwenye umaskini kwani anakuwa na uhakika wa masoko ya mazao yake.

Kwa miaka mingi wakulima wamekuwa wakilima lakini maisha yao yakiendelea kuwa duni kutokana na kukosa masoko ya mazao yao na pale wanapopata wamekuwa wakinyonywa bei.

Katika miaka ya karibuni Kampuni ya Bia ya TBL, ilianzisha kilimo cha mkataba kwenye baadhi ya mazao kama shayiri, zabibu na ngano kwa wakulima wa mikoa mbalimbali.

Chini ya kilimo cha aina hii, wakulima wanajengewa uwezo wa kufahamu namna ya kulima kisasa, wanawezeshwa kwa pembejeo na wakati mwingine urahisi wa kupata mikopo.

Kwenye kilimo cha namna hii wakulima wanaingia mkataba na TBL kwaajili ya kununua mazao yao yote pindi yanapokuwa tayari kwa mavuno.

Wiki iliyopita, kulikuwa na tukio la kupokea ripoti ya tathmini iliyofanywa na kampuni ya Redefine Afrika kuhusu namna jamii inavyonufaika na kilimo cha mkataba.



Naibu Waziri wa Kilimo, Antony Mavunde, akizindua ripoti iliyotathmini faida ya kilimo cha mkataba siku ya Alhamisi jijini Dar es Salaam. Kulia ni Mkurugenzi Mkuu wa Tanzania Breweries Limited (TBL), Jose Ramirez **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

Dhumuni la tathmini hiyo ilikuwa kutathmini athari za mpango huo kwa wakulima wadogo, athari zake pana za kiuchumi na kijamii, na kubaini maeneo ya uboreshaji unaowezekana.

Naibu Waziri wa Kilimo, Antony Mavunde,ambaye alikuwa mgeni rasmi kwenye upokeaji wa ripoti hiyo alisema serikali ingependa kuona wadau mbalimbali wanaiga kilimo cha mkataba unaofanywa na Kampuni ya TBL, kwani unawapa wakulima uhakika wa masoko na kuwaondoa kwenye umaskini.

Kampuni hiyo ndiyo imekuwa na mfumo wa kilimo cha mkataba na wakulima wa shairi, mtama na zabibu kwenye mikoa mbalimbali na kasha kununua mazao hayo yenyewe.

"Tumeona namma TBL inavyowajenga uwezo wakulima na kubadilisha maisha yao na sisi wizara tunataka kuona wakulima wanapata masoko kwa hiyo mfumo wa mkataba sisi ndiyo tunaoutaka ili wakulima waweze kuwa na uhakika wa masoko," anasema Mavunde.

"Huu mfumo tunauunga mkono na tunataka kampuni zingine zinazotaka malighafi ziige kwasababu mfumo unampa uhakika mkulima. Wamesaidiwa kupata ujuzi na kujengewa uwezo wa kufahamu aina za mbegu na mbolea na wamepata fursa ya kupata mikopo," anasema

Anasema serikali inamkakati kabambe wa kujengea uwezo wakala wa uzalishaji wa mbegu Tanzania na kushirikisha sekta binafsi katika kuzalisha mbegu za aina mbalimbali.

Anasema serikali itaweka maeneo mengi ambayo yatatumika kwa kilimo cha umwagiliaji ili iwe rahisi kuzalisha mbegu na kutatua changamoto hiyo kwa kipindo chote cha mwaka bila kutegeema msimu wa mvua.

Moloimet Sane ni mnufaika wa kilimo cha mkataba kutoka Kata ya Monduli Juu mkoani Arusha ambaye amelima shayiri kwa zaidi ya miaka 20.

Anasema shayiri ni zao lenye bei kubwa na ukishavuna unapeleka TBL na baada ya wiki moja tu unalipwa hela ambayo inakidhi kusomesha watoto na kuandaa shamba kwa msimu unaokuja.

"Kilimo cha mkataba kimetuinua sana kwasababu hakuna zao lenye bei kama shayiri na soko ni la uhakika tofauti na mazao mengine ambapo unahangaika kutafuta masoko," anasema

Teteyo Laizer naye ni mmoja wa wanufaika wa kilimo cha mkataba anasema kimemsaidia kupata maendeleo makubwa ikiwemo kusomesha watoto wake na kujenga nyumba ya uhakika.

"Uzuri wa kilimo cha mkataba ni kwamba unapata soko la uhakika kutoka TBL, nimelima kilimo hiki kwa miaka zaidi ya 10. Ninalima ekari 10 na manufaa makubwa nimeyaona tofauti na ningelima kilimo cha kawaida," anasema Teteyo.

Mkurugenzi wa TBL, Jose Ramirez, alisema Kupitia mradi wa kilimo bora, TBL ni mhamasishaji mkubwa wa mnyororo wa thamani kwenye kilimo na kuhakikisha kwamba unamfaidisha mkulima kwenye mazao yake makuu ya mtama, shayiri na zabibu.

"Mradi wa kilimo bora una lengo la kufikia asilimia 100 kwenye ujuzi, muunganiko na uwezeshaji wa kifedha miongoni mwa wazalishaji wa TBL kufikia mwaka 2025," anasema.

Anasema TBL ilianza kutoa zabuni kwa wakulima mwaka 2019 na imefanikiwa kuwashirikisha wakulima 4,524 kutoka Dodoma, Arusha na Manyara huku wakishirikiana na taasisi za utafiti, bima na fedha pamoja na asasi za kiserikali.

Anasema ushirikiano huo umesababisha uzalishaji wa tani 15,233 kutoka kwa wakulima na kwamba kilimo bora kinawasaidia wakulima, lakini pia kinasaidia kufikia malengo makubwa zaidi endelevu.

"Kwa mfano, kinasaidia katika kufanikisha malengo endelevu ya kimaendeleo katika Umoja wa Mataifa ya kutokomeza njaa, kuwezesha upatikanaji wa chakula na lishe bora na kuboresha kilimo na kuhakikisha matumizi endelevu na mifumo ya uzalishaji," anasema.

Anasema kilimo hicho kinasaidia kupambana na mabadiliko ya tabia nchi na athari zake na kuboresha ushirikiano ili kufikia malengo ya dunia na kwamba utafiti, ufahamu, teknolojia na ufadhili wa kifedha ndio funguo za kubadilisha kilimo kwa kiwango kikubwa.

Anaeleza TBL imezingatia hayo ili kuleta maendeleo endelevu ya kilimo na mchango wa wakulima wa Tanzania kupitia mavuno bora, ufanisi wa rasilimali, afya ya mchanga na mapato ya wakulima wadogo.

Anasema mradi wa uchambuzi wa mnyororo wa thamani kwenye kilimo bora unazingatia kuonyesha na kuwasilisha matokeo ya athari za kijamii na kiuchumi katika minyororo ya thamani ya kilimo.

"Ninajiamini kusema kwamba tathmini ya uingiliaji huru inaonyesha kuwa mradi wa kilimo bora wa TBL unafanya vizuri na kulingana na matokeo haya, ripoti inaonyesha kwamba asilimia 62 ya wakulima wamepata ujuzi wa kuongeza aina ya mazao yanayozalishwa na kuboresha mavuno," anasema

Anasisitiza bado kuna fursa nyingi za kuboresha mafunzo ya protokali za uangalizi wa mazao na asilimia 36 ya wakulima wameunganishwa huku matokeo yakiwa bora zaidi kwa wakulima wa zabibu.

Anataja changamoto inayoonekana kwenye kilimo hicho kuwa ni za kimtandao, upatikanaji mdogo wa simu janja na ufikiaji wa intaneti na fursa kubwa ya kuwaunganisha wakulima lakini pia kuhakikisha wanapata jumbe hata kama ni kwa njia ya SMS," anasema.

Anasema Mei mwaka huu walizindua mfumo wa malipo ya teknolojia ya blockchain kwa wakulima ambao umeongeza uzalishaji kwa wakulima na asilimia 85 ya wakulima waliowezeshwa kifedha kwa angalau huduma/bidhaa moja ya kifedha.

Aidha, anasema kimsingi, kwetu, ripoti pia inabaini maeneo ya uboreshaji wa mpango huo na hasa mapungufu yanayoonyesha kwamba asilimia 26 tu ya wakulima ni wa kike.

"Hili pengo kubwa hata hivyo, linatoa fursa ya kuboresha mipango yetu ya kilimo ili kuvutia jinsia katika kilimo, haswa kilimo cha zabibu ambacho kimeangukia katika kilimo cha maua. Tumejitolea kwa mafanikio ya muda mrefu ya wakulima wetu, na kwa hivyo kuendelea kuboresha njia tulizo nazo za kuwaunganga mkono," anasema.

Anaeleza wajibu wa TBL hauishii tu kwenye mnyororo wa thamani ya kilimo na kwamba TBL inajali maendeleo endelevu ya kijamii na mazingira, ikilenga katika kuleta tofauti kwa mazingira na maisha ya watanzania.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Vituko vya chandimu zamani

- Mwenye mpira hachezewi rafu, akiitwa umeisha
- Bonge kipa, giza likiingia rafu

Na Adam Fungamwango

WIKI hii wadau na wasomaji wa safu hii walitaka tueleze jinsi watoto wa miaka ya 1990 kurudi nyuma walivyokuwa wakicheza michezo yao, hasa mpira wa miguu.

Mada hii niliiweka kwenye mtandao wa kijamii na wengi walichangia na kufurahishwa na kile ambacho walichokuwa wakikumbushana miaka hiyo walipokuwa watoto.

Kikubwa ni vituko vyao wanapokwenda kucheza soka na wanapocheza pia. Kulikuwa na kitu kama sheria au kanuni ambazo hazikuwa rasmi, lakini zilikuwa zikitumia kwa watoto wote waliokuwa wakicheza soka Tanzania nzima.

Na wala haukuwa utaratibu, bali vitu vilikuwa vikifanyika vyenyewe tu, na baadaye kuonekana kama utaratibu au kanuni.

Kwanza kabisa miaka hiyo, watoto soka walicheza mashuleni na wakirudi nyumbani mitaani. Sasa huko mitaani ndiko vituko vinapoanza.

Kwanza kabisa picha linaanza, wakati wa likizo, watoto wanaokaa eneo moja kujikusanya na mpira wao na kuanza safari ya kwenda kusipojulikana ili kutafuta mechi.

Watatembea kwa miguu tangu asubuhi mpaka mchana jua kali ili mradi tu kutafuta watoto wenzao sehemu yoyote ili waombe mechi.

Wakikuta sehemu kuna watoto wenzao ambao nao wametoka sehemu nyingine kwenda kuomba mechi, watapitiliza kwenda sehemu nyingine.

Lakini, kila wanapopita wakikuta wenzao wanacheza mechi na hakuna sehemu ambayo wanawakuta wako peke yao, basi wataomba timu itakayofungwa bao moja au mawili ipumzike na wao waingie.

Na kama wakikuta wenzao hawana mechi, wataomba na kitapigwa hata kama ni saa sita mchana. Huo mpira utachezwa hadi jioni. Na mara nyingi huwa hakuna refa. Magoli huwa ni ya kandambili, mawe au mashati ya wachezaji waliovua.

Kwenye mechi hizo, mara nyingi watoto wanapochoka kucheza hakuna filimbi yoyote inayopigwa kuonyesha mechi imemalizika, badala yake rafu zinaanza. Ukiona rafu zimeanza, bila ya mtu yoyote kutangaza kuwa uchezwe mpira wa aina hiyo, basi ujue tayari wachezaji wameshaanza kuchoka. Na mara nyingi huchezwa giza linapoanza kuingia au wachezaji kuchoka kucheza.

Hii iliitwa 'fungulia mbwa', 'orlando', au 'Uruguay' au Bundesliga. Kwanza kabisa hali ikizidi wale wachezaji wanyonge wanaanza kujiengua wenyewe na kubaki wababe. Nao hali ikiendelea basi unazuka ugomvi, mzozo au ngumi ambazo huwa ndizo zinahitimisha mechi yenyewe.



**MWENYE MPIRA NDIYO KILA KITU**

Kwenye mechi hizo za watoto zamani mmiliki wa mpira ndiyo huwa kila kitu, na mipira yenyewe ni ile ya makatarasi, nailoni na nyuzi.

Ni wachache sana waliokuwa na mpira hiyo. Sasa mwenye mpira huwa kama mfalme kwa sababu ni lazima abembelezwe ili watoto waweze kucheza. Akikasirika na kuchukua mpira wake, mechi au mazoezi hapo hakuna.

Kwanza kabisa hata kama hajui kucheza mpira ni lazima apate namba, na anacheza kwenye nafasi ambayo ataamua yeye mwenyewe na siyo wenzake. Pili huwa hawachezi rafu. Wote wanaogopa kumchezea kwa sababu wanajua hilo likifanyika mpira umeishia hapo.

Mwenye mpira anaweza 'kukontroo' wachezaji wa timu zote mbili, hata kama yupo upande mmoja. Anaweza kuamua hata upande mwingine ambao hachezi, nani acheze na nani asicheze. Akiona kuna mtoto anajua zaidi anaweza akakataa asiendelee kucheza, au asiingie.

Kwenye mazoezi, yeye ndiye anayechagua kikosi chake, na atachagua wenye uwezo, wale ambao wenzangu na mimi atakwenda kwenye kikosi kingine atakachocheza nacho.

Anaweza pia kukataa goli ambalo timu yake imefungwa na wote msifanye kitu chochote, mkakubali tu.

Akiitwa kwao mjue na mpira wenyewe umeisha, na kama kuna kazi kwao, basi watoto wenzake watamsaidia ili amalize upesi waende kucheza.

**MWENYE NDALA AKIONDOKA, MAGOLI HAKUNA**

Kwa sababu ndala ndiyo yalikuwa magoli, mwenyewe akiondoka anachukua ndala zake, hivyo mnabaki kucheza bila magoli, upande mmoja, sasa hapo yanawezwa kutafutwa mawe, au mashati ya wachezaji waliovua.

Katika mpira huo mara nyingi kila mtu anavaa nguo yake, hakuna jezi maalum, na wapo wanaocheza pekupeku, wapo wanaocheza na viatu, ingawa nao ni wale tu ambao wataruhusiwa na mwenye mpira.

Wachezaji wanajuana kwa sura tu, huyu ni ndugu yangu, kila mtu na nguo yake, wengine anacheza na suruali, wengine kaptura, labda tu itokee wawepo watoto wenye akili ya kukumbuka kuwa upande mmoja uvue mashati na mwingine uvae, na hayo mashati wakati mwingine wanatumika kama magoli.

Kituko kikubwa ni kile ambacho kipa anaweza kupunguza ukubwa wa goli pale anapoona anashambuliwa. Ni kazi rahisi tu anachomoa ndala kutoka alipoichomeka kwenye mchanga, au kuiweka kwenye nyasi na kuirudisha ndani kidogo ili kumpunguzia uwezo mfungaji wa kupachika bao.



**MPIRA UKIPIGWA NYUMBA JIRANI HAURUDI**

Wakati mwingine zamani hakukuwa na uwanja maalum kwa watoto kucheza, hivyo walicheza karibuni na nyumba na njia pia.

Wakati watoto wanapocheza akipita mtu mzima wanasimamisha mpaka apite. Wakati huo watoto waliona kama watu hao wanafanya makusudi, kwani walionekana hawapiti upesi, wanapita kwa kujivuta mno, au wanafanya hivyo kwa lengo la kuuchukua mpira na kuondoka nao.

Ikitokea bahati mbaya mkubwa akapigwa, anaweza kuuchukua mpira wa kuondoka nao. Watoto nao wanaweza kumfuata nyuma nyuma na kumpora, au wasifanikiwe kabisa.

Kuna mashuti yaliokuwa yakipigwa na wachezaji yanakwenda kuangukia kwenye nyumba jirani na uwanja. Kuna baadhi ya nyumba walikuwa hawarudishi mpira kwa sababu zao binafsi, lakini zipo nyumba ambazo zinaonekana kama wenye nyumba hizo ni wanamichezo au wanajua umuhimu, kwani wanaurudisha mpira watoto na kuendelea kucheza.

**BONGE LAZIMA AWE KIPA**

Zifuatazo ni baadhi ya meseji ya wadau ambao wamezimimina kuhusiana na mada hii.

"Unatakiwa kucheza pekupeku, mwenye mpira hakai benchi, pia magoli ya ndala au mawe." Hiyo ni meseji wa mmoja wa mtoto wa zamani aliyecheza soka miaka hiyo, mwingine naye akaandika.

"Penalti hakuna kupiga dochi, mpira hauna refa, hauna mwisho hadi giza, mwenye mpira ndio aamue ucheze au usicheze, vibonge ndio makipa na hauna kuotea."

"Faulo ya kushika mpira kwa mkono tu, hakuna ya rafu, wakati mwingine mechi haina penalti, watu, watu wafupi ndiyo mawinga, magoli ya mawe au ndala za kipa," huyu ni mchangiaji mwingine.

Mdau mwingine yeye alichangia maneno yafuatayo.

"Kibonge ndiyo golikipa, mwenye ndala akiitwa na magoli yameondoka, kama kiwango chako kidogo mtu anaejua kucheza akija unatolewa."

**Tuma meseji 0716 350534**

HABARI KIMATAIFA

# Rais Putin asaini nyaraka kunyakua rasmi mikoa minne ya Ukraine

**MOSCOW, Russia**

RAIS Vladimir Putin amesaini nyaraka za kuingiza majimbo manne ya Ukraine kuwa katika miliki ya Russia.

Utiaji saini katika nyaraka hizo, ulifanyika baada ya kumaliza hotuba yake na viongozi walioteuliwa wa maeneo yaliyonyakuliwa.

Zoezi la uwekaji saini nyaraka hizo ulifanyika akiwa amekaa mita kadhaa mbali kwenye meza, huku wasaidizi wakizipeleka na kuzirejesha kwa Putin kwa ajili ya kusainiwa baada ya kusaniwa na maofisa wengine.

Wakati wa hafla hiyo, watu waliohudhuria walipiga makofi na kushangilia huku kila mwakilishi wa mkoa mpya anapotambulishwa.

Rais Putin katika hutuba yake, alisema watu wa mikoa minne ya Ukraine ambayo amenyakua wamefanya uamuzi na matokeo yanafahamika vizuri.

"Watu wamefanya chaguo lao, ni chaguo pekee kutoka kura za maoni," alisema Putin.

"Nina uhakika kwamba bunge la shirikisho litaunga mkono mikoa mipya minne ya Russia, maeneo mapya manne ya shirikisho letu kwasababu huu ni utashi wa mamilioni ya watu," aliongeza kusema.

Putin alirejea kudai kwamba katika historia vizazi vingi vimepigana kwa ajili ya ardhi hizo.

Maeneo ya Ukraine yanayonyakuliwa na Russia ni Donetsk, Luhansk, Kherson na Zaporizhzhia.

Hata hivyo, mataifa ya Ulaya na Marekani yamelaani unyakuzi huo na kueleza hawatambui.

Awali, maofisa wa Russia, akiwemo Waziri wa Mambo ya Nje Sergei Lavrov, wamebainisha tishio la matumizi ya silaha za nyuklia ili kuyalinda maeneo wanayopanga kuyanyakua huku Ukraine ikiapa kuwa itayakomboa maeneo yake yote.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Antonio Guterres ameitaja hatua hiyo kuwa ni hatari na ukiukaji wa mkataba wa Umoja wa Mataifa.

" Ili kuwa wazi, Russia ni moja ya wanachama watano wa kudumu wa Baraza la Usalama na inashiriki jukumu maalum la kuheshimu mkataba wa Umoja wa Mataifa. Uamuzi wowote wa kuendelea na unyakuzi wa mikoa ya Donetsk, Luhansk, Kherson na Zaporizhzhia ya Ukraine hautakuwa na thamani yoyote kisheria na unastahili kulaaniwa," alisema.

Aliongeza "Mpango huo unakinzana na mfumo wa sheria za kimataifa. Unakinzana na yale yote ambayo jumuiya ya kimataifa inatakiwa kuyatetea. Unakinzana na madhumuni na kanuni za Umoja wa Mataifa. Ni matokeo ya hatari. Uamuzi huo hauna nafasi katika ulimwengu wa kisasa na haupaswi kukubaliwa."

Wakati hayo yakiripotiwa,Ukraine na Russia zimeshutumiana jana kuhusika na mashambulizi huko Zaporizhzhia na kusababisha vifo vya watu takriban 23.

Msafara huo uliokuwa umebeba raia na vifaa ulishambuliwa karibu na mji wa kusini mwa Ukraine unaokaliwa na vikosi vya Urusi wa Zaporizhzhia.


Gavana wa Mkoa wa Zaporizhzhia Oleksandr Starukh alisema shambulio hilo limeendeshwa na majeshi ya Russia na hivyo kusababisho vifo vya watu 28, ambao wote ni wakazi wa eneo hilo.

Naye Vladimir Rogov, Ofisa anayeiunga mkono Russia alilaumu Ukraine kwa uchochezi na kukanusha kuwa jeshi lao halikuhusika na shambulio hilo.

Eneo la kiwanda cha Zaporizhzhia, lililokuwa na wakazi 700,000 kabla ya vita, liko chini ya udhibiti wa Ukraine lakini limekuwa likikabiliwa na mashambulizi kutoka Russia.

Aidha, shirika la habari la serikali ya Russia limebaini kuwa ofisa aliyeteuliwa na serikali yake huko Kherson, eneo la kusini mwa Ukraine ameuawa katika mashambulizi ya vikosi vya Ukraine.

*DW.*



Rais Vladimir Putin akizungumza kabla ya kutia saini nyaraka za kujumuisha maeneo manne ya Ukraine katika nchi ya Russia. **PICHA: REUTERS**

# Jaribio la mapinduzi laendelea Burkina Faso

**OUAGADOUGOU, Burkina Faso**

MILIO ya risasi imekuwa ikiendelea kusikika karibu na Ikulu ya rais wa Burkina Faso katika kile kinachoaminika kuwepo na jaribio la mapinduzi.

Kasri la rais liko barabara za kelekea kwenye majengo muhimu, ikiwa pamoja na bunge la taifa, kituo cha utangazaji cha taifa na makazi ya Waziri mkuu ambayo yamefungwa.

Mwezi Januari kulitokea mapinduzi baada ya kiongozi wa sasa Luteni Paul-Henri Damiba, kumng'oa Rais Roch Kabore kwa njia ya mapinduzi.

Rais aliyechaguliwa kidemokrasia aliondolewa madarakani kwa kushindwa kudhibiti ghasia za wanamgambo wa Kiislamu.

Sasa Luteni Kanali Damiba anaonekana kukabiliwa na hatma sawa na hiyo.

Alhamisi mamia ya waandamanaji waliingia mitaani katika mji wa Bobo Dioulasso kudai ajiuzulu, wakimlaumu kwa hali ya ukosefu wa usalama nchini humo.

Walioshuhudia wanaripoti kuhusu uwepo mkubwa wa wanajeshi katika mji mkuu.

Shule zimefungwa na wakazi wa mji huo wako majumbani, wakisubiri taarifa kuhusu matukio yanayoendelea nchini humo.

Tangu mwaka 2015, mamlaka nchini Burkina Faso zimekuwa zikihangaika kudhibiti mashambulio ya makundi ya uasi.

Jumatatu ya wiki hii wanajeshi 11 waliuawa katika shambulio la wanamgambo katika jimbo la kaskazini mwa nchi la Soum province, raia 50 waliripotiwa kuwa hawajulikani waliko.

*BBC*

## Rais Biden aongeza ufadhili Pasifiki

**WASHINGTON, Marekani**

RAIS Joe Biden wa Marekani, ameahidi kitita cha dola milioni 810, ambazo ni ufadhili mpya kwenye visiwa vya Pasifiki.

Ahadi hiyo aliitoa jana katika mkutano wa kilele wa kwanza na wa viongozi wa visiwa hivyo mjini Washington. Biden aliapa kuimarisha ushirikiano na eneo la kimkakati lakini lenye watu wachache ambalo China inaweka ushawishi.

Akizungumza na viongozi wa mataifa ya Kusini ya Pasifiki, Biden alisema anataka kuonyesha dhamira ya dhati, akisema usalama wa Marekani unategemea sana usalama wa mataifa hayo.

Marekani imekuwa mshirika mkuu wa eneo hilo tangu iliposhinda Vita vya Pili vya Dunia.

Wakati Marekani ikionekana kutolitilia maanani eneo hilo, China imejiingiza kwa nguvu kupitia uwekezaji, mafunzo ya polisi na makubaliano tata ya usalama na Visiwa vya Solomon.

**DW**

## Uchumi wa Uingereza wakua

**LONDON, Uingereza**

UCHUMI wa Uingereza umeripotiwa kukua katika robo ya pili ya mwaka badala ya kudhoofika kama ilivyotarajiwa awali.

Taarifa hizi zilizochapishwa jana zimepunguza wasiwasi katikati ya mtikisiko uliopo kuhusu bajeti ya serikali inayolenga kupunguza kodi.

Pato la ndani la taifa liliongezeka kwa asilimia 0.2 katika kipindi cha miezi mitatu hadi mwishoni mwa mwezi Juni kutoka 0.1.

Kulingana na ofisi ya kitaifa, Uingereza haipo kwenye mdororo wa uchumi tofauti na makisio ya awali ya Benki Kuu ya Uingereza na zinazotolewa siku mbili baada ya Benki hiyo kuyageukia masoko ya hati fungani ili kuzuia hatari ya mitikisiko wa kifedha.

Bajeli iliyotangazwa na Waziri Mkuu Liz Truss iliibua wasiwasi wa hali ya kifedha ya Taifa hilo.

**DW**

**Pato la ndani la taifa liliongezeka kwa asilimia 0.2 katika kipindi cha miezi mitatu...**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GEOFFREY EDWARD MBANGA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.753 BDX.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU. TAARIFA YA POLISI **MBE/MBE/RB/387571/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GEOFREY JUSTO KITILYA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **LEXUS** yenye usajili namba **T260BMH,** CHASSIS NAMBA: **JT6HJ88JIV0182933** na ENGINE NAMBA **5B22456728.** . Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **DAR/OST/RB/388448/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HELLEN E NGALA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba **T154 AFG.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **ARU/ARU/RB/365555/2022**

## MWAMBA AUCTION MART AND RECOVERIES

### TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa Amri ya Mahakama ya Mwanzo Dodoma Mjini nitauza NYUMBA **Plot no. 44, Block CC (SQM 646) Chinyika Mkonze,** na kiwanja 796450,9314639 796455,9314613 796471,9314616 796465,9314649 Michese Dodoma Chumo la ndoa ya **EULELIA AMANDI TARIMO na JOSEPH PROSPER MOSHI** kutokana na shauri la Madai ya ndoa namba 88 ya mwaka 2021 Muda wa mnada ni saa 4:00 Asubuhi.

| SN | MALI INAYOUZWA | USAJILI WA MALI | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1. | KIWANJA KIMOJA | 796450,9314639, 796455,9314613 796471,9314616 796465,9314649 | 05/10/2022 |
| 2. | NYUMBA MOJA | Plot No. 44, Block CC Mkonze | 17/10/2022 |

**MASHARTI YA MNADA**
- Mnada utafanyika mahali nyumba ilipo/kiwanja kilipo
- Gharama za kubadili hati ya umiliki ni juu ya mnunuzi

Ukihitaji kuuona mtambo huo kabla ya siku ya mnada, piga **0715 170 553**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**

**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI2)**

**Katika mahakama ya mwanzo PONGWE**

**Usimamizi wa mirathi 52/2022**

**Ombi la BRIGTHA EVELYNE MBAPU kuteuliwa Msimamizi mirathi ya marehemu GEORGE AGREY MBAPU**
**Kwa YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja kuhudhuria kesi mnamo tarehe 7/10/2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 13.09.2022

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
PONGWE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA(W) LA MWANZA**

**MAOMBI Na 171 YA MWAKA 2022**

**NELSON ESKARI LEMA..........................................MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

1. **JOSEPHAT KAMUGISHA..............................MJIBU MAOMBI**
2. **KABULA NGAKAMA@LIGHTNESS MUNISI.............MJIBU MAOMBI**

**WITO WA KUITWA BARAZANI**

**KWA**
**1.JOSEPHAT KAMUGISHA**
**2. KABULA NGAKAMA@LIGHTNESS MUNISI.**

Mnafahamishwa kwamba mleta maombi hapo juu amefungua shauri/ ombi dhidi yenu katika baraza la Ardhi na nyumba mkoa wa mwanza, ombi hili limepangwa kutajwa tarehe 19/10/2022 katika chumba na. 1 cha baraza, barabara ya Airport jengo liko mkabala na mahakama ya mwanzo mwanza mjini- Tanzania.
Kwa hiyo mnatakaiwa kuhudhuria katika baraza siku hiyo wewe mwenyewe, wakili wako au mtu mwingine anaye ruhusiwa kisheria kujibu ombi/ shauri hilo linalo kukabili.
**KAA-** ukijua kwamba kushindwa kufika kwako siku hiyo, baraza litasikiliza ombi hilo na kutoa uamuzi bila wewe kuwepo
Imetolewa nami kwa Amri na lakiri/ mhuri wa Baraza leo Tarehe 20/09/2022.

**Mayeye S.M**
**Mwenyekiti**
**Baraza la Ardhi na Nyumba (w) Mwanza.**

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**website: www.ippmedia.com**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MGENI wa ajabu anatokea kwenye kijiji cha Semwanza, Lugoba mkoani Pwani. Anakotoka hakujulikani. Watu wote wanamwogopa. Ni kwa sababu hawamjui. Msichana Siwatu anajitolea kumsaidia mgeni huyo. Kwa kufanya hivyo, anabezwa kwa maneno mengi ya kejeli kwa kumsaidia mtu asiyemjua ambaye anaweza kuwa hatari kwa kijiji. Baadhi ya viongozi wa kijiji waliungana na wanakijiji kutaka wamtimue mgeni huyo asiyejulikana, lakini akakataa katakata. Pamoja na kutishwa kuwa atatengwa na kijiji, bado msichana huyo alisimama na msimamo wake ule ule wa kumsaidia kwa sababu alikuwa na shida kubwa. Matokeo ya haya, yanamuingiza Siwatu kwenye msukosuko mkubwa ambao hajawahi kuupata kwenye maisha yake kiasi cha kumkatisha tamaa. Fuatilia kisa hiki.

# KAMA IPO, IPO TU-25

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Ilikuwa jioni saa 12:00, kwa mtoto wa kike porini na kitu kama kile kuwa na biandamu ambaye ni nusu mfu ilikuwa ni kitu cha kutisha kweli kweli. Hakutishika. Pamoja kwamba alijua siwezi kuamka pia nakaribia kifo, akaniambia kwa sauti kuwa anakwenda kijijini kuita watu. Saa moja baadaye ilikuwa tayari giza limeingia hivi alirudi yeye mwenyewe akiwa ameambatana na huyu kaka yake Dibwela na kijana mwingine."

"Kobelo huyo." Akadakia Dibwela.

"Ewaa bwana shemeji. Ndiyo nikaletwa kijijini. Sikutaka kujitambulisha jinsi nilivyo, nikajitambulisha kama Bakari. Nikaishi hapa kama raia wa kawaida tu. Raha na karaha za kijiji zikanipata. Baadhi ya wanakijiji pamoja na uongozi ulionekana kupinga sana mimi kukaa hapa. Ikasababisha hata kutengwa. Maneno yakawa mengi na ya kukatisha tamaa kwangu na Siwatu. Mtoto wa watu hakukata tamaa. Aliendelea kuwa mwanamke shujaa. Shupavu. Hata kama wote wakimkataa alisimama na mimi. Na mpaka wakati huo tayari watu wote walidhani mimi na Siwatu ni wapenzi kwa sababu tulilala chini ya paa moja. Ni kweli tumelipenda, lakini hakuna hata mmoja aliyewahi kumtamkia mwenzake hilo. Lakini kila kitu kilichobakia kilionyesha kuwa tunapendana. Tunavyotazamana. Tunavyotembea kwenda sehemu mbalimbali. Tunavyoongea, tulionyesha tunapendana na kila mmoja alimuhitaji mwenzake, lakini hakuna aliyemwambia mwenzake. Hata hivyo ilibidi lazima nirejee nyumbani nikamuone mama yangu na dada zangu, nikaone biashara zangu tangu nilivyoziacha. Wakati huo nilipoteza mawasiliano wa ndugu, jamaa na marafiki kwa miezi yote hiyo wakadhani nimefariki. Habari ikaenea kuwa nimeuawa na kutupwa porini, lakini hakuna aliyejua ni wapi. Hilo nililifahamu niliporejea nyumbani. Huku nilimuaga Siwatu. Tukaagana porini siku aliponisindikiza. Tulilia machozi, ilikuwa karibu na kule alikoniokota. Nilimuahidi nitarejea baada ya mwezi mmoja." Akaendelea kuongea kwa hisia, kiasi cha machozi kumlengalenga.




**"Usilie Siwatu, hatimaye mizimu ya baba na mama yako imekuona."**

"Nilirejea nyumbani Dar es Salam na kukutana na mama na dada zangu ambao hawakuamini kama niko hai. Waliniuliza siku zote niliwaficha, lakini kuna siku maalum ambayo nilikaa nao na kuwaeleza jinsi ilivyokuwa, nilivyotekwa, hadi nilivyookolewa na Siwatu mpaka kuondoka. Kusema kweli na wao walitokea kupenda kujua habari za binti wa aina hiyo na kutaka kumuona. Nikawaambia hata mimi nimempenda, lakini sijawahi kumwambia neno hilo. Lakini nikawaambia nitarudi Semwanza Lugoba kwa ajili yake. Mama akaniambia fanya haraka kwa sababu naweza kumkuta amechumbiwa au ameolewa na mtu mwingine. Ni kweli, ni kwa sababu sikuwahi kumwambia nakupenda au nitarudi tena kukuoa, lakini akili yangu nyingine ikawa inaniambia Siwatu hawezi kukubali kuolewa mpaka mimi nirudi."

"Mhh, mwanaume wewe umenishinda tabia, yaani kumbe ulikuwa unanicheza shere, pesha imenipanda mimi mtoto wa watu najua hapa kuna wanaume wawili, kumbe ni wewe tu mmoja, haya ulijigawa vipi, ukaja hapa na hawa wakaja kuleta barua, mkawa mnapishana hapa kama paka na panya?" Akauliza Siwatu ambaye kwa sasa alikuwa ametulia tuli amemshikilia Sam, au Bakari wake kwa maringo baada ya dalili zote sasa kuonekana kuwa ndiye mumewe pekee mtarajiwa na wala hakukuwa na mwingine kama alivyofikiri.

"Nilichotaka hapa ni mambo mengi tu. Kwanza sapraizi, halafu nijue kama kweli mtu huyu ananipenda kwa dhati, achilia mbali tulivyokuwa tukaishi kule, lakini je yuko tayari kuolewa nami? Nikawachukua hawa wafanyakazi wangu, Billy na Daudi, nilianza kuja nao hadi barabarani pale nikawapa ramani yote, halafu nikawaachia kazi. Walirudi na kuniambia barua imekubaliwa. Nilishtuka kidogo, lakini wakaniambia habari ya Siwatu kuwa ameshakataa waanaume wengi sana, lakini ameikubali hii kwa sababu amekaa sana na amepatwa na matatizo ya kubakwa, na ameshachoka kukaa kwenye kijiji, hivyo ameamua kuondoka, na ni kukubali kuolewa. Hiyo ilinipa nguvu kuwa kumbe alikuwa ananisubiri, ila amechoka baada ya kutokea matatizo. baadaye mimi mwenyewe nikaja sasa hapa kama Bakari. Nikamtamkia kuwa nataka kumuoa, wakati najua kuwa barua imekuja na ni yangu. Ilikuchanganya sana bibie, niliona hali uliokuwa nayo, mpaka ukaniambia tutoroke. Hapo nikajua kabisa kuwa unanipenda, na uko tayari kuachana na barua ya mtu ambaye humfahamu. Kwa hili nasema ni kweli nimepata mke wa kweli. Kingine ambacho kabla sijamaliza sikutaka kukisahau ni kwamba nimewasiliana na polisi wa kituo cha Chalinze waje kufanya uchunguzi wa kubakwa kwako. Niliposikia tu hili jambo nilipokuja hapa, niliwasiliana nao, na wiki hii yote walikuwa kwenye uchunguzi, muda si mrefu wataniambia wamefikia wapi. Sasa nathibitisha rasmi kuwa ile barua mliyopokea ilikuwa yangu, na mimi ndiye mchumba pekee wa Siwatu Nataka uwe mke wangu sasa, mama na dada zangu wanakusubiri Dar. Nataka kukufanya uwe malkia."

Kila mtu alionekana kutokwa na jasho. Ilikuwa ni kama hadithi fulani ya kufikirika, lakini ukweli ndiyo ulibaki kuwa huo.

Sam, kijana wa kitajiri ndiye Bakari. Bakari huyo ndiye yule aliyetupwa porini kijijini na kuokolewa na Siwatu. Siwatu huyo ni yule msichana yatima aliyemsaidia mtu asiyemjua na kutengwa na kijiji. Kumbe aliyemsaidia si Bakari ambaye wao walimfahamu kijiji ni kuwa ni kijana hohe hahe aliyetoka kusikojulikana. Ni kijana aliyerithi mali ya marehemu baba yake na akatekwa kwa kutupwa kwa husuda za wafanyabishara wenzake.

Siwatu alimuacha Sam na kumfuata kaka yake, Dibwela ambaye naye alisimama, akamkumbatia. Siwatu akaanza kulia kwa nguvu.

"Usilie Siwatu, hatimaye mizimu ya baba na mama yako imekuona."

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# GGML WAZINDUA MASHINDANO YA SOKA KWA WATOTO

**Na Mwandishi Wetu, Geita**

KAMPUNI ya uchimbaji madini ya Dhahabu Geita (GGML), imezindua mashindano ya mpira wa miguu kwa watoto wanaozunguka mgodi huo, ili kukabiliana na changamoto ya watoto wanaofanya shughuli za uchimbaji bila ruhusa.

Mashindano hayo ambayo yanayohusisha kata za Mtakuja na Nyankumbu za Geita Mjini, yanalenga kuwapatia elimu watoto, walezi na wazazi wao madhara ya kuwatumikisha watoto wadogo katika shughuli za uchimbaji na kuwanyima fursa za kupata elimu.

Katika mashindano hayo, watoto kutoka mtaa wa Nyamalembo na Compound walimenyana na watoto kutoka mtaa wa Elimu na Nyankumbu.

Aidha, akizungumza katika uzinduzi huo uliofanyika katika uwanja wa General Tyre mjini Geita jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Geita Gold Mining Limited, Terry Strong alisema watoto ni sehemu muhimu katika biashara ya kampuni hiyo.

Alisema GGML, imewekeza kwenye shule, hospitali na maeneo mengine ambayo watu wanaweza kupata huduma... ikiwa ni sehemu ya Wajibu wa Kampuni kuisadia jamii inayozunguka mgodi ambapo kupitia mpango huo, GGML ilijenga zaidi ya madarasa 600 mwaka wa 2018.

"Watoto wadogo ndio kizazi cha baadaye na ndio wa kwanza kunufaika na uwekezaji wetu. Kampuni yetu inafuata kanuni elekezi za Umoja wa Mataifa kuhusu biashara na haki za binadamu na kanuni za hiari za usalama. Kwa hiyo, tumekubali kuwalinda watoto dhidi ya hatari zozote zinazotokana na jinsi tunavyofanya biashara," alisema.

Alisema idadi ya watoto wanaoingia kwenye shughuli za uchimbaji bila ruhusa imekuwa ya kutisha.

Awali, Makamu wa Rais wa AngloGold-GGML anayeshughulikia miradi endelevu kwa Ghana na Tanzania, Simon Shayo alisema moja ya tunu muhimu za kampuni hiyo ni kuhakikisha jamii inayozunguka mgodi huo inanufaika.

Alisema mipango ya kampuni hiyo inalenga kuboresha sekta ya afya, elimu, michezo na utamaduni ili kukuza vipaji vya watoto hao.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Geita Gold Mining Limited, Terry Strong akisalimiana na timu ya soka ya watoto wanaozunguka kampuni hiyo kutoka Kata za Mtakuja na Nyankumbu zilizopo mkoani Geita. GGML jana ilizindua mashindano ya mpira wa miguu kwa watoto hao ili kukabiliana na changamoto ya watoto wanaokwepa kwenda shule na kuingia kwenye eneo la mgodi na kufanya shughuli za uchimbaji bila ruhusa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SPC yakabidhi viwanja kwa washindi Kili Marathon

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Surveyed Plots Company Ltd ya Jijini Dar es Salaam jana imekabidhi rasmi zawadi ya viwanja kwa wanariadha wawili walioshiriki mbio za Kilimanjaro Premium Lager Marathon 2022.

Viwanja hivyo, vilivyopo Kigamboni jijini Dar es Salaam vimekabidhiwa kwa Alloyce Simbu aliyeshinda mbio za kilometa 42 kwa upande wa wanaume na Angelina Yumba aliyekuwa wa tatu katika mbio za kilometa 42 na kuwa Mtanzania wa kwanza wa kike.

Wanariadha hao walikabidhiwa hati rasmi za umiliki wa viwanja hivyo katika hafla maalumu iliyofanyika katika ofisi za SPC Jijini Dar es Salaam jana na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali wa riadha, wakiwamo chama Cha Riadha Tanzania, waandaaji na wadhamini wa Kilimanjaro Premium Lager Marathon.

Akizungumza wakati wa makabidhiano hayo, Meneja Masoko wa SPC, Catherine Michael, alisema wanayo furaha hatimaye kukamilisha utaratibu wa kukabidhi rasmi viwanja hivyo ikiwemo kila mmoja kupokea hati ya umiliki.

"Viwanja hivi viko Kigamboni na kila kimoja kina ukubwa wa mita za mraba 400 na thamani ya Tsh 4,000,000 kama tulivyotangaza wakati wa mbio za Kilimanjaro Premium Lager Marathon kule Moshi mapema mwaka huu," alisema.

Akizungumza baada ya kupokea hati ya umiliki, Simbu alisema zawadi hiyo ni fahari kubwa kwake kwani inampa motisha ya kujiandaa vizuri zaidi kwa mbio za mwakani ili aweze kutetea nafasi yake na kushinda kiwanja kingine.

Naye Angelina Yumba alisema, hakuwahi kuwaza kumiliki kiwanja Kigamboni lakini riadha imempa nafasi hiyo ya kipekee.

Akingumza pia wakati wa hafla hiyo, Rais wa Chama cha Riadha nchini, Silas Isangi, aliwashukuru SPC kwa kutimiza ahadi yao na kuongeza hamasa miongoni mwa wanariadha nchini na kuwaasa washindi kuongeza juhudi katika kutaka mafanikio zaidi.

## Tanzania, India kushirikiana kukuza sekta ya filamu

**Na Romana Mallya**

SERIKALI za Tanzania na India zimekubaliana kuongeza maeneo mapya ya ushirikiano ikiwamo sekta ya filamu, ili kuwaendeleza wasanii Wakitanzania kujifunza zaidi uzalishaji wa filamu bora.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akifungua kongamano la ushirikiano katika sekta ya utamaduni baina ya nchi hizo, lililoandaliwa na ubalozi wa India nchini kwa kushirikiana na vyuo vikuu.

Mulamula alisema, ushirikiano wa nchi hizo ni wa kihistoria na umekua imara nyakati zote, na kwa sasa mataifa hayo yamekusudia kuongeza maeneo zaidi ya ushirikiano hususani sekta ya filamu.

"Tumekubaliana na Balozi kuwa tufufue na kupeleka watu wetu kujifunza na watusaidie kujenga uwezo wetu wa kutengeneza filamu zenye viwango kama za India, ili tufike mahali tuwe tunaangalia filamu zetu, tumeshawekeana makubaliano na Balozi," alisema.

Balozi Mulamula alisema ushirikiano wa Tanzania na India umekuwa imara wakati wote kutokana na misingi ya kihistoria iliyowekwa na waasisi wa mataifa hayo, Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere na Baba wa Taifa la India, Mahatma Gandhi.

## Minziro alia na wachezaji wake

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA mkuu wa timu ya Geita Gold, Fred Filex Minziro amelia na wachezaji wake baada ya kupoteza mchezo wao wa Ligi Kuu walioucheza juzi dhidi ya Dodoma Jiji FC.

Akizuñgumza na gazeti hili jana alisema wachezaji wake walipata nafasi nyingi lakini walishindwa kuzitumia.

"Tulipa nafasi nyingi za wazi na tukashindwa kuzitumia wapinzani wetu wakatumia nafasi hizo kutufunga," alisema Minziro.

Alisema walimiliki kwa kiasi kikubwa mpira lakini bahati haikuwa ya kwao kutokana na makosa yaliyofanywa na wachezaji wake.

Alisema mara Kwa mara amekuwa akiwashauri wachezaji wake kuhakikisha wanapata matokeo kwenye michezo ya ugenini.

"Tatizo la umaliziaji linazidi kuwa sugu ndani ya timu yangu ninazungumza na kuwapa mbinu wachezaji inapofika siku ya mchezo wanafanya tofauti na nilivyowaelekeza,alisema kocha huyo.

## ZISIKUPITE

### HAALAND ATAKIWA MADRID

KLABU ya Real Madrid itajaribu kumsajili beki wa Manchester City na Ureno, Joao Cancelo, 28, msimu ujao wa joto na pia wanapanga kumnunua mshambuliaji wa Norway, Erling Haaland mwenye umri wa miaka 22 mwaka 2024. ***(AS)***

### NEVES AWINDWA BARCA

KIUNGO wa Klabu ya Wolves na Ureno, Ruben Neves mwenye umri wa miaka 25, analengwa na Barcelona kuchukua nafasi ya mchezaji wa kimataifa wa Hispania, Sergio Busquets mwenye umri wa miaka 34. ***(Sport).***

### NEWCASTLE YATAKA NYOTA

KLABU ya Newcastle United imewajumuisha kiungo wa kati wa Leicester City na England, James Maddison mwenye umri wa miaka 25, na mchezaji mwenzake wa kimataifa wa Ubelgiji, Youri Tielemans mwenye umri wa miaka 25, katika malengo yao kwa mwaka 2023. ***(90 min).***

### EPL KUCHEZA NA LALIGA

TIMU inayojumuisha nyota wote Ligi Kuu England inaweza kucheza na timu za ligi pinzani kama vile LaLiga au Bundesliga chini ya mipango inayozingatiwa na wakuu wa vilabu. (Times)

### MARTINEZ KUTORUHUSIWA

KLABU ya Aston Villa haina nia ya kumruhusu mlinda mlango wa Argentina, Emiliano Martinez mwenye umri wa miaka 30 kuondoka Januari huku Manchester United ikiwa miongoni mwa klabu zinazomuwania. ***(Football Insider)***

### GAKPO AWANIWA

KLABU za Manchester United, Southampton na Everton bado zinamuwania mshambuliaji wa PSV Eindhoven na Uholanzi, Cody Gakpo mwenye umri wa miaka 23. ***(Football Transfer)***

### TROSSARD AWINDWA

KLABU ya Brighton inapanga kufanya mazungumzo ya mkataba mpya na mshambuliaji wa Ubelgiji, Leandro Trossard mwenye umri wa miaka 27, na kiungo wa kati wa Argentina, Alexis Mac Allister mwenye miaka 23. ***(Athletic)***

### ADEL AGOMBEWA

KLABU ya Liverpool inafikiria kumnunua winga wa Misri na Pyramids, Ibrahim Adel Januari huku Arsenal, Brentford, Brighton na Nottingham Forest pia zikiwa pia zinamtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21. ***(90 Minutes)***

### CONTE APUUZA

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Antonio Conte mwenye umri wa miaka 53, amepuuzilia mbali tetesi zinazomhusisha na kurejea Juventus kuwa "zisizo na msingi". ***(Evening Standard)***

### ASENSIO AGOMBEWA

KLABU ya Juventus inakabiliwa na ushindani kutoka kwa Arsenal, Liverpool, Tottenham, AC Milan na Barcelona kuwania saini ya mshambuliaji wa Hispania, Marco Asensio baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 kukataa kuongezewa mkataba na Real Madrid. ***(Calciomercato)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# HAALAND KUCHEZA LIGI KUU TANO ULAYA

**Baba yake afichua kwamba, kabla ya kutundika daruga lazima akipige Hispania, Italia na Ufaransa...**

**MANCHESTER, England**

BABA mzazi wa Erling Haaland amefichua kuwa mshambuliaji huyo ana nia ya kujipima katika kila ligi kuu tano za Ulaya, akipendekeza kuwa huenda asidumu kwa muda mrefu sana Manchester City.

Mchezaji huyo raia wa Norway alitakiwa na timu nyingi msimu uliopita, lakini akajiunga na City akitokea Borussia Dortmund, ambako alipachika mabao 86 na kutoa pasi za mabao 23 katika mechi 89 pekee katika michuano yote.

Huku Ujerumani ikiweka alama yake, Haaland ameingia kwenye rekodi nyingine nchini England ambako amefunga mabao 14 katika mechi kumi pekee, na sasa baba wa mshambuliaji huyo, Alf-Inge, amekiri kuwa anataka rekodi kama hizo kote Ulaya kabla hajatundika daruga zake.

"Nafikiri Erling anataka kupima uwezo wake katika kila ligi kubwa tano za Ulaya," alisema Inge.

"Anaweza kuwa na miaka miwili na nusu Ujerumani, miwili na nusu Uingereza, na kisha Hispania, Italia na Ufaransa.

"Hatujui kama itakuwa hivyo, lakini nadhani angependa kupima uwezo wake katika ligi kuu."

Baba yake Haaland pia alifichua kuwa, wakati wakizingatia mustakabali wake, waliweka pamoja orodha ya timu zilizokuwa zinamuwania na kuzichambua, huku City wakiibuka kinara.

"Kwenye orodha yetu, nadhani City ndiyo tuliiona kuwa timu bora," alifichua kwenye picha ambazo zilirekodiwa kabla ya uamuzi wa mwisho kufanywa."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,034,9

MECHI KALI
ARSENAL
VERSUS
TOTTENHAM
1 | 2.12
X | 3.50
2 | 3.10

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# JESUS AELEZA SABABU KUONDOKA MAN CITY



**LONDON, England**

GABRIEL Jesus amekiri kwamba alilazimika kuondoka Manchester City ya kocha Pep Guardiola majira ya joto baada ya kutoelewa umuhimu wake pale Etihad.

Mbrazil huyo alianza mechi 21 za Ligi Kuu msimu uliopita na mara nyingi alicheza mbele baada ya kuondoka kwa Sergio Aguero, akifunga mabao nane na kusaidia mengine nane.

Arsenal waliingia kwa nguvu wakati wa majira ya joto na kumfanya Jesus kuwa mshambuliaji wao mpya, akichukua nafasi ya Pierre-Emerick Aubameyang na tayari amefunga mabao manne na kuwaisaidia Washikabunduki hao kuwa kileleni mwa jedwali kwa ushindi mara sita katika mechi saba.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 ameonekana kuimarika msimu huu na alikiri kuwa sehemu yake ni kujihisi "huru" kaskazini mwa London chini ya Mikel Arteta, akiongeza kuwa alichoshwa na mtindo wa uchezaji kule City.

"Jambo lilikuwa jinsi (Guardiola) anaelewa soka na kile anachotaka," alisema Jesus akiiambia ESPN Brazil.

"Basi ilikuwa ni wewe kukubali au usikubali. Niliikubali kwa muda, lakini ilifika wakati niliposema: 'Nataka kitu kingine kwa ajili yangu.' Nilimshukuru, 'asante kwa kila kitu,' alielewa, na tukaendelea.

"Ni tofauti hapa Arsenal. Soka ni tofauti - wachezaji tofauti, njia tofauti za kucheza.

"Pale City, ilikuwa tofauti. Mshambuliaji hakugusa sana mpira, unaona hii kwa kutazama michezo.

"Nilizungumza sana na Arteta kuhusu staili ya Arsenal. Ananifahamu, namfahamu, nilielewa anachotaka kutoka kwangu. Sasa niko huru uwanjani, nikicheza mpira huku nikitabasamu na kujaribu kufanya yangu."

Jesus atashiriki katika mchezo wake wa kwanza wa dabi ya London Kaskazini leo Jumamosi wakati Arsenal watakapoikaribisha Tottenham Hotspur.

# Conte hana haraka na mkataba mpya

**LONDON, England**

ANTONIO Conte ametulia kuhusu hali ya mkataba wake kule Tottenham Hotspur, licha ya kwamba, mkataba wake wa sasa unamalizika mwishoni mwa msimu huu.

Ingawa Spurs wana chaguo la kumuongezea mwaka mmoja kwenye mkataba wa sasa wa Conte - ambao utaendelea hadi 2023, uvumi umeenea kwamba anaweza kurejea Juventus.

Akizungumza kabla ya Tottenham kuelekea kaskazini mwa London kwa wapinzani wao Arsenal, Conte alitaja ripoti kama hizo "zisizo na heshima", na Muitaliano huyo sasa amesema hakuna haraka kukubaliana na masharti mapya.



"Hakuna mkataba, hakuna chaguo, ikiwa klabu na meneja wanataka kufanya kazi pamoja, wataendelea kufanya kazi pamoja. Ikiwa hawataki kufanya kazi pamoja, wanamaliza," alisema Conte akiwaambia waandishi wa habari.

"Jambo muhimu zaidi kwangu ni kwamba ninafurahia sana kufanya kazi na Tottenham, na wachezaji hawa, haswa, na uhusiano na Daniel (Levy) na Fabio (Paratici) ni mzuri.

"Siko sawa na nadhani klabu ina furaha kuhusu hali hii. Sasa, jambo muhimu zaidi kwa sasa Tottenham na mustakabali wa Tottenham ni kupata matokeo bora zaidi (dhidi ya Arsenal)."

905,195/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 01/10/22 | 17:00 | Coventry vs Middlesbrough | 2.70 | 3.30 | 2.55 |
| 02. 01/10/22 | 17:00 | Fulham vs Newcastle | 3.04 | 3.39 | 2.27 |
| 03. 01/10/22 | 17:00 | Rotherham vs Wigan | 2.33 | 3.19 | 3.09 |
| 04. 01/10/22 | 17:15 | Getafe vs Valladolid | 2.44 | 3.03 | 3.08 |
| 05. 01/10/22 | 18:00 | Strasbourg vs Rennes | 2.92 | 3.36 | 2.32 |
| 06. 01/10/22 | 19:30 | Sevilla FC vs Atletico Madrid | 2.84 | 3.14 | 2.54 |
| 07. 01/10/22 | 19:30 | Werder Bremen vs Borussia Monchengladbach | 2.58 | 3.57 | 2.48 |
| 08. 02/10/22 | 14:00 | Lorient vs Lille | 2.92 | 3.42 | 2.30 |
| 09. 02/10/22 | 14:00 | Stoke City vs Watford | 2.38 | 3.18 | 3.03 |
| 10. 02/10/22 | 15:00 | Espanyol vs Valencia | 2.73 | 3.22 | 2.58 |
| 11. 02/10/22 | 16:00 | AJ Auxerre vs Brest | 2.67 | 3.36 | 2.52 |
| 12. 02/10/22 | 16:00 | Troyes vs Reims | 2.47 | 3.36 | 2.72 |
| 13. 02/10/22 | 16:00 | Sampdoria vs AC Monza Brianz | 2.31 | 3.29 | 3.04 |
| 14. 02/10/22 | 16:30 | Hertha BSC vs Hoffenheim | 2.97 | 3.56 | 2.21 |
| 15. 02/10/22 | 17:15 | Celta Vigo vs Betis | 2.45 | 3.29 | 2.84 |
| 16. 02/10/22 | 18:30 | Leeds vs Aston Villa | 2.59 | 3.43 | 2.59 |
| 17. 02/10/22 | 19:30 | Girona vs Real Sociedad | 3.19 | 3.14 | 2.31 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 01/10/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 3461 | Kansanshi Dynamos vs Green Eagles | 3.13 | 2.45 | 2.69 |
| 14:30 | 2914 | Arsenal vs Tottenham | 2.12 | 3.50 | 3.10 |
| 15:00 | 3091 | Cadiz CF vs Villarreal | 5.47 | 3.80 | 1.60 |
| 16:00 | 1306 | Zanaco vs Red Arrows | 2.74 | 2.50 | 2.99 |
| 16:00 | 1334 | Marines FC Gisenyi vs Rayon Sports FC | 4.42 | 3.09 | 1.82 |
| 16:00 | 1539 | Green Buffaloes vs Prison Leopards | 2.18 | 2.65 | 3.78 |
| 16:00 | 3187 | Bugesera FC vs Etincelles | 2.32 | 2.75 | 3.29 |
| 16:00 | 4869 | Napoli vs Torino | 1.57 | 3.96 | 5.21 |
| 16:00 | 4942 | Chambishi FC vs Forest Rangers | 3.00 | 2.56 | 2.66 |
| 16:00 | 5346 | Mukura vs Gorilla FC | 1.92 | 3.01 | 4.04 |
| 16:00 | 5920 | Namungo vs KMC | 2.08 | 2.90 | 3.64 |
| 16:00 | 5989 | Police FC Rwanda vs Gasogi United | 2.14 | 2.89 | 3.48 |
| 16:30 | 1565 | FK Khimki vs CSKA Moscow | 5.41 | 4.20 | 1.52 |
| 16:30 | 1848 | RB Leipzig vs VfL Bochum | 1.23 | 6.00 | 10.00 |
| 16:30 | 4338 | FC Koln vs Borussia Dortmund | 3.20 | 3.66 | 2.02 |
| 16:30 | 4404 | Eintracht Frankfurt vs Union Berlin | 2.22 | 3.25 | 3.10 |
| 16:30 | 5657 | VfL Wolfsburg vs Stuttgart | 2.34 | 3.30 | 2.85 |
| 16:30 | 5675 | SC Freiburg vs Mainz | 2.06 | 3.41 | 3.31 |
| 17:00 | 1084 | West Bromwich vs Swansea | 1.74 | 3.60 | 4.40 |
| 17:00 | 1711 | Bournemouth vs Brentford | 3.20 | 3.30 | 2.16 |
| 17:00 | 1861 | Fulham vs Newcastle | 2.90 | 3.30 | 2.31 |
| 17:00 | 1924 | Cardiff vs Burnley | 2.95 | 3.15 | 2.37 |
| 17:00 | 1987 | Liverpool vs Brighton | 1.34 | 5.01 | 7.41 |
| 17:00 | 2067 | Crystal Palace vs Chelsea | 4.21 | 3.51 | 1.79 |
| 17:00 | 2216 | ES Sahel vs US Tataouine | 1.77 | 3.09 | 4.71 |
| 17:00 | 2366 | Sheffield Utd vs Birmingham | 1.42 | 4.39 | 6.79 |
| 17:00 | 2682 | Southampton vs Everton | 2.13 | 3.25 | 3.30 |
| 17:00 | 2721 | Blackpool vs Norwich City | 3.95 | 3.50 | 1.85 |
| 17:00 | 2917 | Blackburn vs Millwall | 2.23 | 3.15 | 3.20 |
| 17:00 | 4414 | Reading vs Huddersfield | 2.18 | 3.20 | 3.25 |
| 17:00 | 5193 | Esperance Tunis vs CS Sfaxien | 1.50 | 3.48 | 6.86 |
| 17:00 | 5610 | Celtic vs Motherwell | 1.12 | 8.28 | 16.15 |
| 17:00 | 5773 | Sunderland vs Preston | 2.22 | 3.20 | 3.15 |
| 17:00 | 5973 | Bristol City vs QPR | 2.24 | 3.34 | 3.00 |
| 17:15 | 2131 | Getafe vs Valladolid | 2.28 | 3.02 | 3.33 |
| 17:30 | 2490 | FC Vizela vs Portimonense | 2.18 | 3.27 | 3.22 |
| 17:30 | 4075 | Cambuur vs PSV Eindhoven | 8.21 | 5.81 | 1.27 |
| 18:00 | 5263 | Strasbourg vs Rennes | 2.91 | 3.37 | 2.30 |
| 19:00 | 3748 | Inter vs Roma | 2.03 | 3.40 | 3.40 |
| 19:30 | 2349 | West Ham vs Wolverhampton | 1.89 | 3.40 | 3.90 |
| 19:30 | 4348 | Werder Bremen vs Monchengladbach | 2.51 | 3.56 | 2.50 |
| 19:30 | 5815 | Sevilla FC vs Atletico Madrid | 2.87 | 3.12 | 2.49 |
| 19:45 | 2567 | Groningen vs AZ Alkmaar | 4.60 | 3.60 | 1.71 |
| 21:00 | 1963 | Ajax vs GO Ahead Eagles | 1.07 | 9.84 | 21.08 |
| 21:45 | 2312 | Empoli vs AC Milan | 5.19 | 3.89 | 1.59 |
| 21:45 | 4800 | Brugge vs Mechelen | 1.49 | 4.43 | 5.63 |
| 22:00 | 1550 | Paris St Germain vs Nice | 1.20 | 6.57 | 11.55 |
| 22:00 | 2096 | Twente vs Vitesse Arnhem | 1.68 | 3.75 | 4.60 |
| 22:00 | 3512 | Mallorca vs Barcelona | 7.31 | 4.68 | 1.39 |
| 22:30 | 4954 | Vitoria Guimaraes vs Benfica | 7.45 | 4.63 | 1.38 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# WAZIRI MKUU MGENI RASMI SHIMIWI TANGA

**Na Cheji Bakari,Tanga**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika mashindano ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI) yatakayofanyika hapa Tanga.

Kwa mujibu ya taarifa kutoka SHIMIWI na ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Tanga, mashindano hayo ya siku 15 yataanza kutimua vumbi Oktoba leo na uzinduzi rasmi utafanyika Oktoba 5 katika uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga na yatahitimishwa Oktoba 15 mwaka huu.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omari Mgumba katika taarifa yake kwa umma kupitia mitandao ya kijamii na vyombo vya habari alisema: "Nawakaribisha katika mashindano ya michezo ya SHIMIWI ambayo kwa mwaka huu yatafanyika jijini Tanga na michezo hii itahusisha Wizara na Taasisi za kiserikali."

Kauli mbiu ya SHIMIWI mwaka huu ni: "Michezo hupunguza magonjwa yasiyoambukizwa na huongeza tija mahala pa kazi."

Kwa mujibu wa taarifa hizo, michezo itakayofanyika ni pamoja na soka, netiboli, kuvuta kamba, riadha, karata, drafti, bao pamoja na mbio za baiskeli.

Viwanja vitakavyotumika ni pamoja na Mkwakwani, uwanja wa shule ya sekondari Galanos, shule ya sekondari Popatlal, shule ya sekondari Tanga Ufundi,Polisi Chumbageni,shule ya Usagara,bandari pamoja na Tanroads.




Meneja Mkuu wa Surveyed Plots Company (Ltd) SPC, Neema Ally (kushoto) na Mkuu wa Kitengo cha ukusanyaji madeni wa kampuni hiyo, Zena Matondo (kulia), wakiwakabidhi hati za viwanja wanariadha, Aloyce Simbu, na Angelina Yumba, baada ya kampuni hiyo kuahidi kuwapa zawadi ya viwanja wanariadha wa Tanzania walioshika nafasi za juu katika mbio za Kilimanjaro Premium Lager Marathon 2022 yaliyofanyika Moshi mapema mwaka huu, wakishuhudia na Rais wa Riadha Tanzania, Silas Isangi. (wa pili kulia waliosimama) **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Kocha Mgunda aifungia kazi Dodoma Jiji

INATOKA UK. 32

yaliyojitokeza kwa wachezaji ambayo nitakwenda kufanyia kazi na mazuri niliyoyaona nakwenda kuyaboresha zaidi.

"Tunahitaji kufanya vizuri katika mechi zote zilizokuwa mbele yetu, kwa sasa naiangalia Dodoma Jiji ili tuweze kupata pointi tatu kisha tujiandae na mchezo wa kimataifa.

"Kikosi kipo vizuri wachezaji wana morali nzuri naamini nikiyafanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza tutakuwa vizuri," alisema Mgunda.

## Zanzibar yaruhusu ngumi

INATOKA UK. 32

204 ambao wamejikita katika mchezo wa ngumi, lakini walikuwa wakifanya mchezo huo kwa njia za kujificha.

Aidha alizitaja klabu zilizokuwa zikijishughulisha na mchezo huo ikiwemo ya Amani yenye mabondia 22, Mlandege yenye mabondia 47 pamoja na Wakojani yenye vijana 43 huku akimtaja bondia maarufu, Ashraf Suleiman ambaye kwa nyakati tofauti alikuwa akicheza Tanzania Bara.

"Mheshimiwa vijana wanaojishughulisha na mchezo huu wapo visiwani Zanzibar, lakini walikuwa wakifanya shughuli zao kwa njia ya kujificha kwa sababu mchezo wenyewe hauruhusiwi kwa mujibu wa sheria. Huu mchezo jamani ni maarufu duniani kote unaingiza kipato kikubwa na kuitangaza nchi," alisema Othman.

Mwakilishi wa jimbo la Kwahani, Yahya Rashid Abdallah alisema mchezo wa ngumi ni maarufu ambapo unaweza kuitangaza Zanzibar katika ramani ya utalii na kuwa kituo muhimu cha shughuli za maendeleo na kibiashara.

Alisema katika ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi imetaja umuhimu wa kuimarisha shughuli za michezo kwa maendeleo ya jamii na kiuchumi katika kuongeza ajira.

"Kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu la Kwahani naunga mkono kurasimishwa kwa mchezo huu ambao utakwenda kuitangaza Zanzibar ambayo ipo katika juhudi za kujitangaza katika ramani ya utalii duniani," alisema Abdallah.

# Michezo

Jumamosi Oktoba 1, 2022

Nipashe



UKURASA 30

## Jesus aeleza sababu kuondoka Man City



Wachezaji wa Simba wakijifua mazoezini. **PICHA: SIMBA**

# ZANZIBAR SASA YARUHUSU NGUMI

●●●Ni baada ya mchezo huo kupigwa marufuku na rais mwaka 1964 na sasa Baraza la Wawakilishi...

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Zanzibar imetangaza rasmi kuruhusu mchezo wa ngumi kuanza kufanyika visiwani humo baada ya kupigwa marufuku Januari 12 mwaka 1964 na rais wa kwanza, Abeid Amani Karume.

Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Tabia Maulid Mwita alitangaza uamuzi huo katika kikao cha baraza la wawakilishi, baada ya kupata maoni ya wananchi mbalimbali waliohojiwa na kupata baraka za Baraza la Mapinduzi.

Waziri huyo, alisema utafiti mdogo uliofanywa ambapo jumla ya wananchi 5,702 walihojiwa katika mikoa mitano ya Zanzibar na watu 3,614 sawa na asilimia 63.4 walitaka mchezo huo uruhusiwe.

Aidha alisema yamefanyika mahojiano mbalimbali kupitia vyombo vya habari ikiwemo redio pamoja na televisheni pamoja na vipindi yakibainisha wananchi kutoa maoni ya kukubali kuruhusiwa kwa mchezo huo.

Alifahamisha mara baada ya kukusanywa kwa maoni hayo waraka ulipelekwa katika baraza la Mapinduzi kwa vikao zaidi kuanzia Machi 24, 2022 ambapo Baraza la Mapinduzi liliridhia kuanzishwa kwa mchezo huo.

"Mheshimiwa Spika napenda niwajulishe wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba, Baraza la Mapinduzi limeridhia rasmi mchezo wa ngumi kuruhusiwa baada ya kuyapokea maoni ya Wananchi walioulizwa katika mikoa mitano ya Unguja," alisema Waziri huyo.

Alizitaja hatua zinazotarajiwa kuchukuliwa mara baada ya baraza la wawakilishi kuridhia mchezo huo ikiwemo kufanya usajili wa mchezo huo na kuanzishwa kwa klabu zitakazoshughulikia mchezo huo.

Baadhi ya wajumbe wa baraza la wawakilishi waliochangia hoja hiyo walikubaliana na maamuzi ya serikali kuhusu kuruhusu mchezo wa ngumi kwa ajili ya kuitangaza Zanzibar kiutalii.

Mwakilishi wa jimbo la Mpendae, Shaaban Othman ambaye aliwasilisha hoja hiyo mbele ya baraza la wawakilishi kuruhusiwa kwa mchezo wa ngumi mwaka jana, alisema amefurahishwa na uamuzi huo ambao umelenga kuinua vipaji vya vijana wa Zanzibar katika mchezo huo.

Othman alisema wapo vijana wapatao

INAENDELEA UK. 31

# Kocha Mgunda aifungia kazi Dodoma Jiji

**Shufaa Lyimo Na Hadija Mngwai**

KOCHA wa Klabu ya Simba, Juma Mgunda amesema anaelekeza akili zake kwenye mchezo wa Ligi Kuu kati yao na timu ya Dodoma Jiji FC utakaopigwa kesho Jumapili kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa.

Akizungumza na gazeti hili Mgunda alisema mazoezi na michezo ya kirafiki waliyoicheza Visiwani Zanzibar yamewajenga kwa kiasi kikubwa wachezaji wake.

"Mazoezi na michezo tuliyoicheza Zanzibar imewasaidia wachezaji wangu kuwaweka imara zaidi kuelekea kwenye mchezo wa Ligi Kuu pamoja na ule wa Kimataifa," alisema Mgunda.

Alisema anaupa umuhimu mchezo huo akiwa na lengo la kupata pointi tatu kwenye uwanja wa nyumbani.

Kocha huyo alisema wachezaji wote wanaendelea vizuri na kudai baada ya mchezo huo wataanza maandalizi ya safari kuelekea nchini Angola kucheza na De Agosto kwenye Ligi ya mabingwa Afrika.

Aidha Mgunda amesema michezo hiyo imempa kitu baada ya kubaini ubora na mapungufu ndani ya kikosi hicho.

Mgunda hadi sasa amesimamia kikosi cha Simba mechi tano ambapo hajapoteza mchezo hata mmoja dhidi ya Big Bullets ya Malawi mchezo wa Ligi ya mabingwa Afrika, ambapo alishinda michezo yote miwili nyumbani na ugenini jumla ya mabao 4-0.

Aidha mechi nyingine aliyosimamia ni ya Ligi Kuu dhidi ya Tanzania Prisons ambapo alishinda bao 1-0 kisha michezo ya kirafiki dhidi ya Malindi SC aliyoshinda bao 1-0 na kumalizia ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Kipanga FC.

Mgunda alisema kuwa, kupitia mechi mbili alizocheza za kirafiki ameweza kugundua baadhi ya mapungufu ambayo ataenda kuyafanyia kazi kabla ya kuivaa Dodoma Jiji kesho Jumapili.

"Mechi hizi nilizocheza nimeweza kubaini baadhi ya mapungufu

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >